

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Tatu – Tarehe 31 Januari, 2008

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 29

Uuzaji Pombe Kwenye Maduka ya Kawaida.

MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA aliuliza:-

Kwa kuwa siku hizi kumejitokeza mtindo kwa baadhi ya wauza maduka ya bidhaa za kawaida kuuza pombe kama vile bia, konyagi na kadhalika kwenye maduka yao:-

Je, Serikali inalifahamu jambo hilo na kama inalifahamu imechukua hatua gani dhidi ya wenye maduka hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Leseni za Vileo Na. 28 ya mwaka 1968 na marekebisho yake ya mwaka 2002, Sehemu III, Kifungu Na. 8, kinazungumzia aina 14 za leseni za vileo zinazopaswa kutolewa na Bodi ya Vileo. Aina hizo ni kama uuzaji wa pombe kwa jumla (*wholesale*) Baa au (*Retailer's on*) Grosari au (*Retailer's off*) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 11 cha Sheria hiyo kinamtaka muuzaji wa Grosari au (*Retailer's off*) kuhudumia mteja au kumuuzia mnunuzi wa pombe kwa kiasi chochote kisichozidi robo painti na si zaidi ya Galoni mbili (2) ya pombe kali kwa ajili ya matumizi yake nje ya eneo la duka hilo (nyumbani kwa mtumiaji). Kwa pombe isiyokuwa na vileo vikali, Sheria inamtaka muuzaji kuuza Galoni kumi na nne (14) ikiwa katika hali ya kufungwa (*sealed*) kwa matumizi ya nje ya duka hilo (yaani nyumbani.)

Mheshimiwa Spika, wenyе maduka yanayouza pombe, wanaruhusiwa kuomba leseni za kuuza pombe katika maduka yao kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa kwenye Sheria hii. Sheria hii haimruhusu mwenye leseni ya Grosari kumuuzia mteja na kunjwa kwenye eneo la duka lake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya II, kifungu cha 3 na 4 kimezipa mamlaka Halmashauri za Vijiji, Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji utoaji wa leseni za vimeo katika maeneo yao. Katika utoaji wa leseni ya aina yoyote ya vimeo, msimamizi mkuu ni Bodi ya Vileo ya sehemu inayohusika. Aidha, anayehusika moja kwa moja na ufuutiliaji na ukaguzi, ni Afisa Biashara wa Halmashauri kwa niaba ya Halmashauri husika. Tatizo linalojitokeza ni kuwa wenyе maduka ya kawaida ambaо wana leseni za kuuza vimeo wanakiuka taratibu za leseni zao wakati wa usiku kwa kuwaruhusu wateja wao kunywa katika maeneo ya maduka yao. Hili ni kosa na ikigundulika kuwa mwenye leseni anakiuka utaratibu anachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika Manispaa ya Ilala, kwa mwaka 2007 watu 130 walipatikana na makosa yafuatayo:-

Wateja kunywa pombe kwenye grosari, kuweka viti nje ya grosari, kuuza pombe kwa muda usioruhusiwa kisheria, kupiga mziki wa kelele. Kati ya watuhumiwa hao, 121 walitozwa faini na Manispaa kupata jumla ya shilingi 10,538,000/- na watu kumi walipelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba kuna baadhi ya maduka ya vyakula au bidhaa za kawaida yanayouza pombe na inachukua hatua kwa mujibu wa Sheria kama ilivyoelezwa hapo juu.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Sheria ya *The Intoxicating Liquours* kama sikosei ni ya mwaka 1968 ndiyo Sheria inayo-control unywaji wa vimeo, ni ya siku nyingi sana na kwa kweli kwa wakati huo Baa zilikuwa ni chache hali ambayo ni tofauti sana na sasa. Je, Serikali iko tayari kuleta Sheria hii hapa ili tuweze kuipitia na kutunga Sheria nyingine ambayo italingana na mazingira ya sasa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Sheria hii ilishapitiwa upya mwaka 2002. Kama kutakuwa na ulazima wa kurekebisha tena Sheria hii, nawaomba wadau mbalimbali walete mapendekezo ili ifanyiwe marekebisheso lakini kwa sasa sisi tunaona kwamba inafaaa. Hata hivyo, katika Manispaa mbalimbali au Majiji na mamlaka mbalimbali za Bodi za Vileo pia zimefanya marekebisheso mbalimbali kwa mfano upande wa faini, kwa sasa faini zinazotumika sio zile ambazo zilitolewa mwaka 1968 ambazo zimepitwa na wakati.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa bidhaa ndogondogo nyingi zinauzwa madukani ambazo zinatumika majumbani; na kwa kuwa watu wengi wana mazoea ya kuwatuma watoto kwenda dukani kununua bidhaa hizo, huoni kama kwa kuwatuma watoto wadogo kwenda kununua vinywaji vinavyoweza kuwalewesha ni kichocheo na wao kuiga mtindo huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, hairuhusiwi kunywa palepale kwenye Grosari mtu anaruhusiwa kununua na kwenda kunywea nyumbani kwake. Kwa hiyo, hii ni mojawapo ya kuzuia wale wanaokunywa pale ili wasiweze kuwasumbua wale wateja ambao wanakuja kununua zile bidhaa nyagine. Kwa hiyo, Sheria ipo ni suala la utekelezaji tu.

Na. 30

Tume ya Kero za Muungano

MHE. ALI SAID SALIM aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliunda Tume ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi ili kushughulikia kero kadhaa za muungano:-

(a) Je, mbali na Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, wajumbe wengine waliomo katika Tume hiyo ni akina nani?

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumiwa na Tume hiyo katika mikutano yake na ni mikutano mingapi imeshafanyika?

(b) Je, vikao vya Tume vinagharamiwa na nani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi ni matokeo ya maagizo ya Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoyatoa katika Semina Elekezi kwa Viongozi iliyofanyika Ngurdoto Arusha mwezi Machi, 2006 ya kuwataka Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kukutana ili kujadili jinsi ya kutatua vikwazo vinavyoukabili muungano wetu. Hivyo basi, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa hii sio Tume bali ni utaratibu wa Kiserikali uliowekwa kwa madhumuni ya kurahisisha utendaji wa kazi wa Ofisi ya Makamu kwa Rais inayosughulikia masuala ya Muungano. Baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mratibu wa vikao hivi ni Ofisi ya Makamu wa Rais. Vikao vinahusisha wajumbe kutoka pande zote mbili, kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Sekta za Muungano na kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni Mheshimiwa Waziri Kiongozi, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Sekta husika. Aidha, zinapoibuka hoja za masuala yasiyo ya muungano, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Sekta husika hushiriki katika vikao ili kutafuta ufumbuzi.

(b) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, inapokea hoja mbalimbali zilizoibuliwa kutoka pande zote mbili za Muungano na zinajadiliwa kwanza na Watendaji Wakuu wa sekta husika na baada ya hapo ndipo hoja hizo hujadiliwa katika vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi. Hadi hivi sasa, vimeshafanyika vikao viwili. Kwa sasa, Ofisi ipo katika maandalizi ya kufanya kikao cha tatu.

(c) Mheshimiwa Spika, vikao hivi vinagharamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Bajeti yake kwa kuwa ndiyo inayowajibika kuratibu masuala yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Baada ya majibu hayo ya Serikali, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, mimi sijui niite Tume au kikundi cha watu lakini kwa vyovyyote itakavyokuwa, mazungumzo hayo yanaongozwa na upande mmoja tu yaani upande wa Serikali. Sasa je, katika zama hizi za ukweli na uwazi, Serikali itakubaliana na mimi kwamba iko haja mbali ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi na upande wa Mawaziri kutoka Zanzibar na Bara kuongeza au kuwa na uwakilishi kutoka Kambi ya Upinzani kupata ufanisi zaidi?

La pili, kwa kuwa shughuli hii imeanza zamani na mazungumzo yanaendelea, je, hadi swali hili linajibowi sasa hivi, Serikali inaweza kutuambia ni mambo gani ya msingi yamezungumzwa na tayari yamepata ufumbuzi?

SPIKA: Sina hakika na hilo la pili kwa sababu litahitaji orodha ya masuala yote yaliyokubalika lakini kama upo tayari basi jibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, hii ni Kamati na si Tume na ni Kamati inayoshirikisha viongozi wa Serikali wa pande mbili baada ya kupokea maoni ya wananchi wa kawaida, Wabunge, Wawakilishi, vyama visivyo vya Kiserikali, Kambi ya Upinzani na kadhalika. Kwa hiyo, hii ni Kamati inayoshughulikia kutatua masuala ya muungano kwa kutumia Sheria na mambo mengine mbalimbali na hivyo lazima ifanywe na watendaji wa Serikali. Lakini kama hoja ya Mheshimiwa ni kwamba pengine Kambi ya Upinzani ina maoni, kila mara tupo tayari kuyapokea na tunaendelea kuyapokea kupitia Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo gani yamepata ufumbuzi, kama ulivyosema orodha ni ndefu sana na ninakumbuka katika hotuba yetu ya Bajeti, nilieleza maeneo zaidi ya sita ambayo yamefanyiwa kazi na yamepata ufumbuzi katika kipindi kifupi. Namwomba Mheshimiwa Mbunge apitie tena kitabu chetu cha Bajeti, ataona maeneo mengi yakiwemo suala zima la Tume ya Haki za Binadamu kufanya kazi zake Zanzibar, uvuvi katika Bahari Kuu, masuala ya uchimbaji na utafutaji wa mafuta na masuala mengine kadhaa ambayo tuliyaoorodhesha kikamilifu ambayo kwa kuwango kizuri yamefikia hatua muafaka na kuna ambayo tumeyamaliza kabisa.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wabunge ndiyo wawakilishi wa wananchi na kero hizi zimekuwa nyingi tangu mwaka 1972 baada ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Zanzibar na kwa vile orodha unayo, je, uko tayari sasa kutuletea orodha hiyo na sisi Wabunge tukazifahamu na hasa tukajua yale ambayo hayajapatiwa ufumbuzi?

SPIKA: Nadhani linakuwa kama swali jipya hili kwenye orodha au Waziri unajibu? Bahati nzuri, anayo majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, kama orodha anayokusudia ni orodha ya matatizo au kero zinazokabili muungano wetu, si kwamba ni orodha ambayo iko pale haibadiliki. Kila siku tunaendelea kupokea maoni ya wananchi katika maeneo ambayo wangependa yafanyiwe kazi ambayo yanaonekana ni kero. Kwa hiyo, hakuna orodha maalum iliyokuwepo bali kama nilivyosema awali tunasikiliza maoni kutoka kwa Wabunge, kutoka kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kutoka kwenye Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wananchi kwa ujumla tunayaingiza katika ratiba ya ajenda ya vikao vyetu ili hatimaye tupate ufumbuzi wa kudumu wa matatizo yanayoukabili muungano wetu. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie

Mheshimiwa Mnyaa kwamba kwa sasa tunayo orodha lakini orodha hiyo haibaki hivyo hivyo, kila mara tunaendelea kuongeza kutokana na masuala yanayoletwa na wananchi.

Na. 31

Mfumuko wa Shule za Sekondari na Upungufu wa Walimu.

MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH (K.n.y. MHE. BENITO W. MALANGALILA) aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Serikali kwa kushirikiana na wananchi, imejenga shule nyingi za sekondari nchini:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa upo upungufu mkubwa sana wa Walimu wa masomo ya sayansi hususani katika shule za Luhuya, Kasaya, Mninga, Mebungu, Nyololo na nyingine nyingi zilizopo katika Wilayani Mufundi gani na ni hatua gani zimechukuliwa kuondoa tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa mfumuko huo wa shule za sekondari unaweza kusababisha kushuka kwa ubora wa elimu je, ni mkakati gani umeandaliwa ili hali hiyo isitokee?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (a) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua upungufu mkubwa wa Walimu wakiwemo wa masomo ya sayansi. Hadi kufika Desemba 2007, Shule za Sekondari za Luhuya, Kasanga, Mninga, Mebugu, Nyololo na nyingine za Wilaya ya Mufundi, zilikuwa zinakabiliwa na upungufu wa jumla ya Walimu 113 wa masomo hayo. Katika mwaka 2006/2007, Walimu 40 wakiwemo 12 wa masomo ya Sayansi walipangwa katika Wilaya ya Mufindi. Kwa mwaka 2007/2008, Walimu 76 wakiwemo 32 wa masomo ya sayansi, walipangwa katika Wilaya hiyo. Wizara itaendelea kuwapanga Walimu wakiwemo wa masomo ya sayansi katika Wilaya ya Mufindi kadri wanavyopatikana. Tunaomba tushirikiane katika kuandaa mazingira mazuri ikiwa ni pamoja na mapokezi kwa Walimu wapya na kuendelea kujenga nyumba za Walimu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuhakikisha kuwa ubora wa elimu haushuki kutokana na ongezeko kubwa la shule za sekondari nchini, Wizara inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Wizara imeandaa mkakati wa kuongeza idadi ya Walimu wakiwemo wa masomo ya sayansi, kwa kuongeza nafasi zaidi katika vyuo vya Ualimu wa Stashahada.

(ii) Kupata Walimu wa Shahada kutoka Vyuo Vikuu na kufanya majadiliano na Vyuo Vikuu ambavyo havina vitivo vya Ualimu ili vianzishe.

(iii) Kuendelea na vipaumbele katika Bajeti vinavyolenga kuinua ubora wa elimu ambavyo ni; ujenzi wa nyumba za Walimu, ununuzi wa vifaa vya kufundishia, kujifunzia na kuimarisha mafunzo ya Walimu kazini (*In-service Training*).

MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Swali la msingi hapa ni tatizo la upungufu wa Walimu Mufindi lakini hali hiyo inajitokeza nchi nzima katika Majimbo yetu yote. Ninazo taarifa kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imesomesha Walimu na wako Walimu 2100 wamekosa ajira na *syllabus* zetu ni moja, je, Serikali ina mpango gani wa kuwachukua Walimu hao kutoka Zanzibar kuja kusaidia kufundisha Tanzania Bara?

Swali la pili, kama Serikali haina taarifa hiyo, nina uhakika kwamba taarifa Serikali inayo na kinachotakiwa ni utekelezaji, je, Serikali inasemaje kuhusu suala hili?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, Serikali ina taarifa kwamba Zanzibar wana Walimu wa ziada na tulishaongea na Waziri wa Elimu wa Zanzibar na tunalifanyia kazi na hasa kwa kuangalia kama tukiwachukua tutawatumia katika kiwango gani.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Katika swali la msingi, limezungumziwa suala jema la Serikali kushirikiana na wananchi katika kujenga shule nyingi za Sekondari nchini, jambo ambalo sote tunalipongeza. Kazi hii kubwa imefanywa na wazazi katika Halmashauri zote nchini kwa kujenga madarasa, kununua madawati na kadhalika. Lakini matokeo yake baada ya mtihani huu uliopita 2007, nusu tu ya wanafunzi nchi nzima ndiyo wamefaulu. Kwa hiyo, wazazi wale ambao wamejenga shule na kufanya juhudhi kubwa, watoto wao hivi sasa wako majumbani kwa sababu ya maksi mia kama ndiyo *cut off point* na inaelekea mtihani wa mwaka jana ulikuwa mgumu sana. Serikali inasema nini kuhusu uwezekano wa kufanya *standardization* au utaratibu mwingine wa kuweza kurekebisha jambo hili ili watoto hawa walioko nyumbani wakapata fursa ya kupata elimu hiyo ya Sekondari?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote na viongozi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kujenga shule za Sekondari. Tunawaomba muendelee kujenga kwa sababu bado tuna mahitaji makubwa.

Sasa kuhusu wanafunzi kufanya vibaya mwaka jana, wamefanya vibaya lakini si kiasi ambacho kimeelezewa kwa sababu waliofaulu ni zaidi ya asilimia 54 ambayo si mbaya sana ingawa tunasema ukilinganisha na mwaka uliopita ndiyo upungufu unaojitokeza pale. Lakini mimi nasema kwamba kwa taratibu za kielimu au taaluma ya ualimu, *standardization* haifanywi katika kipindi hiki, inafanywa wakati wa kusahihisha. Kwa hiyo, yote yale kama ni ya kurekebisha, hatua hiyo imeshapita wakati. Tunachokifanya sasa hivi Wizara ya Elimu, ni kuendesha utafiti, tena nimeona hata kikundi cha wataalam wetu wa Mkoa wa Dodoma, walikuwa wanafanya hiyo kazi kuangalia ni sababu gani zilizofanya hadi matokeo yakashuka. Kwa hiyo, sasa hivi nchi nzima zoezi hilo linafanya ili tutambue matatizo yaliyojitokeza halafu turekebishe ili mwaka unaofuata basi matokeo yawe mazuri zaidi. Moja ambalo tumeshaanza kulifikiria hata kabla ya utafiti, ni kusaidia Walimu kupitia *in-service training* ili tuone maeneo ambayo wanafunzi hawakufanya vizuri waweze kufanya vizuri mwaka unaofuata.

Ombi langu mimi badala ya kuomba pengine kushusha alama au nini, uzuri ni kwamba jinsi madarasa yanavyokaa yanazidi kukomaa na yanazidi kuwa mazuri zaidi mwaka kesho. Kitu kikubwa ni kuwaombeni kwamba tuangalie katika maeneo yetu jinsi gani ya kusaidiana na Walimu ili wafanye vizuri zaidi ili mwaka kesho matokeo yowe mazuri zaidi. Lakini napenda kumalizia kwa kuwashukuru tena kwa kujenga shule nydingi, ahsateni sana.

Na. 32

Kesi Zinazohusu Ubadhilifu wa Fedha

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA (K.n.y. MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI) aliuliza:

Kwa kuwa, kuanzia mwaka 2002, kila mwaka Bunge letu limekuwa likitoa kibali cha kuridhia ufutwaji wa upotevu wa fedha na vifaa, ambao pamoja na mambo mengine huchangiwa na wizi wa fedha, ubadhilifu na uhariufiga wa makusudi wa vifaa ndani ya Taasisi za Serikali:-

(a) Je, kwa kipindi cha mwaka 2002 – 2006, ni kesi ngapi ambazo Serikali ilishtaki kuhusiana na kadha ya wizi na ubadhilifu huo?

(b) Je, kesi hizo zilihusisha fedha kiasi gani?

(c) Je, ni kesi ngapi kati ya hizo ambazo Serikali ilishinda na ni kiasi gani cha fedha kilirejeshwa Serikalini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB) aliibuu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002 – 2006, Serikali ilishtaki jumla ya kesi 321 kuhusiana na kadha ya wizi na ubadhilifu.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi chote hicho, jumla ya Shilingi 4,403,305,623.90 zilihusishwa na wizi na ubadhilifu wa fedha na vifaa mbalimbali vya Serikali kama ifuatavyo:-

Mwaka 2001/2002, fedha taslimu shilingi milioni 434,407,200.05/-, vifaa vya thamani ya shilingi milioni 439,811,553.05/- jumla ni shilingi 874,218,753.10/-.

Mwaka 2002/2003, fedha taslimu shilingi milioni 725,476,025.33/-, vifaa vya thamani ya shilingi milioni 185,123,607.50/- jumla ni shilingi 910,599,631.83/-.

Mwaka 2003/2004, fedha taslimu shilingi milioni 392,149,464.30/-, vifaa vya thamani ya shilingi milioni 78,563,389.10/- jumla ni shilingi 470,712,853.40/-

Mwaka 2004/2005, fedha taslimu shilingi milioni 1,133,525 854.75/-, vifaa vya thamani ya shilingi milioni 323,110,817.57/- jumla ni shilingi 1,456,636,672.32/-

Mwaka 2005/2006, fedha taslimu shilingi milioni 555,661,482.25/-, vifaa vya thamani ya shilingi milioni 135,476,220.00/- jumla ni shilingi 691,137,712.25/-.

(c) Mheshimiwa Spika, kati ya kesi hizo, Serikali ilishinda kesi 14 na katika kesi hizo kiasi ambacho kilitakiwa kirejeshwe na wahusika ni jumla ya Shilingi 391,304,039.19.

Mheshimiwa Spika, potevu zinazoombewa kufutwa huwa zinajumuisha zenye kesi na zisizo na kesi. Potevu zenye kesi Mahakamani huwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 baada ya kesi zake kutolewa hukumu. Taarifa za potevu zilizopita, zinaonyesha kuwa imekuwa vigumu kwa Serikali kurejeshewa fedha zilizohusika katika ubadhilifu kwa sababu mbalimbali kama vile hukumu kutokumtaka mhusika arejeshe fedha/vifaa baada ya kifungo, wahusika kufariki, watuhumiwa kutoroka au kukosekana kwa ushahidi Mahakamani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kesi ambazo Serikali imeshinda, fedha hizo hurejeshwa kwa Afisa Masuhuli wa Fungu husika na anazikatia Stakabadhi ya Serikali na kuziingiza kwenye Akaunti ya Maduhuli ya Wizara, Idara au Mkoa husika na kila mwisho wa mwezi Hazina huhamishia kiasi hicho katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, fedha zinazopotea kwa ubadhilifu na uzembe ni jasho la Watanzania; Bunge lako Tukufu halioni kuendelea kuridhia kutoa kibali kwa ufutaji wa upotevu wa fedha kama hizi ni kuendelea kutoa mwanya kwa wahusika kuendelea *ku-misuse* fedha za wananchi?

(b) Kwa kuwa watumishi wa Serikali wamepewa dhamana kubwa ya kusimamia kikamilifu na kutunza fedha za wananchi kwa ajili ya maendeleo yao; Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kufuta kabisa mpango wa kuleta Miswada kama hii hapa Bungeni na badala yake isimamie kikamilifu kuhakikisha kwamba kila mhusika anasimamia kikamilifu na anaheshimu hela za wananchi kwa ajili ya kuboresha maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, ahsante!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba kufutwa kwa upotevu wa fedha ni kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge lako Tukufu ambayo ni Sheria ya Fedha ya mwaka 2001. Napenda ifahamike kwamba siyo Wizara ya Fedha kwa utashi wake ambayo inaleta kufuta fedha hizi katika Bunge lakini hii ni baada ya *PAC*, Kamati ya Hesabu za Fedha za Serikali kukaa pamoja baada ya *Controller and Auditor General* pamoja na *Accountant General* kupeleka maombi yao na kuelezea hali halisi ya upotevu wa fedha au maduhuli hayakukusanywa ili kutafutia ufumbuzi na kuweka vitabu vyya Serikali sawa. Kwa hiyo, hii ni Sheria ambayo imetungwa na Bunge lako Tukufu na Sheria ambayo ipo na hili ni baada ya kupata kibali cha Kamati yako ya *PAC* ndipo Wizara ya Fedha inaleta kibali hicho hapa katika Bunge lako Tukufu kuweka vitabu vyake vyya mahesabu sawa.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Zitto Kabwe na karibu tena Bungeni! (*Makofii*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ahsante! Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya wananchi dhidi ya matumizi mabovu ya fedha za umma na jana Serikali kuitia Wizara ya Fedha, wametangaza taarifa rasmi kwamba watu waliokopa fedha kuitia Mfuko wa *Import Support* waweze kuzirejesha ndani ya miezi mitatu badala ya kuwapeleka Mahakamani kwa sababu muda wao wa kulipa umekwishapita, je, Waziri atalihakikisha Bunge hili kwamba hatutaona mtu ye yeyote ambaye ameshindwa kulipa kuitia mkopo wa *Import Support* Bunge likiombwa liidhinishe kufutwa kwa deni hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):

Mheshimiwa Spika, *Import Support* utaratibu wake ni tofauti kabisa na fedha hizi ambazo zinapotea kwa kuitia akaunti zingine za Serikali. Kwa hiyo, hilo si fedha ambazo zinaweza kuletwa hapa tukasema kwamba zifutwe.

Huduma za Benki zetu

MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. TEDDY L. KASELA-BANTU) aliuliza:-

Kwa kuwa sasa hivi ziko benki nyingi kwa sababu ya soko huria; na kwa kuwa benki kama *NBC* haitozi gharama yoyote kwa kuweka fedha hata kwa mtu aliye na akaunti nao; na kwa kuwa benki ya *NMB* inatoza gharama tena kubwa kwa kuweka tu fedha kwenye akaunti yako kupitia kwenye branchi ambayo siyo yako:-

- (a) Je, kwa nini *NMB* inatoza gharama hizo?
- (b) Je, kwa nini *NBC* haitozi gharama hata kama huna akaunti na benki hiyo ila unaweka fedha kwa mtu ambaye ana akaunti huko?
- (c) Je, kuna mantiki gani kwa *NMB* kutoza gharama kwa mtu anayeweka fedha hasa ikizingatiwa kuwa ziko benki nyingine zenye mitandao mikubwa hadi vijijini lakini wanapoteza wateja?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi kupata huduma za kibenki kwa gharama nafuu. Hata hivyo, katika mfumo wa soko huria, mabenki yanatoza gharama kulingana na gharama zake za uendeshaji na vile vile ushindani uliopo katika soko. Suala la *NMB* kutoza gharama katika uwekaji wa hela kwenye akaunti isiyo yako au katika tawi lisilo lako na suala la *NBC* kutotoza gharama, ni la kiutendaji ndani ya benki ambapo Serikali haiwezi kuingilia. Hata hivyo, *NMB* walikwishaondoa sharti hilo kuanzia tarehe 1/12/2007.

Aidha, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania, imetoa waraka kwa mabenki yote nchini kuchapisha gharama wanazotoza katika vipeperushi na kuviveka katika kaunta za benki zao ili wateja na wananchi waweze kulinganisha na kuchagua benki zenye gharama nafuu ambayo wanaweza kuweka fedha zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na jitihada zake za kuboresha mazingira ya kiuchumi vijijini ili kuvutia mabenki mengi zaidi kupeleka huduma zake na hivyo kuongeza ushindani.

Uchimbaji wa Bwawa katika Kijiji cha Rungwa

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Mfuko wake wa Kuhifadhi Wanyamapor Tanzania (*TWPF*) ilitenga fedha tangu mwaka 2006 ili kujenga bwawa la maji kijiji cha Rungwa baada ya bwawa hilo kubomolewa na mvua:-

(a) Je, ni kitu gani hasa kinachelewesha ujenzi wa bwawa hilo wakati fedha zimetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo kwa takriban miaka miwili iliyopita na ni lini ujenzi huo utaanza?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuzidi kuchelewa kwa kazi hiyo kumeongeza zaidi gharama za ujenzi wa bwawa hilo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapor Tanzania (*Tanzania Wildlife Protection Fund – TWPF*), kutokana na makadirio yaliyotolewa na Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Manyoni, ilitenga shilingi 200,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa bwawa la maji katika Pori la Akiba Rungwa.

Hata hivyo, wakati mchakato wa kumtafuta mkandarasi wa kufanya ukarabati huo ukiendelea, ilibainika kuwa bwawa liliendelea kubomoka kwa kasi kutokana na mvua nyingi zilizokuwa zinaendelea kunyesha. Hali hiyo ilisababisha kiasi cha fedha zilizokuwa zimetengwa zisiweze kutosheleza ukarabati kwa ufanisi. Kufuatia hali hiyo, Wizara ililazimika kusitisha mpango wa kufanya ukarabati na kuamua kuwa bwawa hilo lijengwe upya. Baada ya tukio hili, Wizara ilishauriana na Wilaya ya Manyoni ili Mhandisi wa Maji atengeneze makadirio ya ujenzi wa bwawa hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, kufuatia mashauriano hayo, Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Manyoni alifanya makadirio ya kujenga bwawa hilo. Makadirio hayo yalifikia shilingi 417,000,000/=. Kazi ya ujenzi wa bwawa upya inatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2008/2009. Bodi ya Mfuko imeona kuwa ujenzi wa bwawa hilo unahitaji muda wa kutosha kwa kufanya utafiti kuhusiana na eneo bwawa litakapo jengwa, masuala ya udongo, haidrojia ya eneo hilo, tathmini ya athari ya mazingira pamoja na utalaamu wa kihandisi utakaohitajika kukidhi ujenzi wa bwawa la kudumu. Ili watumishi wa Pori la Akiba la Rungwa na wananchi wa kijiji cha Rungwa wasiendelee kukosa huduma ya maji, Wizara inatarajia kutumia shilingi 100,000,000/= kwa ajili ya uchunguzi wa

upatikanaji wa maji na kuchimba visima. Mchakato wa ujenzi wa visima vitatu upo katika hatua za mwisho ikiwa ni njia ya muda mfupi ya kuwapatia maji watumishi na wananchi wa Rungwa wakati utaratibu wa kujenga bwawa jipyga ukiendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wa muda mfupi (*short term vision*), ni kweli kuwa kucheleweshwa ujenzi wa bwawa kutaongeza gharama za ujenzi. Hata hivyo, tunaamini gharama zitakazoongezeka ni sehemu ndogo tu ya fedha zitakazotumika kujenga bwawa upya. Gharama hizo zitafidiwa na ubora na uimara wa bwawa litakalojengwa kwa kuzingatia misingi na kanuni za uhandisi wa ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji.

Na. 35

Wizi na Usafirishaji wa Nyara za Serikali

MHE. HAFIDH ALI TAHIR aliuliza:-

Kwa kuwa mwezi Julai, 2007 kilitoka tendo la kashfa la kusafirishwa kwa Nyara za Taifa zenye uzito wa tani tano ambazo zilitolewa *Ivory Room* kinyume na utaratibu na kukamata nchini Taiwan:-

- (a) Je, ni akina nani walihusika katika kuiba na kusafirisha Nyara hizo kwenda nchini Taiwan?
- (b) Je, Serikali imechukua hatua gani juu ya jambo hilo?
- (c) Je, Serikali inafanya juhudhi gani za kurudisha Nyara hizo za mabilioni ya fedha hapa nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, *Hajat*, majibu! (*Makofu/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Wizara yangu ina taarifa ya tukio la kukamatwa meno ya tembo tani tano katika Bandari ya Kaohsiung nchini Taiwan mwezi Juni, 2006. Mpaka sasa hakuna uthibitisho kwamba nyara hizo zimetokea Tanzania ingawa uchunguzi unabainishwa kuwa zilipitishwa kwenye Bandari ya Tanga, Tanzania kwa lengo la kupelekwa Manila, Ufilipino. Kuna watuhumiwa saba ambao kesi dhidi yao kuhusiana na meno haya inaendelea.

(b) Kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali kufuatia taarifa za kukamatwa kwa meno hayo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia hususan kitengo cha Polisi wa Kimataifa pamoja na Kikundi Kazi cha Mkataba wa Lusaka chenye Makao Makuu Nairobi – Kenya, tumefuatilia taarifa hiyo, tumefanya upelelezi na kuweza kufungua kesi dhidi ya watuhumiwa. Kesi hiyo dhidi ya watuhumiwa saba ni ya kuhujumu uchumi *EC No. 2/2006* ya tarehe 15/09/2006 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Tanga.

(c) Wizara yangu kwa kushirikiana na Polisi toka kitengo cha *Interpol* na Kikundi Kazi cha mkataba wa Lusaka ilituma wataalam wa upelelezi nchini Taiwan kufuatilia suala la kesi hii tarehe 28/02/2007. Maafisa hao walifanya majadiliano na Serikali ya Taiwan na kukubaliana kuwa nyara husika zirejeshwe Tanzania. Serikali inaendelea kukamilisha taratibu na matakwa ya Mkataba wa Biashara ya Kimataifa ya Wanyama na Mimea iliyo Hatarini Kuteweka kurejesha nyara hizo nchini ili zitumike kama vielelezo vyta kesi ya uhujumu uchumi *EC No. 2/2006*.

Mheshimiwa Spika, alipokuwa nyara hizo zilisafirishwa kupitia Bandari ya Tanga – Tanzania, bado haijathibitisha kama nyara husika zinatokana na tembo wa Tanzania kwa sababu upo uwezekano wa nyara hizo kutokea nchi jirani zenye tembo au zinazofanya biashara ya meno ya tembo ambazo hutumia Bandari za Tanzania kusafirisha bidhaa zao. Ili kuthibitisha hili, uchunguzi wa kisayansi unafanyika na Idara ya Wanyamapori na Samaki (*Wildlife and Fisheries Services*) nchini Marekani kwa kushirikiana na Lusaka *Agreement Task Force (LATF)* ili kuthibitisha meno hayo yametokana na tembo wa nchi gani ya Kiafrika.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake kwa swali langu Na. 35 lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu amesema kwamba Serikali ya Tanzania haijathibitisha kwamba nyara hizi ni za Tanzania, lakini hapo hapo anatuambia kwamba kuna watu saba wako Mahakamani; Sasa hao watu walioko Mahakamani walikamatwa kwa kesi gani wakati haijathibitishwa kwamba hizi nyara ni za Tanzania? Wakati huo tusisahau kwamba kesi hii ni ya kuhujumu uchumi, je, hao waliokwenda Mahakamani ni Watanzania au wananchi wa nchi gani?

(b) Pia katika jibu lake anasema kwamba haijathibitishwa kwamba nyara hizo pia ni za Tanzania, lakini Serikali imeomba nyara hizo zirudishwe Tanzania; zinarudishwaje Tanzania wakati mali si yetu? Hapa hakuna neno la siri ambalo limefichwa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina bandari ambazo zinatumwiwa na mataifa ambayo hayana bandari yanayojulikana vyema na Bunge hili Tukufu na ambayo nayo yana ndovu katika nchi zao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, labda utatusaidia baadaye katika msamiati wa mnyama huyu ili kusiwe na utata kama tumwite ndovu au tembo. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Mwite ndovu, inapendeza zaidi!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hafidh Ali ameuliza kama haijathibitishwa tembo hawa ni wa Tanzania au kwingineko kwa nini kesi imefunguliwa?

Mheshimiwa Spika, uthibitisho huu utafanywa kisayansi kama ambavyo unachunguzwa katika maabara za Ki-Marekani; na uthibitisho huo utapelekwa Mahakamani kama ushahidi ili tujue kwamba tembo hawa wanatoka wapi. Ninaomba Bunge lako Tukufu na Watanzania wengine tuvute subira wakati Mahakama inaendesha kesi hii ili hatimaye tujue ni kitu gani hasa kilitokea.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya tukio hilo, Serikali imefanya uhakiki (*Audit*) wa meno yote ya tembo ambayo yako *Ivory Room* na wakati huu sasa ripoti hiyo inatengenezwa na itakapokuwa tayari, basi tutawenza kujuu hasa hali halisi ya stoo yetu ikoje.

Na. 36

Shamba la Ng'ombe la Mabuki

MHE. BUJIKU P. SAKILA aliuliza:-

Kwa kuwa tangu shamba la ng'ombe la Mabuki lianzishwe zaidi ya miaka ishirini iliyopita, limeshindwa kuwabadilishia wengi wa wafugaji na wachungaji wanaolizunguka shamba hilo utamaduni wa ufügaji, uchungaji na aina ya ng'ombe waliokuwa wanafuga kabla ya kuanzishwa kwa shamba hilo licha ya mawazo mazuri na nia njema ya waanzilishi wa shamba hilo:-

(a) Je, hiyo si ishara tosha kuwa malengo mahsusini ya kuanzishwa kwa shamba hilo yameshindwa kufikiwa kikamilifu hivyo ibuniwe mbini mpya mbadala ya kutekelezwa ili kufikia malengo yaliyotarajiwa?

(b) Je, kuna sababu zipi za msingi zilizopo zitakazoendelea kuishawishi Serikali isianze kufikiria kwa makini wazo la kubadilisha matumizi ya shamba hilo ili kujenga Uwanja wa Ndege mkubwa wa Kimataifa ambao pamoja na shughuli za Uwanja wa Ndege wa Kimataifa utawenza pia kuhudumia vizuri Jiji la Mwanza, Mji wa Shinyanga, Mji Mdogo wa Ngudu, Misungwi – Maswa, Magu, Sengerema na Geita na Miji mingine mingi inayolizunguka Ziwa Victoria?

(c) Je, Serikali haioni kuwa licha ya juhudhi za mara kwa mara za kukarabati na kupanua Uwanja wa Ndege Mwanza jambo ambalo kwa baadaye litakuwa gumu na la gharama kubwa lifanye uamuzi mapema wa kuligeuza shamba hilo kuwa Uwanja wa Ndege ili kuliokoa Taifa kutafuta na kupata eneo kubwa la kutosha ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa kwa gharama kubwa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shamba la ng'ombe la Mabuki lilianzishwa miaka 36 iliyopita kwa lengo la kuzalisha ng'ombe wa maziwa na kuwasambaza kwa wafugaji kwa bei nafuu. Aidha, shamba hilo linatumika kwa utafiti wa mifugo baada ya kufungwa kwa shamba la Malya huko nyuma. Shamba hili hutumika pia kutoa mafunzo kwa wafugaji. Shamba la Mabuki linamilikiwa na Serikali kuptitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na mpaka sasa limezalisha na kusambaza mitamba zaidi ya 7,500, Maksai zaidi ya 7,250 na madume bora 250 kwa kipindi hicho cha miaka 36 tangu mwaka 1972 shamba lilipoanza uzalishaji chini ya Serikali. Mifugo hii imesambazwa kwa wafugaji wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Mikoa mingine ya Tanzania Bara na Visiwani. Wafugaji waliopata mifugo hiyo wamefaidika sana na uboreshaji wa mifugo ikiwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa maziwa. Kwa sehemu kubwa na kulingana na uwezo wa Serikali kifedha, malengo mengi na mahsusini ya kulianzisha shamba hili yamefikiwa.

Mheshimiwa Spika, mipango ya baadaye ni kuongeza shughuli za utafiti na mafunzo ambazo zitakuwa sambamba na uzalishaji wa mitamba. Utafiti na mafunzo yatakayotolewa na shamba la Mabuki pamoja na uzalishaji wa mitamba bora utawasaidia wafugaji wetu ili waweze kuongeza ubora wa mifugo yao na uzalishaji. Lengo la shamba kwa kila mwaka ni kuzalisha mitamba 500, madume bora 400 na maksai 100. Aidha, ikumbukwe kuwa shamba la Mabuki ni shamba pekee linalozalisha mitamba na madume bora, vilevile ni kituo pekee cha utafiti wa mifugo na mafunzo katika eneo la Kanda ya Ziwa. Hivyo, ni mhimili wa maendeleo ya sekta ya mifugo katika kanda hiyo na nchi nzima kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shamba hilo hadi kufikia sasa limeshasambaza ng'ombe zaidi ya 15,000 (ambapo mitamba ni 7,500, Maksai ni 7,250 na madume bora 250) kwa wafugaji wadogo wadogo nchini, ni dhahiri kwamba limechangia ufügaji wa ng'ombe wa maziwa nchini. Hii ni sababu tosha ya kuliendeleza shamba hili kwani linawawezesha wafugaji kubadili aina ya mifugo yao na kupata mbegu bora chotara kwa ajili ya uzalishaji mkubwa zaidi. Kanda ya Ziwa na maeneo mengine yenye ukame hayana chanzo kingine kikubwa cha mifugo bora kama Mabuki. Hivyo haitakuwa busara kuwaondolea wafugaji chanzo hicho cha mifugo bora kwa kubadilisha matumizi ya ardhi na kujenga uwanja wa ndege.

(c) Mheshimiwa Spika, siyo lazima kufikiria kubadilisha matumizi ya ardhi ya shamba la mifugo la Mabuki ili kujenga uwanja wa ndege mkubwa zaidi wa uliopo sasa pale Mwanza. Hii ni kwa sababu Mkoa wa Mwanza na Mikoa ya jirani kama Shinyanga, kwa bahati nzuri ina maeneo mengi makubwa na tambarare ambayo yanafaa kujengwa uwanja wa ndege mkubwa.

MHE. BUJIBU P. SAKILA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

(a) Kabla shamba hili halijaanzishwa, wako wananchi ambaao walihamishwa kutoka eneo hilo na eneo hilo liliwekewa uzio, kwa hiyo ikawa siyo rahisi kwa wafugaji walio karibu kuingia kwenye shamba hilo. Sehemu nyingi za eneo hilo sasa hivi hazina uzio na wananchi wengi sana sasa hivi kwa bahati mbaya ikitokea ng'ombe wao wakiingia kwenye shamba hilo, kuna faini ya shilingi 3000/= hadi 5000/= kwa kila ng'ombe ambayo mimi naona ni kama kuwaongezea umaskini watu wa eneo hilo; je, Wizara iko tayari sasa kurudishia uzio huo?

(b) Chini ya mpango shirikishi, wananchi wetu wangependa angalau kushirikishwa kuelezwu hasa ni mambo gani yanayoendelea katika shamba hilo; je, Serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wananchi wa Misungwi na Kwimba angalau waweze kuelewa kitu gani kinachotokea katika eneo hilo ili waweze kunufaika haraka zaidi kuliko watu wa maeneo mengine kama Mtware? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, Wizara ina mpango wa kuweka uzio katika eneo la shamba la Mabuki ili kusudi wananchi waweze kuona vizuri zaidi mipaka hiyo ambayo walio wengi hata hivyo wanaifahamu.

Mheshimiwa Spika, pili, wazo la ushiriki wa wananchi, kusema kweli tunalisisitiza. Nitumie nafasi hii kutoa wito kwamba wananchi wanakaribishwa wakati wote kuja kutoa maombi yao ya kupewa kozi za aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na kununua mitamba kwa bei nafuu ili waweze kuboresha mifugo yao.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali dogo kuhusu shamba hili la Mabuki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka utafiti katika shamba hili lakini kwa sababu hili shamba limezungukwa na wananchi wafugaji wa eneo hilo, kwa nini sasa Serikali isingeweka mkakati maalum ili wasiingiliane na wananchi wanaolisha kwenye shamba hilo, ikashiriki kuwasaidia hata kuwachimbia malambo pembezoni ili wasiwe wanaingiliana na shamba hili?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa pongezi kuhusu suala la utafiti.

Pili, kuhusu suala la uchimbaji wa malambo, Serikali ina Mpango mkubwa kabisa wa Maendeleo ya Kilimo Wilayani (*DADPS*). Ninatoa wito kwa wananchi wa Mabuki na Misungwi, Wilaya ya Misungwi pamoja na Mkoa wa Mwanza na Wilaya zote nchini, waweze kuchangamkia suala la kuibua miradi itakayopelekea kuchimba malambo kwa ajili ya kupata maji ya mifugo. Pesa zipo, suala tu ni kuhakikisha kuwa wananchi wanasaidiwa ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya mifugo yanazingatiwa ipasavyo ili kusudi tuweze kuboresha mifugo yetu nchini.

Na. 37

Kiwanja cha Michezo cha Memorio – Moshi

MHE. PHILEMON NDESAMBUTO aliuliza:-

Kwa kuwa ni Sera ya Serikali kwa sasa kufufua Michezo, lakini bila viwanja hatuwezi kuwa na michezo, na kwa kuwa katika Manispaa ya Moshi, kiwanja cha Memorio ambacho ndicho kiwanja pekee cha michezo kwa Mkoa wa Kilimanjaro lakini kimegeuzwa kuwa soko na kwa hivyo vijana wa Moshi kwa sasa hawana kiwanja cha Michezo:-

(a) Je, Serikali kupitia Manispaa ya Moshi kukigeuza kiwanja hiki kuwa soko, haipingani na Sera ya Serikali ya kufufua michezo?

(b) Je, uongozi wa Manispaa ya Moshi ilikosa sehemu nyingine ya kuweka soko mpaka kugeuza kiwanja cha michezo kuwa soko?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. JOEL N. BENDEREA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini kwamba kukigeuza kiwanja cha MEMORIO kilichopo Mjini Moshi kuwa soko ni kwenda kinyume na Sera yetu inayolenga kufufua na kuendeleza michezo hapa nchini.

Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kuwa Sera ya Serikali kwa sasa ni kufufua na kuendeleza michezo na viwanja ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo hayo. Hatua iliyochukuliwa na Manispaa ya Moshi ya kuwaweka wafanyabiashara ndani ya eneo la uwanja huo ni ya mpito.

(b) Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Moshi inakabiliwa na ufinyu wa maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii. Kwa hivi sasa eneo la Manispaa lina ukubwa wa kilomita za mraba 58 tu kukiwa na wakazi wapatao laki moja na sabini elfu(170,000)

Hali hiyo iliifanya Halmashauri ya Mjini Moshi kuitia vikao vyake vya kisheria kuamua kuwaondoa wafanyabiashara ambao walikuwa wamevamia viwanja katika maeneo mbalimbali ambavyo vilitakiwa kuendelezwa na kuwaweka kwa muda kwenye uwanja wa MEMORIO wakati jitihada za kuwapatia eneo la kufanya biashara zikiendelea.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa Mheshimiwa Mbunge atashirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Moshi kuweza kuchukua hatua za kusaidia kulitafutia ufumbuzi suala hili kuitia vikao vya kisheria ambapo yeze ni mmoja wa Madiwani wa Manispaa hiyo.

MHE. SUZAN A. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba tatizo hilo ni la mpito, je Serikali sasa ina mikakati gani ya makusudi kusaidia wananchi wale ili tatizo hilo liishe?

(b) Kwa kuwa kumekuwepo na taarifa za kipingana kuhusu matumizi ya uwanja wa mpira wa Nyamagana kule Mwanza Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu uwanja huo kwa sababu tulipata taarifa kwamba wanataka kujenga hoteli?

SPIKA: Nadhani swali la pili linaleta kitu kipyka kabisa kuhusu mgogoro wa ardhi kule Mwanza, huo ni mgogoro, kwa hiyo ninaomba ujibu swali la nyongeza la kwanza na hilo la kuhusu Nyamagana Mheshimiwa anaweza kulileta tena kwa muda muafaka ili likaweza kujibiwa.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. JOEL N. BENDERA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba tatizo la uwanja wa Moshi MEMORIO ni tatizo ambalo linaweza kutatuliwa na Halmashauri yenyeze ya Manispaa ya Moshi na ndiyo maana nikasisitiza kwamba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Madiwani wanao uwezo wa kukaa na kulitatua tatizo hili. Halmashauri zote masuala ya viwanja ni wao wenyeze wanaohusika katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kutoa wito kwa Halmashauri zote katika nchi yetu kwamba suala la viwanja vya michezo walipe uzito kwa sababu bila ya kuwa na viwanja vya michezo hakuna maendeleo ya michezo. Kwa hiyo, naomba sana wasibadilishe matumizi ya viwanja kufanya vitu vingine ama kutokuviendeza, huu ni wakati wa kusimamia masuala haya ili yaende vizuri.

Na 38

Kuwaongezea Ujuzi Waandishi wa Habari

MHE. JANETH M. MASSABURI Aliuliza:-

Kwa kuwa Waandishi wa Habari wamekuwa ni sehemu kubwa ya kusaidia kuwaelimisha wananchi jinsi ya kuondoa umasikini na kujiletea maendeleo yao na pia wito wa Serikali kujiunga na Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na kwa kupitia vyombo vya habari kuufahamisha umma majanga mbalimbali yanayotokea:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaongezea ujuzi Waandishi wa Habari wa vyombo vya umma na vya binafsi kwa kuwapeleka nje ya nchi kama Marekani, Uingereza, China (*short course*) ili wajenge uwezo zaidi?

(b) Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo kutasaidia kuwajengea uzalendo na uwezo mkubwa zaidi wa kuipenda kazi yao na kuendeleza kazi yao vizuri?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. DANIEL N. NSWANZUGWAKO) Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na vyombo vya habari vya umma na watu binafsi, imeandaa programu ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005. Ilani hiyo inaitaka Serikali kutoa mafunzo kwa Waandishi wa Habari yanayolenga kutoa Elimu ya Juu ya Uandishi wa Habari. Majukumu wa Wizara yangu chini ya Programu hii ni kuratibu upatikanaji wa misaada kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya habari kuandaa *programme* ya mafunzo kwa Waandishi wa Habari wanaofanya kazi kwenye vyombo vyao. Mafunzo hayo yanaweza kufanyika hapa hapa nchini kwenye Vyuo vyetu Vikuu vinavyotambulika kama vile Chuo Kikuu cha Tumaini, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha St. Augustine kule Mwanza.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, mafunzo yatakayotolewa kwa Waandishi wa Habari yatasaidia kuwajengea uwezo mkubwa wa

kuipenda na kuendeleza kazi yao vizuri zaidi na kuzingatia maadili na uzalendo kwa nchi yetu.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa Vyombo vya Habari hapa nchini vimeshirikiana na Serikali katika kuhamasisha umma kushiriki katika maendeleo kwa mfano Mkoa wa Dar es Salaam tumefanikiwa sana kushirikiana na Vyombo vya Habari tukapata kiwango kikubwa katika kuchangia ujenzi wa madarasa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha sekta ya habari kwa mwaka 2007/08 na hasa katika maendeleo vijijini?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. DANIEL N. NSWANZUGWAKO): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Vyombo vya Habari vimeshirikiana na Serikali kwa karibu sana, vimeshirikiana na wanajamii wengine kwa karibu sana katika jitihada za kuondoa umaskini na hata hili la michango ambalo Mheshimiwa Janeth Massaburi analizungumza.

Kuhusu kuboresha sekta hii ya habari kwa mwaka 2007/08, ni kama ambavyo nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba tunayo *programme* maalumu ambayo sisi Wizara kazi yetu kubwa itakuwa ni kuratibu *programme* hiyo na *programme* hiyo itajikita katika utoaji wa mafunzo ndani ya nchi na nje ya nchi yetu. Kwa hiyo, nisisitiza tu kwamba Serikali kwa ujumla wake inathamini sana mchango wa Vyombo vya Habari na mwaka 2007/08 utakuwa ni mwaka ambao utakuwa na matumaini makubwa sana kwa Vyombo vyetu vya Habari hasa katika eneo hili la mafunzo.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ni wamiliki wa Vyombo vya Habari wawe na *programme* zao wenye katika maeneo yao na kwa kufanya hivyo wataboresha sekta hii na kuboresha na kuongeza ujuzi kwa Waandishi wa Habari na Mwandishi wa Habari mwenye ujuzi mkubwa zaidi ni dhahiri atakuwa mzalendo zaidi kwa sababu atakuwa anaandika kitu ambacho anakifahamu vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine tuendelee kushirikiana na Vyombo vya Habari katika kuendeleza juhudhi hizi za kusaidia jamii yetu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na sahihi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba uniruhusu kwa niaba ya Serikali kumpongeza sana Mheshimiwa Bwana Reginald Mengi, Mwenyekiti wa IPP kwa kupewa Tuzo, jana na Marekani ya (*Martin King Junior*). (*Makofit*)

Bwana Mengi tunajua kwamba amesaidia sana jamii katika mambo mbalimbali ya kuimarisha mazingira, masuala ya kusaidia Walemvu, Vyombo vyaa Habari vyake vimesaidia kuelimisha umma lakini zaidi kusaidia kutibu vijana wenye matatizo ya moyo nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu liungane na Serikali kumpongeza Bwana Mengi na Waswahili husema “mcheza kwao hutunzwa”, nafikiri Bwana Mengi, anastahili kutunzwa, hongera Bwana Mengi. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ni jambo zuri kwa Serikali kuwatambua Watanzania wanaochomoza katika mambo mbalimbali.

Na. 39

MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

MHE. DAMAS P. NAKEI aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya Mfuko wa Afya ya Jamii hauonyeshi mafanikio ya kuridhisha na kwa muda mrefu mfuko huo umekosa mwamko:-

Je, Serikali inasema nini juu ya hiyo Sera yake?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII – (MHE. DR. AISHA O. KIGODA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Eng. Damas P. Nakei, Mbunge wa Babati Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii (*Community Health Fund*) unaolenga kuwashirikisha wananchi katika uchangiaji, uendeshaji na usimamizi wa huduma za afya ulinzi kwa majaribio Wilayani Igunga ulianza mwaka 1996.

Serikali kupitia Wizara yangu, imefanikiwa kuufanya Mfuko wa Afya ya Jamii ukubalike nchi nzima. Hadi kufikia Desemba 2007, Halmashauri zote za Wilaya zilikuwa zimeridhia Sheria Ndogo ya Mfuko wa Afya ya Jamii. Tayari Halmashauri zaidi ya 74 zimekwishazindua mpango huu na kati ya hizo Halmashauri 30 zimeawezesha wananchi wao kuchangia zaidi ya shilingi milioni 800 kwa miaka miwili 2005/06/07. Katika kipindi hicho, Wizara imeweza kuchangia Mfuko wa Afya ya Jamii katika Halmashauri hizo kupitia Mpango wa Tele kwa Tele kiasi cha shilingi milioni 800 sawa na michango ya wananchi waliojiunga.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Mfuko wa Afya ya Jamii yamebainika wazi katika kuchangia na kuboresha huduma za afya katika Halmashauri mbalimbali.

Maeneo yaliyoonyesha mafanikio ni pamoja na:-

Kuboreka kwa upatikanaji wa dawa muhimu;

Kuimarika kwa sauti ya wananchi kudai huduma bora pale inapotokea mapungufu;

Kuundwa kwa Bodi na Kamati Shirikishi za Afya ili kuimarisha umiliki wa wananchi wa huduma za afya katika maeneo yao;

Kufanyika ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma;

Familia maskini zimekuwa zikipewa kadi za uanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii bila wao kulipia;

Wadau mbalimbali kuunga mkono jitihada za Halmashauri katika kuboresha huduma za afya kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii; na

Nchi nyingine kama vile Msundi, Rwanda, Kenya na Zambia kuja kujifunza kwetu jinsi ya uanzishaji na utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa maelezo hayo, napenda kumuarifu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba kwa ujumla utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii, unaonyesha mafanikio ya kuridhisha na mwamko upo. Hata hivyo, kuna maeneo machache ikiwemo Babati ambako utekelezaji wa mpango huu hauridhishi. Kwa mfano katika kipindi cha 2002/2006, Halmashauri ya Wilaya ya Babati iliweza kukusanya kiasi cha milioni 7.5 ikiwa ni kiwango kidogo sana ikilinganishwa na Mbulu (jirani yake) ambayo kwa kipindi hichohicho iliweza kukusanya jumla ya shilingi milioni 84.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kuendelea kushirikiana na Halmashauri zao katika kuwashamasisha wananchi kuijunga na kuchangia Mfuko huu wa Afya ya Jamii. Aidha, Wizara yangu itaendelea kusimamia kutathmini na kutoa ushauri wa kitaalam juu ya utekelezaji wa Mfuko huu katika Halmashauri zote.

MHE. DAMAS P. NAKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya swali la nyongeza na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili:-

(a) Kwa kuwa hapa nchini kuna zaidi ya Halmashauri 110 na ni Halmashauri 30 tu zimechangia Mfuko huu, je, Serikali inaridhika na mwenendo huu wa Halmashauri 30 kuchangia katika Mfuko huu na kama inaridhika na mpango wake wa kuboresha afya za wananchi nchini?

(b) Kwa kuwa mimi binafsi nilichangia sana Mfuko huu katika Halmashauri yangu ya Babati lakini matokeo yake ndiyo hayo ya kuchangia mil.7 tu je, watendaji wenyewe wa Halmashauri wamechukua hatua gani kutokana na hali mbaya hii ya utendaji katika Halmashauri yetu wa kutokuwa na mwitikio mzuri wa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya Babati?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII – (MHE. DR. AISHA O. KIGODA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Halmashauri 74 zimeridhia na Halmashauri 30 zimechangia. Kama nilivyosema, ni jukumu la Halmashauri husika kuwahamasisha wananchi ili waweze kuchangia katika mifuko hii ili hatimaye iweze kuwa Halmashauri zote 110 kama alivyosema. Kwa hiyo, napenda nirudie kusema kwamba ni kazi ya sisi viongozi hasa katika Halmashauri husika kuwahamasisha wananchi wetu ili waweze kuona umuhimu wa mfuko huu na faida watakayoipata ili wewe kuchangia.

Mheshimiwa Spika, swalilake la pili, kwanza nichuke nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kushiriki kikamilifu kwa kuchangia pesa hii ambayo nimeitaja ya mil.7.5 lakini vile vile napenda niseme kwamba Mfuko huu wa Bima ya Afya, unamiliikiwa na Halmashauri husika. Kama alivyosema kwamba pesa iliyochangiwa ni ndogo kwa maana hiyo nafasi ya Watendaji inaonekana kwamba hawakufanya vizuri. Lakini niseme kwamba Watendaji wa Halmashauri kama kutakuwa na matatizo yeote ni Halmashauri husika ndiyo inachukua hatua kuweza kuona ni wapi wamekosea na wapi warekebishiwe na kama kuna ubadhilifu basi waweze kuwajibishwa.

Nachukua nafasi hii tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani huko waliko na viongozi wote, twende katika Halmashauri zetu tuone kwamba wananchi wanahamasishwa na iwapo kama kutakuwa na uhamasishaji mzuri basi tuhakikishe kwamba wale watendaji kama hawafanyi kazi zao vizuri wachukuliwe hatua zinazofaa kwa kadri kanuni na taratibu zinavyotaka.

Na. 40.

Njia ya Kwenda Geita Kupitia Mgodi wa Dhahabu Geita

MHE. KABUZI F. RWILOMBA aliuliza:-

Kwa kuwa mgodi wa dhahabu wa Geita ulizua njia fupi ya kwenda Geita Mjini kwa wananchi wa Vijiji vya Saragulwa, Nyamwilolewa, Chigunga, Kabugozo, Nyachiluluma, Bukondo na Chankorongo; na kwa kuwa, wananchi hao waliwekewa barabara nyininge ambayo ni ndefu sana kupitia mapororini ambako wasafiri huporwa mali zao na majambazi na wakati mwingine hata kuuawa lakini licha ya tatizo hilo njia hiyo inapitia kwenye kilima kirefu ambacho magari mengi yanashindwa kupita na matokeo yake husababisha ajali na vifo vya wasafiri:-

(a) Je, ni baiskeli ngapi zimekwishaporwa katika pori hilo na watu wangapi wamepoteza maisha yao kwa kuvamiwa na majambazi na kuanguka na magari tangu barabara hiyo ilipoanza kutumika?

(b) Je, kwa nini mgodi husika usiweke uzio ili wananchi waweze kutumia njia fupi kwenda Geita?

(c) Je, wanaomiliki mgodi na Serikali wanaahidi kutoa fidia gani kwa mali na watu wanaopoteza maisha yao kwa njia hiyo hadi hapo mgodi utakapofunga kazi zake za uchimbaji?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwiomba, Mbunge wa Busanda, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Saragulwa, Nyamwilolelwa, Chigunga, Kabugozo, Nyachililima, Bukondo na Chankorongo vipo katika Tarafa ya Butundwe Magharibi mwa mgodi wa dhahabu wa Geita. Kabla ya mwaka 2000, Vijiji hivi viliunganishwa na Mji wa Geita na barabara iliyokuwa na urefu wa kilimota 12. Kwa sasa vijiji hivyo vinaunganishwa na Mji wa Geita kwa barabara yenyе urefu wa kilomita 21 ambayo ilijengwa badala ya ile ya awali, ili kukwepa maeneo ya mgodi. Sehemu ya barabara hiyo hupitia katika maeneo yasiyo na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa barabara nyingine ambayo ilikuwa na lengo la kukwepa maeneo ya mgodi wa Geita, lilijadiliwa sana na wadau mbalimbali wa Wilaya ya Geita ukiwemo uongozi wa Wilaya, Vijiji ambavyo viliunganishwa na barabara iliyokuwepo awali na uongozi wa mgodi wa Geita katika kipindi cha miaka 1999 na 2000. Makubaliano yalifikiwa kuwa ichongwe barabara kutoka eneo la *Copcot* mpaka njia panda ya Nyarugusu na barabara hii ilipewa jina la Kabuzi *Road*. Tunaamini kwamba jina hili ni kwa heshima ya Mheshimiwa Mbunge kwa kazi ambayo amekuwa akiifanyia katika Jimbo lake. Barabara hii ni ya kiwango cha moramu na inapitika kipindi chote cha mwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Kabuzi, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baiskeli nne (4) zilikwishaporwa na majambazi kutoka kwa wananchi wakati wakipita katika maeneo yasiyokuwa na makazi ya watu. Hakuna taarifa za watu kuuawa au kunyang'anywa mali nyingine tofauti na baiskeli.

Mheshimiwa Spika, licha ya kiwango kizuri cha barabara hiyo, jumla ya ajali mbili zimeshatokea katika njia hiyo kutohana na ubovu wa magari husika kupita kiwango

chake. Ajali ya kwanza ilihuisha gari la mizigo ambapo watu wawili walipoteza maisha na ajali ya pili ilihuisha gari dogo la abiria ambayo haikuhusisha kifo wala majeruhi

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na Kanuni za Usalama Migodini, mmiliki wa mgodi anatakiwa kutoruhusu kuwepo kwa shughuli za kijamii ndani ya eneo la mgodi ili kuepusha ajali na maafa yanayoweza kutokea kutokana na shughuli za uchimbaji madini zinazohusisha mitambo mikubwa na ulipuaji wa baruti.

Mheshimiwa Spika, kuweka uzio kwa maeneo kadhaa yanayofanyiwa kazi na kuruhusu kutumika kwa njia ya zamani ambayo ni fupi, kutakiuka Kanuni za Usalama Migodini na ni hatari kwani hali hiyo inaweza kusababisha ajali na maafa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita katika kuhakikisha barabara hiyo inakuwa katika hali ya ubora wakati wote.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la mali na watu wanaopoteza maisha kutokana na ujambazi hushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria za Makosa ya Jinai na Sheria ya Bima, Serikali inaadhi kuendelea kuimarisha usimamizi wa Sheria hizi ili kuwezesha haki kutendeka kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha vyombo vyake vya usalama vinalinda usalama wa wananchi na mali zao kwa kuimarisha ulinzi katika njia hiyo kwa kufanya doria za mara kwa mara. Aidha, tunatoa rai kwa watoa huduma ya usafiri kuhakikisha kwamba vyombo vyao ni salama na vinakidhi viwango vya ubora kwa mujibu wa Sheria na taratibu za nchi ili kuepusha ajali zinazosababishwa na ubovu wa vyombo hivyo.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize maswali mawili ya nyongeza. Nasikitika kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri nadhani ni kwa kuwa hajafika kule akaona matatizo yanayojitokeza, ajali zilizotoke si kwamba ni kwa sababu ya magari mabovu, ni kwa sababu ile njia ina kilima kirefu magari hayawezi kupita hata kama magari yangekuwa mazuri. Kitu kinachoitwa *Kabuzi Road* mpaka sasa haipitiki na ilipatikana kwa shinikizo kubwa, mpaka sasa bomba la Saragurwa linalopeleka maji mgodini wananchi wamelivamia na kulibomoa na wameendelea kuteseka:-

(a) Kwa kuwa mgodi huo unatarajiwa kuwepo zaidi ya miaka 30-50 na inavyoonekana Serikali inakubali wananchi waendelee kuteseka, je, inaturuhusu sasa kwa kuwa ilituhamisha na sisi tutafute namna yeoyote ili tuweze kupita njia yetu kwa sababu ni mateso ya kudumu kwa wananchi hao?

(b) Mheshimiwa Spika, kupita pembedi, watu kuperwa na kubakwa ingawa vitu vingine ni siri, wako tayari kulifanya utafiti na wakigundua kwamba kuna watu wameporwa, wamebakwa, wameuawa pale, wako tayari kuwafidia kwa sababu njia ile imepindishwa kwa makusudi ili watu wasipite mgodini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, naomba nifafanue kwamba maeneo hayo nayaafahamu vizuri na kwa kweli mwezi wa nane mwaka jana nilikuwa kule, nimefika maeneo hayo, nayaafahamu. Lakini naomba nisisitize na ninamshauri Mheshimiwa Mbunge tukubaliane kwamba kilima anachokisema nakifahamu na si kweli kwamba magari yote yanashindwa kupita pale na vilima vingi tu ambavyo vimeduwa vikipitwa na magari yenyeye viwango tofauti, lakini kwa kweli kilima hicho si cha kusema kwamba magari yanashindwa kupita, ni kilima ambacho kina matatizo lakini siyo kwa kiwango kile ambacho pengine katika hali ya kawaida tungeweza kukisemea.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kulifanya kazi ombi lake kama alivyosema kwa yale ambayo yanajitokeza na hasa hizi athari za ubakaji. Sisi tunaahidi kulifanya utafiti na tunamwomba tushirikiane na wananchi kutoa taarifa kwenye Vituo vyetu vya Polisi. Kwa sababu fidia zinapatikana kupitia Sheria zetu za Madai ya Jinai lakini pia kwa mujibu wa Sheria za Bima, kwa hiyo, tuendelee kushirikiana na wananchi ili mradi taarifa za uhakika zinafika.

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa majibu yake mazuri na vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Rwilomba kwa kuwaonea huruma wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni kumekuwa na uchukuaji wa Sheria mkononi kwa maeneo mengi na mimi nimeshtuka Mheshimiwa Rwilomba kusema kwamba na wananchi watatafuta njia ya kuwahamisha wale, naona hiyo ni kuchukua Sheria mkononi. Napenda kusisitiza kwamba Mheshimiwa Mbunge na Serikali wakae pamoja kuona kwamba tatizo hili linapata ufumbuzi wake badala ya yeze kufikiria kuchukua Sheria mkononi na ninawaomba wananchi kwa ujumla katika kulinda na kuimarisha amani ya Tanzania, wasipende kuchukua Sheria mkononi. (*Makofii*)

Na. 41

Miradi ya Umeme ya Dongobesh na Daudi

MHE. MARTHA J. UMBULLA aliuliza:-

Kwa kuwa nishati ya umeme ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi vijijini; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne katika kutekeleza Ilani ya CCM, imekwishaidhinisha na kugharamia miradi mingi vijijini vikiwemo na vijiji nya Dongobesh na Daudi Wilayani Mbulu:-

(a) Je, kuna matatizo na vikwazo gani kwa *TANESCO* kufanikisha miradi hiyo ya Dongobesh na Daudi ambayo imechukua muda mrefu sana sasa?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani ya kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilika haraka ili ahadi hiyo kwa wananchi itimizwe kabla ya mwaka 2010?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Dongobesh unajumuisha ujenzi wa kilomita 22 za laini kubwa ya umeme (*high tension*) na kilomita 4 za laini ndogo ya umeme (*low voltage*). Hadi sasa nguzo zote za laini kubwa na ndogo za umeme zimeshasimikwa na waya wa laini kubwa ya umeme imeshawekwa katika umbali wa kilomita 16.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Daudi unajumuisha ujenzi wa kilomita 16 za laini kubwa ya umeme (*high tension*) na kilomita 2 za laini ndogo ya umeme (*low voltage*), tayari nguzo za laini kubwa ya umeme zimeshasimikwa katika umbali wa kilomita 7.5

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukosefu wa vifaa nya ujenzi wa laini kama vile nguzo na waya uliopo, miradi hiyo miwili imesimama. Hata hivyo, vifaa hivyo pungufu vimeagizwa na vinatarajiwa kuwasili katikati ya mwezi wa Februari, 2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Martha Umbulla, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyosababisha miradi kusimama ni ukosefu wa vifaa nya ujenzi wa laini hizo kutokana na hali ya mbaya ya kifedha iliyokuwa ikiikabili shirika la *TANESCO*.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi, tayari Shirika la *TANESCO* limeshachukua hatua za kuagiza vifaa vilivyohitajika kwa miradi hiyo na mara vifaa vitakapofika Mkoani Manyara mwezi Februari mwaka huu, kazi ya kukamilisha miradi hiyo itaendelea mara moja.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo mimi naona hayakidhi matumaini ya wananchi, naomba kuuliza maswali madogo nya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika kufuatilia suala hili miaka miwili ya nyuma, tumeambiwa kwamba tatizo kubwa ni upatikanaji wa aina fulani ya nyaya ambazo haipo hapa nchini na kwa kuwa nguzo zilikwishaplikana na kwa sehemu nyingine kusimikwa tayari jambo ambalo limegeuka kero na shutuma kubwa kwa viongozi na hasa Wabunge, je, kwa nini Serikali isiliwezeshe Shirika la *TANESCO* ili liweze kuagiza aina hiyo ya nyaya kutoka huko nje ya nchi ili kuweza kukamilisha miradi ya aina hii hata kwa sehemu zingine za nchi? (*Makofî*)

(b) Kwa kuwa miradi hii miwili ambayo niliitaja ya Dongobesh na Daudi haipo katika mpango wa usambazaji wa umeme vijijini, ningependa kujua ni vijiji vingapi katika Wilaya ya Mbulu ambayo iko chini ya mpango huu wa kusambaza umeme vijijini chini ya Wakala wa Usambazaji Umeme vijijini? Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, la kwanza, hatua ambazo tunazichukua kuliwezesha Shirika la *TANESCO* ni pamoja na kurekebisha sera. Kama mnavyofahamu hivi karibuni na kwa kweli katika Mkutano huu, tunatarajia kuleta mbele ya Bunge hili Tukufu Muswada ambao utawezesha hatimaye kutunga sheria mpya itakayoshughulikia masuala ya umeme na nishati kwa ujumla. Sababu ya msingi inayosababisha kuleta Muswada huu mbele ya Bunge hili Tukufu ni kuweza kufungua wigo ili kuwezesha pia watoa huduma wengine na hasa sekta binafsi kuingia na kutoa huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu uwezeshaji ungeweza kuwa wa kifedha kwa shirika la *TANESCO* lakini kama tunafahamu sera yetu, tumejaribu mara kadhaa na wote tunafahamu kwamba sera yetu ni ya soko huria pamoja na tunafahamu Shirika la *TANESCO* ama huduma ya umeme ingeweza pia kuimarishwa na ushiriki wa Serikali, lakini kwa sababu ni suala la kisera tukadhani kwamba kwa sababu mahitaji ni mengi sana kuiwezesha *TANESCO* kwa kutoa ruzuku kama ambavyo imejitokeza katika historia ya nchi ingeweza pia kukwamisha shughuli zingine. Lakini kingine ambacho ninaweza kusema ni kwamba Serikali imeendelea kushirikiana na Shirika la *TANESCO* kuliimarisha kiutalaam lakini pia kulijengea mazingira zaidi ili liweze kutoa huduma nzuri zaidi na hasa ushindani utakapokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ambayo iko katika Wilaya ya Mbulu, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu bahati mbaya au nzuri hapa hatuna orodha ya miradi ambayo iko katika huu utaratibu wetu wa Wakala wa Umeme Vijijini basi nimkaribishe ofisini kwetu tumpe orodha kwa sababu tuna orodha ya nchi nzima. Kwa Wabunge wengine pia tuko tayari kuwapa miradi ambayo inakwenda kwa awamu mbalimbali katika utekelezaji wake kupitia Wakala wa Umeme Vijijini.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swalı moja tu la Wizara ya Miundombinu. Kwa hiyo, sasa namuita kwa swalı la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini.

Matumizi ya Bandari ya Mtwara

MHE. MOHAMED S. SINANI aliuliza:-

Kwa kuwa, Bandari ya Mtwara ambayo ina kina kirefu kuliko bandari zote hapa nchini, ina vifaa vya kupakia na kupakulia makontena na imefanyiwa matengenezo (*heavy duty paving*) hivi karibuni kwenye sehemu ya kuwekea makontena hayo lakini kwa sasa inafanya kazi wakati wa msimu wa korosho tu:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuitumia bandari hiyo ili kupunguza msongamano kwenye bandari ya Dar es Salaam?
- (b) Je, ni lini Serikali itakamilisha matengenezo yaliyobaki?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

- (a) Ni kweli kuwa Bandari ya Mtwara ina kina kirefu cha asili na ina vifaa vya kupakia na kupakulia makontena na imefanyiwa matengenezo sehemu ya kuweka makontena na kwamba hufanya kazi zaidi msimu wa korosho.

Kwa sasa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, inafanya mazungumzo na wenge kampuni za meli kuweza kutumia bandari ya Mtwara ili kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam. Aidha, kampuni za *Emirates* na *DIL* na *H&H Lines* zimeonyesha mwelekeo wa kuanza kutumia Bandari ya Mtwara kwa kupeleka meli kubwa katika bandari hiyo na kwa jinsi hiyo utaratibu wa kutumia meli ndogo (*feeder vessel*) kwa ajili ya kuleta mizigo kutoka kwenye meli kubwa kuja Dar es Salaam uko mbioni kukamilika. Aidha, inatarajiwa utaratibu huu utaanza kutumika mwezi Februari 2008 na hivyo kutapunguza msongamano wa makontena katika kitengo cha makotena katika Bandari ya Dar es Salaam.

- (b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, ina mpango wa kukamilisha matengenezo yaliyobaki sambamba na ukamilishaji wa Mpango wa Utafiti wa Uboreshaji Bandari (*Post Master Plan Study*) ambao utasaidia kupata matumizi bora ya bandari. Aidha, mpango huu utajumuisha utafiti wa kuendeleza eneo la *Export Processing Zone* linalomilikiwa na Mamlaka lenye ukubwa wa hekari 2,600 na hivyo kuongeza matumizi ya Bandari ya Mtwara na kuiboresha kuwa ya kisasa zaidi.

MHE. MOHAMED S. SINANI: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika hizi hekta 260,000 zilizochukuliwa na bandari kuna baadhi ya wananchi hawajalipwa fidia zao, je, ni lini Serikali itawalipa hizi fidia? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI): Mheshimiwa Spika, asilimia 99.9 ya wale ambaو walichukuliwa maeneo yao wamelipwa, waliokuwa hawajalipwa ni kama wawili ambaو mazungumzo yanaendelea kupata kina hasa cha fidia kinachotakiwa kulipwa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama nilivyomwambia tulipokuwa Mtware kwamba wale waliobakia watalipwa baada ya kujiridhisha. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita. Kwa bahati mbaya nimebakiza maswali mawili, sina ufanisi mzuri kama ule wa Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri udhaifu huo, lakini tutaendelea kubadili hiyo ili maswali yote yajibiwe. Kwa hiyo, hayo maswali mawili ya Miundombinu yaliyosalia, tutajitahidi kuyaweka ili yajibiwe katika Mkutano huu.

Matangazo, tunaanza na wageni. Mgeni wa Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia, ni ndugu Said Yaku, ambaye ni Mtangazaji Mstaafu wa *BBC London* lakini kwa sasa amerejea nyumbani. Bwana Said Yaku, yule pale, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wetu wengine leo ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Chibuji kule Kwimba, bwana Clement Luchanganya, ni Mgeni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila kutoka Kwimba. Ahsante sana karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia vijana 15 wa kikundi cha sanaa kinaitwa Mshikemshike cha hapa Dodoma, hao hapo. Hakuna ufanuzi, sanaa yao ni ipi labda kwa kuwa bado tuko Dodoma tutakuja kushuhudia.

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Paul Kimiti ambaو ni vijana katika ukoo wake, Proper Kimiti, Steven Triponi na Mary Joseph, wale pale. Karibuni sana. Wote hao niliowataja wa Ukoo wa Kimiti wako Chuo Kikuu, wanasomea taaluma ya utawala, tunawatakia kila la kheri katika masomo yenu.

Taarifa za vikao, Mheshimiwa Job Ndugai, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, kukutana leo tarehe 31/1/2008 saa tano asubuhi katika ukumbi 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 31 katika kikao cha Kamati saa saba mchana, chumba namba 219, kuna mkutano muhimu sana. Kwa hiyo, Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), chumba namba 219, ghorofa ya pili jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge, mtagundua kwamba tumechelewa kutoa nakala rasmi za Kanuni za Bunge, sababu ni nzuri tu kwamba kulikuwa na mambo machache ambayo ilibidi tushauriane na kukubaliana na Serikali. La msingi hapa ni kwamba tumekubaliana

kwamba Bunge letu litakuwa na utaratibu wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, maswali hayo kama mlivyoamua si ya maandishi kwa hiyo yatakuwa ni ya papo kwa papo. Kwa hiyo, ili kutengeneza utaratibu huu, imebidi sehemu hiyo iandikwe vizuri na saa 11.00 nitamuomba Mheshimiwa Naibu Spika, aweze kuleta rasmi sasa pendekizo hilo ili likishakubaliwa na Bunge liingie sasa katika Kanuni ili kila Alhamisi tuwe na kipindi cha nusu saa cha kumuuliza moja kwa moja Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, baada ya hayo kutendeka sasa kesho asubuhi tutaweza kugawa nakala za Kanuni za Bunge, tolea la 2007. (*Makofi*)

Basi baada ya taarifa hiyo, namuomba sasa Mheshimiwa Naibu Spika, aweze kushika Meza wakati nikishughulikia mambo mengine.

Hapa Naibu (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu shughuli inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi Vya Ukimwi
Nchini wa Mwaka 2007 (The HIV and Aids Prevention and Control Bill, 2007)**

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote hapa kuweza kuhudhuria Mkutano huu wa Bunge.

Kabla sijaanza kutoa hoja yangu, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa salaam za rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rungwe Magharibi kwa familia ya aliyejewa Mbunge wa Kiteto.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnavyotoka, mtoke kimya kwa sababu kazi inaendelea.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Hayati Benedict K. Losurutia. Kwa hakika, kifo chake kimeacha pengo kubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Kiteto na kwa Taifa kwa ujumla. Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ailaze roho yake mahali pema peponi, amen.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Napenda kumwahidi ushirikiano wa hali ya juu wa Wizara yangu katika kutekeleza majukumu haya mapya kama Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw' kwa mchango wao mkubwa ambao umeniwezesha kuwasilisha Muswada huu Bungeni siku ya leo.

Pia napenda kushukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Muswada huu pamoja na jedwali la mabadiliko kwa umakini na kwa wakati. Aidha, shukrani zangu za pekee ziwaendee wadau wote walioshiriki kujadili Muswada huu kwa kina na kuleta mapendekezo ambayo yamezingatiwa, niwataje baadhi ya wadau kama ifuatavyo:-

Kuna *Civil Society Organizations* vyama 62, *Ingonet Legal and Human Rights Centre*, Muungano wa Wafanyabiashara, *National Organization for Legal Assistance*, *Disable Organization for Legal Affairs and Social Economic Development, Tanzania Gender Networking Program*, *UN- Aids* na washirika wa maendeleo katika mchakato mzima wa kudhibiti Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya awali, sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria Uitwao *The HIV Aids Prevention and Control Act* wa mwaka 2007 pamoja na jedwali la mabadiliko kama ulivyopangwa katika orodha ya shughuli za leo sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya kuwepo UKIMWI hapa nchini ilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1983 katika Mkoa wa Kagera. Tangu kipindi hicho, ugonjwa huu umeenea Mkoa hadi Mkoa; hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2004, ilikadiriwa kwamba Watanzania milioni 1,300,000 walikuwa wameambukizwa virusi vya UKIMWI na kiwango cha maambukizi kilikadiriwa kuwa ni asilimia 7 kwa watu wazima wenye mhemko wa kingono. Kutokana na kukua kwa tatizo hilo, Serikali ya Awamu ya Tatu, mnamo Desemba mwaka 1999 ilitangaza UKIMWI kuwa ni janga la Taifa. Kwa mujibu wa kampeni ya upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari inayoendelea hapa nchini na iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais, tarehe 14/7 mwaka jana, takwimu zinaonyesha maambukizi sasa yameshuka na kufikia asilimia 5 Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba asilimia kubwa ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yanatokea kwenye mazingira ya usiri na makubaliano kati ya wahusika. Hivyo ni vigumu kudhibiti maambukizi ya UKIMWI kwa kutumia elimu na ushawishi peke yake bila kutumia afua nyingine (*interventions*). Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imeanzisha afua mbili na hizi ni pamoja na utoaji wa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI bila malipo kwa wagonjwa wenye UKIMWI, vile vile kampeni inayoendelea ya Kitaifa ya upimaji wa VVU wa hiari.

Hata hivyo ni miaka 25 sasa tangu UKIMWI uingie hapa nchini na Serikali na wadau wengine wamekuwa wakitekeleza afua mbalimbali lakini tatizo bado linaendelea. Hivyo linapendekezwa kutumia pia afua ya nyongeza ya kutunga sheria. Sheria inayopendekezwa itajikita kwenye masuala ya huduma za afya na kijamii, elimu ya afya kwa umma, kuondoa ubaguzi na unyanyapaa, kutunza siri ya mtu anayeishi na VVU na kuweka utaratibu wa kisheria wa kuvunja usiri huo pale inapobidi, kusimamia tafiti mbalimbali za VVU na Ukimwi na magonjwa nyemelezi na kuweka adhabu kwa watakaodhihirika kuwa wanaambukiza wenzao virusi vya UKIMWI kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumni ya Muswada. Tangu mwishoni mwa miaka 1980, Wizara yangu imekuwa ikijibu maswali mbalimbali ya Bunge ambapo Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakiitaka Wizara kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Udhibiti UKIMWI.

Aidha, katika kikao cha Bajeti kilichopita mwaka 2007, Serikali kupitia Wizara yangu mnamo tarehe 13 Juni, ilijibu swali namba 11 ambapo Mheshimiwa Mbunge, Omar Kwaangw' alitaka kujua maeneo ambayo wadau wametaka kutungwa kwa sheria na ni lini sheria hii itawasilishwa Bungeni. Katika kujibu swali hili, tulainisha maeneo muhimu yatakayoangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukamilisha azma hiyo ya Serikali pamoja na wananchi mbalimbali, Muswada ulio mbele yenu ulisomwa kwa Mara ya Kwanza katika Bunge hili tarehe 5 Novemba, 2007. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mikutano yake mbalimbali ya hadhara, amekuwa akiwataarifu wananchi hatua ya Serikali ya kuandaa Muswada wa Sheria ambao pamoja na mambo mengine utaweka adhabu kwa watu watakaogundulika kuwa wanaeneza virusi vya UKIMWI kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inayo Sheria ya Magonjwa ya Kuambukiza, Sheria hii ni ya mwaka 1921. Sheria hii inasisitiza masuala ya kuwatenga wagonjwa, kuwapima wagonjwa kwa lazima, kuvunja siri ya wagonjwa na kadhalika. Ugonjwa huu ni tofauti na magonjwa mengine ya kuambukiza kwani ni mlimbiko wa dalili (*syndrome*) na kutokana na kwamba Sheria iliyopo haizingatii haki za binadamu na kwamba kumekuwa na mabadiliko mengi ya kisayansi na kiteknolojia ni wazi kwamba sheria iliyopo haikidhi kikamilifu matakwa ya kukabiliana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kupata maoni umechukua muda mrefu kutokana na ugonjwa huu ambao ni mgeni na uko tofauti na magonjwa mengine ya kuambukiza. Kutokana na hali hiyo, mnamo mwaka 1993, Wizara ya Afya iliwasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuiomba Ofisi hiyo, iangalie uwezekano wa kuwa na Sheria itakayosimamia suala zima la ugonjwa wa UKIMWI. Kutokana na ombi hilo la Wizara ya Afya, Wizara ya Sheria, mnamo mwaka 2001 iliwapa jukumu Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kufanya mapitio ya Sheria zote za nchi ili kuona ni kwa namna gani zinakwamisha mapambano dhidi ya UKIMWI na kutoa

ushauri Serikalini. Mapitio hayo ya TAWLA pamoja na mapendekezo yao yaliwasilishwa katika vikao mbalimbali vya wadau ambao walipendekeza kutungwa kwa Sheria na vile vile kufanya mapitio ya baadhi ya Sheria ili kuweza kuweka masuala yanayohusu UKIMWI.

Tangu kipindi hicho, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Taifa ya Kudhibiti (*TACAIDS*), ilifanya mawasiliano na wadau mbalimbali ili kupata maoni kuhusu pendekezo la kuwa na Sheria Mahususi itakayosimamia masuala ya VVU na UKIMWI. Aidha, katika mchakato huo na maandalizi ya Sheria, timu ya watalaam kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Katiba na Sheria, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) mwaka 2004 ilipata mafunzo ya uandishi wa Sheria za aina hii nchini Marekani kwa nia ya kupata uzoefu wa kutekeleza Sheria za aina hii.

Vile vile mwaka 2005 timu hiyo hiyo ilitembelea nchi za *Vietnam* na *Philippines* ambazo zina sheria za kudhibiti Ukimwi kwa lengo la kupata uzoefu kuhusu utekelezaji wa Sheria za aina hii. Uzoefu walioupata kwa kiasi kikubwa umesaidia maandalizi ya Muswada ulio mbele yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mafunzo hayo, timu hiyo ya watalaam kwa kushirikiana na Wahadhiri wa Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Paramagamba Kabudi na Profesa Sifuni Mchome, ilianda mada ya dhana (*Concept paper*) ambayo ilibainisha Sura muhimu ya Sheria inayopendekezwa. Mada ya dhana hiyo, litumika katika kupata maoni kutoka kwa wadau katika kanda mbalimbali nchi nzima. Warsha hizo za kikanda zilianza mwezi Desemba, 2006 na kumalizika Agosti 2007. Mikutano hiyo ilifanyika kikanda katika Mikoa ya Iringa, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mtwara na Morogoro.

Napenda nitumie nafasi hii kuishukuru Tume ya Kudhibiti Ukimwi nchini kwa kututafutia wahisani ambao waligharamia mafunzo ya watalaam na warsha za wadau ambazo zilisaidia kupata maoni na mapendekezo ya Muswada.

Vile vile nashukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maandalizi ya kupata maoni na katika kukamilisha Muswada huu pamoja na Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushiriki katika mchakato mzima wa kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lingine la kutungwa kwa Sheria hii ni kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi. Sera hiyo, ndiyo dira inayotuongoza katika vita dhidi ya UKIMWI hapa nchini. Muswada huu pia unalenga kutekeleza yafuatayo:-

Moja, Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti UKIMWI, Mkakati wa Sekta ya Afya Kudhibiti UKIMWI, malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu watu wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi, matamko mbalimbali ya Kitaifa kupitia Shirika la Afya Duniani na Umoja wa Mataifa ambao Tanzania iliyakubali na kuridhia na uamuzi wa Baraza la Mawaziri namba 12 ya mwaka 2007 kuhusu pendekezo la kutunga Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wa miaka mingi iliyopita, utaratibu uliozoleka wa kupambana na magonjwa ya kuambukiza ulikuwa ni wa kutunga Sheria kandamizi zilizojikita zaidi katika kuainisha makosa na kutoa adhabu, kuweka *quarantine*, kuwatenga wagonjwa bila kuzingatia uti, haki za binadamu na ujumla wa tatizo. Hata tatizo la UKIMWI lilipojitekeza Duniani baadhi ya nchi zilitunga Sheria za aina hii na utekelezaji wake ulikuwa mgumu na kuleta malalamiko toka kwa watetezi wa haki za binadamu.

Hata hivyo, uzoefu mpya wa utekelezaji wa Sheria za Afya Duniani na hasa za kusimamia udhibiti wa magonjwa ya kuambukizwa ikiwemo hali ya mtu kuwa na UKIMWI, Sheria huandaliwa kwa mwelekeo wa kuangalia tatizo la ugonjwa kwa ujumla wake (*Holistic approach*). Mtazamo huu huzingatia mipango mbalimbali ya elimu ya afya kwa umma, haki na wajibu wa wagonjwa, wajibu wa watalaam wa afya katika kukabiliiana na tatizo, wigo na mipaka ya tafiti mbalimbali, majukumu ya Serikali, asasi mbalimbali na jamii kwa ujumla, ushawishi wa kijamii kuhusu kubadili mienendo ya maisha na tabia na kuweka adhabu pale inapobidi.

Sheria za aina hii hutoa motisha na adhabu, kwa kuwa utekelezaji wake kwa kiasi kikubwa unalenga katika kubadili tabia za mhusika/wahusika katika mazingira ya kuheshimu Sheria kwa hiari na hasa kuzingatia elimu ya afya kwa umma, aidha, adhabu kali hutolewa endapo kutakuwa na ukiukaji wa Sheria ambayo inaweza kusababisha maambukizi na maafa kwa jamii kwa kuzingatia zaidi maslahi ya umma kuliko ya mtu binafsi.

Kwa misingi hiyo, mtazamo uliochukuliwa katika Muswada huu ni ule wa kuangalia tatizo kwa ujumla wake kwa kuangalia masuala ya afya ya jamii, elimu ya afya, kuzingatia haki za binadamu kwa wanaoishi na *VVU*, makosa ya jinai na kadhalika. Muswada huu kwa kiasi kikubwa umezingatia mwongozo wa umoja wa mataifa wa *VVU* pamoja na haki za binadamu uliotolewa mwaka 2006 ambao kwa Kingereza unaitwa (*The International Guidelines on HIV Aids and Human Rights 2006 Consolidated Version*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio yetu ni kwamba baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa Sheria na kuanza kutekelezwa yafuatayo yatapatikana:-

Moja, kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa unyanyapaa na ubaguzi ambao ni kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya UKIMWI, katika vituo vya huduma za afya na jamii kwa ujumla;

Pili, kuimarika na kuongezeka kwa tafiti juu ya tiba, chanzo na tafiti zingine zinazohusiana na UKIMWI kwa kuzingatia utu na heshima ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI;

Tatu, kuboresha huduma za afya ya msingi na kijamii (*care and support*) kwa wale wanaoishi na VVU;

Nne, ni kuongeza kasi ya huduma za upimaji wa VVU katika sehemu za kutolea huduma za afya hapa nchini;

Tano, kuboresha huduma za afya kwa watumishi wa afya katika vituo vya kutolea huduma;

Sita kuimarisha huduma za upatikanaji wa damu salama;

Saba, kuboresha masuala ya msingi katika kupambana na VVU katika vituo vya kutolea huduma za afya;

Nane, kuwa na mipango kabambe ya elimu ya afya kwa umma na mipango mbalimbali katika vita dhidi ya UKIMWI;

Tisa, kuwa na utaratibu ambapo watalaam wa sekta ya afya wataweza kuvunja siri inapobidi kwa mujibu wa Sheria na hivyo kusaidia kupunguza maambukizi ya UKIMWI; na

Kumi, mwisho ni kutoa adhabu kali kwa wale watakaothibitishwa kuwa wanaambukiza wenzao virusi vya UKIMWI kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mambo niliyoyaainisha hapo juum Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu 12.

Sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayopendekezwa na matumizi ya Sheria hiyo. Pia inatoa tafsiri ya baadhi ya majina na misemo muhimu inayotumika mara kwa mara katika Muswada huu.

Sehemu ya pili, inapendekeza kuweka misingi mikuu katika kutayarisha na kutekeleza mipango, mikakati inayohusu virusi vya UKIMWI na UKIMWI na kuhamasisha mashirika ya dini kufanya juhudi thabiti katika kuzuia kutoa huduma za kiafya na kudhibiti VVU katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Sehemu ya tatu, inahusu utoaji wa elimu kwa umma na program zinazohusu VVU na UKIMWI. Sehemu hii pia, ina masharti yanayohusu elimu kwa umma na program

katika kuzuia ubaguzi na unyanyapaa kwa wanaoishi na VVU na UKIMWI. Huduma kwa wagonjwa, uzuiasi wa magonjwa ya zinaa na upigaji wa kampeni endelevu dhidi ya virusi vya UKIMWI katika shule, Vyuo vya Elimu ya Juu na sehemu za kazi.

Sehemu ya nne, inahusu masharti yanayohusu upimaji wa watoa damu au wanaochangia viungo vya mwili, wajawazito na utoaji wa ushauri nasaha kwa wahusika. Sehemu hii pia inahamasisha wafanyakazi wa sekta ya afya, Waganga wa Tiba za Asili na Tiba Mbadala, Wakunga wa Jadi na mtu yejote ambaye anatoa huduma kwa wagonjwa wa jamii kwa ujumla kupima VVU.

Sehemu ya tano, inaweka masharti yanayohusu usiri katika taarifa, kumbukumbu za Kidaktari, majalada, data, na matokeo ya vipimo vya VVU na UKIMWI. Hata hivyo, usiri unaweza kuondolewa au kutozingatiwa kutokana na masharti yanayoainishwa katika Sheria hii inayopendekezwa kwa ajili ya maslahi ya jamii (*public interest*).

Sehemu ya sita inahusu utoaji wa huduma za msingi za afya na kijamii kwa wanaoishi na VVU na UKIMWI pamoja na yatima waliofiwa na wazazi wao. Pia inazuia tabia na mienendo inayoweka mazingira ya kueneza UKIMWI katika shule, ajira, sehemu za kazi na sehemu yoyote ile.

Sehemu ya saba inaweka masharti yanayozua unyanyapaa na ubaguzi kwa wanaoishi na VVU na UKIMWI na kutoa adhabu kwa atakayekwenda kinyume na vifungu hivyo. Sehemu ya nane inaweka masharti yanayohusu haki za wanaoishi na VVU na UKIMWI. Haki hizo zinajumuisha haki ya huduma ya afya ya akili na mwili katika kiwango cha juu kinachoweza kutolewa kwa kuzingatia uwezo wa Serikali.

Sehemu ya tisa ya Muswada huu inahusu Kamati Shirikishi ya Taifa ya kusimamia utafiti wa VVU na UKIMWI. Sehemu hii pia inaainisha majukumu ya Kamati hiyo. Sehemu ya 10 inapendekeza masharti yanayohusu usimamizi na tathmini katika baadhi ya maeneo kama yalivyoainishwa katika Sheria yaliyopendekezwa kama vile ukubwa na kuongezeka kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI. Sehemu ya 11 inahusu masharti yanayohusu makosa na adhabu ambazo zinaweza kutolewa endapo kutatokea ukiukwaji wa masharti ya sheria inayopendekezwa.

Na sehemu ya 12 na ya mwisho inaweka masharti ya jumla ambayo yanajumuisha mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni ili kuweza kutekeleza masharti ya Sheria yanayopendekezwa pamoja na kutokuyalazimisha mashirika ya dini au kundi lolote lile la dini kuelezea afua ambazo zinakwenda kinyume na misingi ya dini au kundi hilo endapo imani hiyo haiendi kinyume au kukiuka sheria nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha mapendekezo niliyoyawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu yamezingatiwa maoni ya wadau ambayo tuliyapata katika ngazi mbalimbali ya maandalizi ya Muswada huu.

Maoni ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Huduma ya Jamii yamezingatiwa. Kamati hii chini ya Uongozi mahiri wa Mwenyekiti Mheshimiwa Omar

Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini wametoa michango mingi na mizuri inayolenga kuboresha Muswada ulio mbele yenu. Jedwali la marekebisho lililoambatishwa katika shughuli za leo ni matokeo ya michango mizuri tuliyoiopata kutoka Kamati hii.

Napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za kipekee kwa Kamati hii kutokana na michango yao na ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa tukipata kutoka kwao. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuomba Waheshimiwa Wabunge wajadili mapendekezo yaliyomo katika Muswada huu na hatimaye kuupitisha kuwa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti virusi vya UKIMWI nchini (*The HIV/AIDS Prevention and Control Act*) ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu au Mwakilishi wake. Mheshimiwa Mwenyekiti Omar Kwaangw! (*Makofi*)

MHE. OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii uliyoipa jukumu la kufikiria Muswada wa Sheria ya Kuzua na Kudhibiti UKIMWI (*The HIV and AIDS (Prevention And Control) Act*) wa Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati naomba nianze kwa kutoa heri ya mwaka mpya kwako na kwa Wabunge wote. Aidha, nachukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia na wananchi wa Jimbo la Kiteto kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao, Mheshimiwa Benedicto Loosurutia. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi Amina. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Gertrude Rwakatare kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum, na tunakutakia heri katika kazi yako ya Ubunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipata muda wa kutosha kufikiria Muswada wa Sheria ya Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2007. Aidha, Kamati ilitenga siku moja kusikiliza maoni ya Wadau. Kamati inawapongeza wadau wote kwa kujitokeza kwa wingi na kwa michango iliyosaidia Kamati kuchambua Muswada.

Vilevile naomba nitoe pongezi za pekee kwa Waheshimiwa Wabunge chini ya Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o wa TAPAC kwa kutoa maoni na mchango mzuri sana katika kuboresha Muswada huu. Pia Kamati ilipata muda wa kutosha kujadiliana na Waziri wa Afya akisaidiwa na Naibu Waziri, jopo la wataalamu wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kupitia vifungu na vipengele vyote vya Muswada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu kuwa hivi sasa Mataifa yote yapo katika harakati za kupambana na vita dhidi ya UKIMWI na maambukizi yake. Aidha, wote tunafahamu kuwa tatizo la ugonjwa wa UKIMWI ultajwa kuwa JANGA katika Taifa letu, na kuwa Serikali imewahi kuchukua hatua za kupambana na janga hili ikiwa ni pamoja na kutunga Sera ya kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2001, kuweka Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI na kwa kuunda Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) na *NACP* na hatua ya tatu ni ya Serikali kuleta Muswada huu wa Sheria ya Kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hii muhimu katika kufanikisha mapambano dhidi ya UKIMWI ikiwa ni hatua ya kuanzisha nguvu ya kisheria ya kutekeleza Sera na Mkakati wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI. Muswada huu unatoa msukumo wa kuhakikisha kuwa Sekta zote katika jamii zinashiriki kikamilifu kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Muswada huu unatokana na ukweli kwamba wapo watu wanaoambukiza wengine kwa makusudi. Aidha, kupitia wale walioathirika au kwa kutumia njia zingine kama vile kutumia vifaa kama sindano au kuongeza damu isiyo salama kwa mukusudi ya kuathiri watu wengine kwa sababu zozote zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kufahamu kuwa janga hili ni tatizo kubwa katika jamii kwani ugonjwa huu hauna mipaka kwa namna unavyosambaa na kuleta athari kubwa kwa jamii na kwamba:-

- (i) Ni vigumu sana kujua gharama za huduma kwa wagonjwa na mara nyingi imewaangukia akina mama.
- (ii) Vilevile ni vigumu sana kukisia gharama za vifo na mazishi yanayotokana na UKIMWI kwa familia na Taifa kwa ujumla.
- (iii) Vilevile matatizo yanayotokana na athari za kisaikolojia na unyanyapaa (*stigma*) hayapimiki.
- (iv) Gharama za chakula na dawa ni zaidi ya uwezo wa kawaida wa familia na umaskini unazidi kujikita kwa familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Muswada kuanzisha Sheria ni Kuzuia na Kudhibiti VVU/ UKIMWI nchini, kwa kutumia kwa pamoja mtazamo wa afya ya jamii, haki za binadamu na Sheria za makosa ya jinai katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI, kutoa ushauri nasaha na utoaji wa huduma ya Afya kwa watu wanaoishi au kuwa katika hatari ya kuambukizwa VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaunga mkono hatua ya Serikali kuleta Muswada wa Sheria hii ikiwa na dhamira ya dhati ya kuongeza kasi ya kupambana na kutokomeza ugonjwa huu ambaa hauna kinga wala tiba. Kamati pia inaunga mkono

muswada huu kwa kuweka adhabu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wale watakaodhahirika kueneza virusi vya UKIMWI kwa makusudi au kutumia vibaya fedha au rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga hoja hii, Kamati inatoa maoni yafuatayo kwa lengo la kuboresha na kufanikisha utekelezaji wa Sheria hii.

(a) Jina la Muswada (*Long title*), Kamati inapendekeza kuwa maneno ‘*where resources allow*’ yaondolewe na badala yake yawepo maneno ‘*using available resources*’ ikiwa ni kuthibitisha dhima au ‘*commitment*’ ya Serikali kutenga fedha za kutosha kuhudumia waathirika wa UKIMWI na shughuli zinazohusu kudhibiti kuenea Virusi vya UKIMWI. Kwa kuzingatia ushauri huu maneno ‘*where resources allow*’ popote yalipo katika Muswada huu yabadilishwe na kuwa ‘*using available resources*’. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa rasilimali zote zitakazotengwa kufanikisha mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI zitumike kama ilivyokusudiwa. Ushauri huu unazingatia na maoni ya wadau.

(b) Sehemu ya Kwanza, katika ufanuzi wa maneno yaliyotumika, Kamati inapendekeza maneno ‘*Informal sector/ Private Sector*’ yaongezwe ili kuweka dhana ya kuhusisha Sekta binafsi na isiyo rasmi katika kufanikisha utekelezaji wa Muswada.

(c) Sehemu ya Pili, Kifungu (4)(2), Kamati inapendekeza kuwa baada ya maneno ‘*leaders*’ yaongezwe maneno ‘*and employees in the private sector*’. Aidha, katika kifungu 4(3), maneno yanaonesha kifungu hicho kutohusisha Idara na Taasisi za Serikali, hivyo Kamati inapendekeza kifungu hicho kisomeke ‘*institution, organization, government, political, religious, traditional leaders and employees in the private sector*’ kwa lengo la kushirikisha jamii nzima katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Aidha, katika Kifungu cha 6(1) cha Muswada baada ya neno ‘*gender*’ Kamati inapendekeza maneno ‘*including disability*’ yaongezwe kukidhi mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu wa aina mbali mbali.

(d) Sehemu ya Tatu, Kifungu cha 7(1), Kamati inakubali kuwa kifungu hiki kirekebishwe ili maudhui yake yajumuise jamii na Serikali nzima katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa kuongezwe kifungu kidogo cha (2) katika Kifungu cha 7 ambacho kitawezesha vijana katika ngazi mbalimbali kupata elimu kuhusu athari za ugonjwa unaotakana na VVU na UKIMWI .

Kifungu cha 8 Kamati inapendekeza kuwa kiongezwe kifungu kidogo cha (3) ambacho kitaleta dhana ya kushirikisha kikamilifu jamii ya watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali katika mapambano dhidi ya UKIMWI. (*Makofii*)

Katika Kifungu cha 11(5) Kamati inapendekeza kuwa vitajwe viwango vya adhabu vya chini na juu badala ya kuiachia Mahakama kuamua.

(e) Sehemu ya Tano, Kifungu cha 18(3), Kamati inapendekeza kuwa pamoja na usiri unaotakiwa kuzingatiwa na wataalam wa afya kwa waathirika wa UKIMWI,

kiongezwe kifungu kidogo ambacho kitamwezesha mwanafamilia wa karibu sana na anayehusika kufahamishwa chanzo cha kifo cha muathirika wa UKIMWI.

Kifungu cha 19(1), Kamati inapendekeza kuwa baada ya neno ‘AIDS’ maneno ‘vulnerable children’ yaongezwe ili kuwezesha watoto walioathirika na yatima kupata huduma za Afya na haki zao. Kifungu cha 21, Kamati inapendekeza kifungu hiki kirekebishwe kulingana na maudhui ya vitendo vilivytajwa na adhabu zake.

(vi) Sehemu ya Nne, Kifungu cha 23(2), Kamati inapendekeza kuwa kiweseshes watu wenyewe ulemavu wa aina tofauti kuwekewa mazingira yatakayowawezesha kupata kwa usahihi maelekezo ya matumizi vifaa vya kuzuia maambukizi ya VVU. Kifungu cha 23(3) kinahusika na adhabu mbalimbali zitakazotolewa kwa watakaothibitika kukiuka masharti ya kifungu hiki. Kamati inapendekeza kuwa Sheria iweke wazi kiwango cha chini na cha juu cha adhabu badala ya kuiachia mahakama kuamua itakavyoona inafaa.

Kifungu cha 25 Kamati inapendekeza kuwa maneno ‘loss or pecuniary loss’ yaondolewe na badala yake liwekwe neno ‘injury’ ili kuleta maana halisi ya kusudio la ibara hii.

(vii) Sehemu ya nane, Kifungu cha 35(1), Kamati inashauri kuwa ili kuwawajibisha wote watakaotumia vibaya fedha zitakazotolewa kudhibiti UKIMWI au kuhudumia wanaoishi na VVU katika watoto yatima na wajane maneno ‘public institutions’ yaongezwe kwa kuzingatia kuwa Taasisi za Serikali nazo hupata fedha nyingi kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI. Hivyo ni muhimu kwa Taasisi za Serikali kuwajibika ipasavyo kama NGOs. CBOs na kadhalika. Aidha, Kamati inakubali viwango vya adhabu zilizopendekezwa kwa kuzingatia uwezo wa Shirika, Taasisi na watu binafsi. Kuhusu Kifungu cha 35(2) Kamati inashauri kuwa matumizi mabaya ya fedha au misaada inayotolewa kwa Waathirika wa UKIMWI, adhabu zilizopendekezwa zionyeshe wazi kiwango cha chini na cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 47(b) kinapendekeza adhabu kwa watakaothibitika kueneza VVU kwa makusudi. Kamati inapendekeza kuwa adhabu iwe ni kifungo kuanzia miaka 5 hadi 10 kutokana hali halisi na uzoefu wa nchi nyingine. Kwa mfano, Kenya ni faini ya shilingi laki tano (milioni tano za Tanzania) na kifungo kisichozidi miaka saba. Philippines ni kifungo cha miaka 6 hadi 12 na kadhalika. Katika eneo hili tunahitaji vilevile kujifunza zaidi kutoka kwa mataifa mengi zaidi ili kuzingatia zaidi ubaya wa matukio ya aina hii katika jamii. Hivyo adhabu hii ni kianzio tu.

(viii) Sehemu ya tisa, Sheria inaunda Kamati ya Kitaifa ya kusimamia shughuli za Utafiti kuhusu UKIMWI. Tunashauri kuwa pamoja na idadi ya wajumbe iliyopendekezwa pia waongezwe wawakilishi wengine kutokana na umuhimu wao kama ifuatavyo:-

(j) One member representing National Institute of Health forum.

(k) Vilevile *one member representing the Association of Private Health Facilities of Tanzania.*

(l) *One member representing organizations of people living with HIV and AIDS;* na

(m) *One member from the Commission for Human Rights and Good Governance.*

Aidha, Kamati inashauri kuwa utunzaji na usambazaji wa takwimu na taarifa za matokeo ya utafiti kuhusu VVU na UKIMWI uzingatie pia na mahitaji maalumu ya walemavu wa aina mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Sheria hii haiwezi kutekelezwa kwa ufanisi endapo Serikali haitazifanyia marejeo na marekebisho Sheria 23 zifuatazo ambazo zinagusa maisha ya wananchi na huduma zao. Sheria hizi kwa kifupi ni:- (1)

Medical Practitioners and Dentist Act, Cap 152 R.E 2002; (2) Nurses and Midwives Registration Act, CAP 352, R.E 2002; (3) Private Hospitals (Regulation) Act, 1996, Cap 151 R.E 2002; (4) Private Health Laboratory Technologists Registration Act, 1997, Cap 136 R. E 2002; (5) Local Customary (Property Inheritance) Law (Declaration) Order, (No. 4) 1963; (6) Rule 66 of the Local Customary Law (Declaration) Order 1963, G.N. 279; (7) The Pharmacy Act No. 7, 2002; (8) The law of Marriage Act, 1971, Cap 29 R.E 2002: Property Rights and Marital Status; (9) Adoption Act, Cap 335 R.E 2002; (10) Children and Young Persons Act, Cap 13, R.E 2002; (11) Employment and Labour Relations Act, 2004: Medical Examination, Termination of Contract and Care of Welfare; (12) Workman's Compensation Act, 1982 Cap. 263 R.E 2002; (13) Disabled Persons (Employment) Act, Cap. 263 R.E 2002; (14) The Immigration Act, Cap. 54 R.E 2002; (15) The Refugees Act, Cap. 37 R.E 2002; (16) The Penal Code, Cap. 16 R.E 2002; (17) The Sexual Offences (Special Provisions) Act, 1998. Cap. 101 R.E 2002; (18) The Criminal Procedure Act No. 9 (1985). Cap. 20 R.E 2002; (19) The Prisons Act, 1967, Cap 58 R.E 2002; (20) Media: The Newspaper Act, 1976, Cap. 229 R.E 2002; (21) Media: The Broadcasting Services Act, 1993, Cap. 106 R.E 2002; (22) The Hotels Act, Cap. 105 R.E 2002; and (23) The Spirits Act, Cap. 222 R.E 2002. Caps zake zimetajwa na zitaonekana kwenye Hansard.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuleta jedwali la marekebisho ya Muswada huu linalozingatia maoni ya Kamati yangu na Wadau kwa kiasi kikubwa. Na kwa yale ambayo hayakupata nafasi bila shaka yatajitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria na marekebisho yanaweza kufanyika. Pia Kamati inamshauri Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuandaa Kanuni kwa ajili ya kutekeleza Sheria hii ya Kudhibiti UKIMWI katika kipindi kifupi mara baada ya Sheria kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni ya jumla, Kamati inashauri kuwa Serikali itumie rasilimali zake kwa nguvu zaidi kutilia mkazo kwenye kuwalinda wananchi asilimia 93 wanaosadikiwa kuwa hawajaambukizwa virusi vya UKIMWI. Wakati huo huo juhudhi ziendelee katika kuwajali watu asilimia 7 wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wagonjwa kwa kuwapatia huduma muhimu na dawa za kuwapunguzia makali ya UKIMWI. Aidha, dawa za kupunguza makali ya UKIMWI ambayo watumiaji

wanalalamika kuwa zinawaumiza badala ya kuwasaidia zifanyiwe uchunguzi na ikithibitika kuwa hazifai au zinawaletea madhara watumiaji hatua za kurekebisha hali hiyo zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna njia ya mkato zaidi ya kuendelea kuielimisha jamii kujikinga na kubadili tabia na kupima afya kila mara na hivyo tunaishukuru Serikali kwa hatua inazochukua ikiwa ni pamoja na kuimarisha kampeni ya watu kupima afya zao na kuongeza uwezo wa kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Pia Kamati inashauri Asasi zote zinazojishughulisha na udhibiti wa ugonjwa huu kwenda zaidi vijijini kutoa elimu ya UKIMWI.

Mwisho, tunapendekeza kuwa Muswada huu baada ya kuwa Sheria, itolewe tafsiri kwa lugha ya Kiswahili ya Sheria hii ili kila mwananchi aweze kuielewa vema ili kusiwe na visingizio vya kutoilewa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa kuwapongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa Dk. Aisha Kigoda, Mbunge, kwa ushirikiano waliota wakati Kamati ilipokuwa ikifikiria Muswada huu. Aidha, nawapongeza Wataalamu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Wilson Mukama na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati kutoa majibu ya hoja za Wabunge kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Kuzua na Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2007. Nawapongeza wadau waliojiandaa na kujitoneza kwa wingi kutoa maoni yao kuhusu Muswada wa Sheria hii. Kamati inathamini sana michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kazi ya mwisho kwa Kamati hii kabla ya Kamati kutoa Taarifa yake ya nusu mwaka na hatimaye kuundwa upya wakati wa Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja. Hivyo naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa namna ya pekee pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge na Kamati zote za Bunge kwa Ushrikiano tuliopata katika kutekeleza kazi zetu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao tumefanya nao kazi kwa karibu sana, na pia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara zote kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa namna ya pekee nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa umakini wao na kwa ushirikiano wao. Kwa heshima sasa naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii waliochambua Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI wa Mwaka 2007 kwa kuwataja majina:-

Mheshimiwa Dk. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dk. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Mariam

R. Kasembe, Mheshimiwa. Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Omari A. Mzee. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge wengine ni: Mheshimiwa Khadija S. Ngozi, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Usi Amme Pandu, Mheshimiwa Faustine K. Rwiolomba, Mheshimiwa Mwanakhamisi K. Said, Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim, na mimi Omari S.Kwaangw', Mwenyekiti. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kutambua ushirikiano wa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Theonest Ruhilabake, kwa ufanisi wa kazi yao kwa Kamati yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu. Msemaji Mkuu atakuwa Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali. (*Makofii*)

MHE. DR. ALI TARAB ALI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu muswada wa sheria ya Kuzuia na Kudhibiti VVU /UKIMWI Nchini ya mwaka 2007 (*The HIV AND AIDS (Prevention and Control) Bill, 2007*) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 52(6) (c) na Kanuni ya 85(6).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia za wale wote waliofiwa na wazazi wao, watoto wao na wake zao. Pia napenda kutoa pole kwa Wabunge wote kwa kumpoteza Mbunge mwenzetu, Marehemu Benedict Losurutia. Aidha, nawapa pole wapiga kura wa Jimbo la KITETO kwa kumpoteza Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara pamoja na timu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuhakikisha kuwa maoni yaliyotolewa na wadau yanafanyiwa kazi katika muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5 cha Muswada kinachosema nanukuu “*The ministry shall promote utmost safety and universal precautions...*” ili kuhakikisha kuwepo na kupungua kwa maambukizi ya VVU. Kambi ya Upinzani inaona kifungu cha 12 kingeondolewa kwa kuwa kifungu cha 5 kinakidhi yale yote yaliyomo. Neno *universal precautions* linatosha kabisa kubeba maana iliyomo kwenye kifungu cha 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba kupatiwa ufanuzi kwa baadhi ya vifungu kama vinavyosomeka katika Muswada huu. Kifungu cha 9 sentensi ya mwisho naomba kunukuu “... *distribution of condoms and support to people living with HIV and AIDS*” kwa kuwa lengo ni mpango wa kutoa elimu ya kinga ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa nini *condoms* zitolewe kwa waathirika tu badala kutolewa kwa wote? Yaani walioathirika na ambao hawajaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11 cha Muswada kinachohusu michango ya damu au viingo mbalimbali, ukiangalia kifungu cha 11(5) kinachoelezea makosa na adhabu zitakazotolewa, Kambi ya Upinzani inaona kifungu hicho cha 11(5) kwa kulinganisha na vifungu vilivyopo juu yake, hakina sababu ya kuwepo hapo. Na kama kitaendelea kuwepo ni bora adhabu ziwe ni zile zilizotajwa kwenye kifungu cha 47.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16(2) (c) kinachohusiana na matokeo ya vipimo vya VVU kuwa yanaweza kutolewa kwa mke, mme au mtu yeoyote wanayeshirikiana katika tendo la ndoa. Kifungu cha 16 (1) kinaongelea usiri/ unyeti wa matokeo ya vipimo kuwa majibu yatatolewa kwa yule aliyepima tu! (*Confidentiality of test results and shall be released only to the person tested*). Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri aeleze ni katika mazingira yapi matokeo ya vipimo vya HIV yatatolewa kwa washirika wake wa tendo la ndoa bila kuvunja mwiko wa usiri/unyeti (*confidentiality*)?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 26 (c) kinachohusu fidia kwa “*health practitioner*” ambaye anaweza kuambukizwa VVU wakati akiwa kazini. Kambi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa bora na muhimu kwa sheria hii kutamka aina ya fidia pindi janga hili litakapotokea au Muswada kwa maana nyingine ni kuwa unawataka *Health Practitioners* wote wawekewe BIMA na waajiri wao kama angalizo la yanayoweza kutokea hapo mbeleni. Hii ni sawa na ajali kazini (*high risk work*) na ajali kazini utaratibu wake wa kisheria unaeleweka na uko wazi. Mwajiri anatakiwa kuwawekea bima wafanyakazi wake. Kama haitawekwa katika sheria basi Mheshimiwa Waziri wakati wa kutengeneza kanuni jambo hili liwekwe wazi ili kuondoa uwezekano wa kuwasumbua na kuwakosesha haki zao wale wote watakaokuwa wamekumbwa na janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 27 kinachohusu kutoa taarifa au habari isiyo sahihi kuhusiana na tiba ya VVU na UKIMWI, kifungu hiki kinapendekeza taarifa itolewe pale tu itakapoendana na ushahidi wa tafiti za kisayansi (kimaabara) vinginevyo adhabu zimependekezwa. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki hakikuzingatia mazingira halisi ya waganga wetu wa jadi na ugumu wanaokumbana nao katika kuhalalisha madawa yao kuwa ya kisayansi. Hivyo basi, tunashauri kuwepo na kipengele katika sheria hii kitakachotoa mwongozo kwa waganga wa jadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 36 kinasema juu ya uanzishwaji wa kitengo cha utafiti kwenye masuala ya VVU na UKIMWI (*National HIV and AIDS Research Fellowship Committee*). Kwa kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inayo

kitengo tayari kinachojihusisha na utafiti wa magonjwa mbali mbali nchi nzima (*NIMR*), kwa kufanya hivyo ni kazi zile zile kufanywa na taasisi nyingine wakati mtoa fedha ni yule yule.

Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni kuongeza na kutokuwa na mpango mzuri wa matumizi ya fedha za walipa kodi, kwa kuanzisha kitengo kingine tofauti na *NIMR* kinachohusu tafiti za masuala ya VVU na UKIMWI badala ya kukiongezea nguvu kiutendaji kile kitengo kilichopo (*NIMR*). Kwa kufuata ushauri wa Kambi ya Upinzani, tafiti zinazohusu VVU na UKIMWI zitakuwa ni rahisi kuhusishwa (*coordinated*) na tafiti za magonjwa mengine kama vile kifua kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasisitiza kuwa mitaala ya elimu ya mabadiliko ya kimaumbile ya kijana anapotokea utoto kuingia kwenye utu uzima (life skills) na urahisi wa maambukizo ya VVU/UKIMWI ifundishwe kwenye vyuo vya ualimu na mashulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa taarifa yako. Sasa nitamwita Msemaji wa kwanza, atakuwa Mheshimiwa Mgana I. Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Benson Mpesya, halafu Mheshimiwa Said Nkumba. Nafikiri hao wanatosha kwa asubuhi hii.

MHE. VITA R. KAWAWA : Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA : Tafadhali mwongozo wa Spika!

MHE. VITA R. KAWAWA : Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wa Spika lakini... !

NAIBU SPIKA : Hauna Kanuni?

MHE. VITA R. KAWAWA : hauna Kanuni, naomba niendelee. Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge letu hili, Mkutano wa |Kumi, sijaona tukipatiwa hotuba za Serikali zinazohusu Miswada inayowasilishwa hapa Bungeni. Na pia hata hotuba za maoni kutoka Kamati hatujapatiwa, tunazoziona hapa ni hotuba za Kambi ya Upinzani tu. Juu ya yote sijaona ratiba ya shughuli za Bunge hili la Kumi. Asante sana.

NAIBU SPIKA : Nafikiri uko sahihi, jana pia nilipokuwa hapa Mezani nilidadisi kupata hotuba ya mtoa hoja na hotuba ya Kamati iliyoshughulikia shughuli hizi. Lakini ya Kamati ilikuja baadaye, nadhani Upinzani ndio wenyewe wameleta hii nakala. Kwa hiyo, ni utaratibu kwamba wazilet zile hotuba kabla hatujaendelea na kazi. Halafu ule utaratibu wa kazi, Kamati ya Uongozi imeendelea kuliangalia hilo swali linalohusika na ratiba. Tunaendelea! Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Lucy ajiandae.

MHE. MGANA I. MSINDAI : Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi nichangie juu ya Muswada huu. Nianze kwa kuunga mkono 100 kwa 100 na nimpongeze sana Waziri wa Afya na Naibu wake kwa kuleta Muswada huu pamoja na kwamba umeletwa kwa kuchelewa. Nasema kwamba umeletwa kwa kuchelewa kwa sababu kuna mambo mengi yamekwishafanyika kienyeji bila Wizara husika kuhusishwa. Lakini nina imani kuanzia sasa mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme *UKIMWI* sio maafa. *UKIMWI* ni ugonjwa kama malaria, kifua kikuu, ambayo yanamaliza watanzania wengi. Kwa hiyo, naomba kuanzia sasa tusiuite maafa, tuite ugonjwa. Na kwa sababu ni ugonjwa sasa mambo yake yote yahamie Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata hela nyingi sana kutoka kwa Wafadhili, fedha hizi hazipiti Wizara ya Afya. Kwa hiyo, kuanzia sasa tunaomba hizi fedha zianze kupita Wizara ya Afya kama fedha za *Busket Fund* zinavyopita. Na vilevile utengenezwe muongozo wa matumizi ya fedha hizi kama zile za *Busket Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema bila woga kwamba hizi fedha nyingi haziwafikii walengwa. Mimi niko kwenye Kamati ya kukagua mahesabu ya Halmashauri za Wilaya. Tumekagua Wilaya nyingi, na mpaka zingine tukawambia *CAG* aingie kwa undani. Mamiloni ya pesa yanapotelea kwenye makongamano, safari, vitafunwa, na hata wale walioathirika na huu ugonjwa hawafaidi.

Mifano ipo na mfano mmoja ambao tuliuufanya na taarifa ikatolewa na *CAG* ni Wilaya ya Nzega. Wahusika wachukue ile taarifa wataona. Na ni wilaya nyingi sana, zaidi ya $\frac{3}{4}$ ya Halmashauri za Wilaya hazitumii vizuri hizo fedha. Haziwafikii walengwa na kuna Wilaya zingine kabisa wagonjwa, watoto yatima na kadhalika hawapati msaada kutokana na hizo fedha. Kwa hiyo, namshauri kabisa Waziri wa Afya kuanzia sasa atakapotoa *regulations* zake hizi fedha ziwe chini yao zote zinazopitia *TACAIDS, Global Fund*, na zingine. Na kitengo hiki kama inawezekana kitoke kwa Waziri Mkuu, kwa sababu sio maafa, huu ni ugonjwa, kiende Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ametuambia hapa kwamba *percentage* ya walioathirika imeshuka. Mimi namwambia sio kweli, kwa sababu mpaka sasa watu waliopima ni wachache sana ukilinganisha na watanzania walivyo. Watanzania walioko vijijini hivi vipimo havijafika. Kwa hiyo, mimi naomba wafanye upya, waende vijijini. Na mimi najua kuna kampuni zinazouza *testing kits*, Waziri mwenyewe amewapa vibali lakini bado Halmashauri hazipati hivyo vipimo na hawajawa na ile kasma ya kununua. Fedha zinatengwa, zinaishia kwenye makongamano, safari, vitafunwa, haziendi kule. Naiomba sana Serikali iingilie kati hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna zahanati mpaka kwenye *grass roots*, bado haya mambo hayajafika. Wapimaji waende mpaka kule, kama hizi *testing kits* zimeruhusiwa na Serikali kwa nini zisipelekwe kule? Tunaishia hapa juu. Na hapa juu mimi sina wasiwasi kusema kwamba sio wote tunaopima, sisi viongozi tunadanganya tu. Wengi hatujapima na wengi hatupimi. Nafikiri kitengenezwe kipengele iwe ni lazima na sisi

tupime. Sisi tuwe kioo cha wananchi wetu, tunaogopa nini ? Kama nimeshapata virusi si ndio nianze kutafuta dawa, kwa nini tuogope ? Tunakwenda kwenye majukwaa kwa ajili ya kuwaonesha watu, wanapima wachache na wengine humo humo kwenye majukwaa wanatoroka. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalie upya hili jambo. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme bado unyanyapaa upo na upo maeneo yote. Bado wenye *UKIMWI* hawapati ajira, bado akijulikana mwenye *UKIMWI* anafanyiwa mizengwe anaondolewa. Kwa hiyo, huo ni unyanyapaa mkubwa kupita kiasi. Naiomba Serikali iingie ndani, huu ugonjwa utatumaliza. Tuwaheshimu na kuwashudumia wale ambaeo bahati mbaya walishaupata.

Huo ugonjwa unaweza ukampata mtu ye yote yule. Tunasema una njia nyingi za kuambukiza. Tunasema kwenye sindano, kwenye tendo la ndoa, na kadhalika. Sasa tuwaheshimu wale waliopata na tuwaheshimu zaidi wale wanaowahudumia walio na ugonjwa huu. Wengi sasa hivi wanaogopa. Tuwape bima ya kutosha na tuwawezeshe vifaa vya kutosha na sasa hivi kama inavyofahamika vifaa vingi vinavyotoka *MSD* sio imara vya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutafute njia nyingine tupate vifaa imara, tupate vitu vyote ambavyo vinahusu mgonjwa ahudumiwe. Na niseme hata hawa wa ushauri nasaha, mara nyingine wanawaogopesha watu wanaokwenda kupima. Wanatumia lugha ambayo mtu anaogopa. Kwa hiyo, tutafute njia zingine tuweze kusaidia kumaliza hili janga. Uhamasishaji bado haujawa tayari, haujaenea kote.

Tuna vikundi vingi sana vijijini, hivi vikundi vya utamaduni vikiwezesha ni wahamasishaji wazuri kuliko sisi tunaotoka Wilayani au Mikoani kwenda Taifani, tunakaa siku moja na kugeuza. Hawa walioko kule vijijini ndio wanaokaa na wananchi, hawa walioko kule vijijini ndio wanawajua kina nani wako kule. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kifungu cha 9. Kondomu tunasema wapewe walioathirika. Kwa nini isiwe lazima watu wote wapewe na ziende mpaka kwenye zahanati zetu? Na tuangalie ubora wa hizi kondomu, watalamu wanasema nyingi hazifai. Mimi sio mtaalamu lakini tuzichunguze lakini ziende kwa watu wote, kwenye majumba yote ya starehe, na nyumba zote za kulala wageni na kuwe na ukaguzi maalumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha sana kuona mabilioni yanayokuja kwa ajili ya *UKIMWI* hayawafikii walengwa. Mimi nirudie tena Serikali ipitie taarifa ya *CAG* watajua, hakuna kinachofanyika. Pesa zinakwenda zinatumika, na tumegundua Wilaya moja kiongozi wa ile Wilaya au wa Serikali Kuu au Halmashauri walipewa zaidi ya milioni moja. Waligawiwa tu milioni moja, wanaambiwa za kuhamasisha *UKIMWI*. Taarifa hazikurudi kuonesha wamehamasisha wapi, na kazi gani zimefanya. Kwa hiyo, ni lazima tujipange upya. Mheshimiwa Waziri wa Afya, nirudie kusema kuwa hili jukumu ni lako, kama viko vitengo vya kusaidia vingi havifikasi kwa walengwa. Sasa mjipange upya tunataka kuona watanzania wote wanapata huduma zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

MHE. LUCY F. OWENYA : Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote napenda kutoa pole kwa familia pamoja na Wabunge kwa kufiwa na Mbunge mwenzetu, Benedict Lesurutia. Hapo hapo napenda nitoe pole kwa familia, ndugu na marafiki wote waliofiwa na ndugu na jamaa kutokana na ugonjwa huu wa *UKIMWI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumpongeza Mchungaji Getrude Rwakatare, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalumu. Pia napenda nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kuleta Muswada huu Bungeni japo kwangu naona kama umechelewa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *UKIMWI* ni janga la Taifa na Dunia kwa ujumla. Kwa kiasi kikubwa *UKIMWI* umepunguza Nguvu Kazi ya Taifa. *UKIMWI* umeongeza magonjwa mengi hata yale ambayo yaliyokuwa yamedhibitiwa kama vile kifua kikuu na hatimaye umefanya uchumi na maendeleo yetu kurudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba kutokana na takwimu za Taifa, asilimia 93 ya watanzania bado hawajaambukizwa *UKIMWI*. Na milioni mbili ya watu wameambukizwa *UKIMWI*. Lakini cha kusikitisha ni kwamba pamoja na watu kuwa na *awareness* ya kujua kwamba *UKIMWI* ni ugonjwa hatari lakini bado maambukizi mapya yamezidi kuongezeka. Hii ni changamoto kwetu sisi, bado kuna matatizo ya udhibiti wa *UKIMWI* na hili ni tatizo la Taifa pamoja na watu kwa ujumla, ina maana watu bado hawajabadilisha tabia na mienendo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya umasikini wetu kwa sasa hivi mtu wa kawaida Tanzania anaishi kwa kiwango cha chini ya dola moja kwa siku. Ukizingatia elimu ya *UKIMWI* imejikita zaidi mijini, kule vijijini bado watu hawajapata ufahamu wa kutosha. Kwa maana hiyo tumeelezwa kwamba kudhibiti *UKIMWI* ni kubadilisha tabia, kutumia kondomu, kuwa mwaminifu na mwenzi wako au kutokufanya tendo la ndoa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swal langu ambalo nataka Mheshimiwa Waziri atueleze, kutokana na umasikini wetu Tanzania wakati kondomu huwa hazipatikani, na zikipatikana nyingine zinauzwa na watu hawawezi *ku-afford* hizi kondomu ; je, ni watanzania wangapi wataweza *ku-afford* hizi kondomu ? Hata kujinunulia chakula ambacho ni lishe bora kwa wale walioathirika ? Nafikiri Muswada huu ungewasaidia wale wote ambao wameathirika ambao wanahitaji kondomu waweze kupewa kondomu bure ili tuweze kupunguza maambukizi kwa ile asilimia 93 ya wale watu ambao bado hawajaambukizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 26 katika Muswada, napenda nimpongeze Waziri kwamba wametambua kwamba wale wanaohudumia wagonjwa wa *UKIMWI* watapewa fidia. Lakini katika Sheria wangetamka wazi kwamba watafidiwa kiasi gani ili waweze kuwa na motisha ya kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada kifungu cha 13 kinazungumzia kuhusu *HIV Testing Centres*. Katika vyombo vya habari, magazeti na kadhalika, tumeona kwamba wamekuwa waki-complain kwamba hizi *testing kits* nyingi hazijawa *approved* na WHO. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri, atatueleza ni vipimo gani ambavyo Tanzania vimekuwa *approved* kutumia? Kwa sababu tumeona kuna watu wengine wanaenda kupima UKIMWI wanaambiwa kwamba hawana, baadaye unakuta wanaao UKIMWI. Sasa Mheshimiwa Waziri, angeeleza vizuri kabisa hizi *Testing Centres* zinaanzia katika ngazi ipi? Kwa sababu hizi damu zikipimwa zinakuja mpaka ngazi ya Wilaya, je, kule chini kwenye vijiji itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kifungu cha 14 wamezungumzia kwamba kutakuwa na mambo ya *counselling*, kutakuwa na *Training Centre*. Sasa sijui hizi *training*, I mean kutakuwa na washauri nasaha ambao wameenda kufanya *training*, sijui hivi Tanzania kuna vyuo vingapi vya kufanya *training* kwa ajili ya *counselors*? Na kama hiyo *training* ipo katika *scheme of service* ya Wizara?

Vilevile kwa ufahamu wangu Tanzania hatuna hawa *clinical psychologists*, sasa hii sheria kama hatuna vitu vyote hivi sidhani kama tutaweza kuitimiza. Kwa sababu watu wengi wanaokwenda kwenye *training*, wengine wanakwenda kwa wiki mbili wanapewa *certificate* tu, ndio maana inapelekea watu wanaenda kupima wanapopata ushauri nasaha, hawashauriwi vizuri. Wengine waenda kupima hawachukui majibu wanakimbia, wengine wanaenda kujinyonga, na kadhalika kwa sababu ushauri nasaha bado haujawekewa mikakati madhubuti jinsi ya kutoa ushauri kwa sababu hawapati mafunzo ya kutosha. (*kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 47, kinachozungumzia kwamba maambukizi ya makusudi, hapa kidogo nachanganyikiwa, maambukizi ya makusudi ni maambukizi ya namna gani? Utaelewaje mlalamikaji anaenda kulalamika kwamba nimeambukizwa kwa makusudi? Utaelewaje huyu mtu kama alikuwa hana UKIMWI kabla?

Tunaelewa kabisa kwamba ukienda kupimwa UKIMWI leo kuna ile *window period*. Nikipima leo sio lazima kwamba sina UKIMWI. Na mtu ukipimwa mara moja usifikirie kwamba huna UKIMWI, kwa siku ile uliyoambiwa huna UKIMWI, kuna ile *winodow period*. Sasa hapa tutaelewaje? Mtapima kwa kiasi gani kuelewa kwamba mtu huyu ameambukizwa, alikuwa na UKIMWI kabla, pengine anamtumia mwanadamu mwenzake kucheki kama ana UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona kifungu hiki kina utata kidogo, kwa sababu watu wengine hawapimi UKIMWI. Kweli anaweza akakutana na mwenzi wake wakaenda wakafanya tendo la ndoa, yule mwingine akawa na makusudi yake pengine alikuwa na UKIMWI anaamua kumkomoa mwenzake, anasema kwamba nimemwambukizwa na huyu. Kwa hiyo, hii itakuwa ngumu kweli kujua kwamba mtu huyu ameambukizwa UKIMWI kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kuna hizi *blood donations*. Sasa kama tulivyosema kuna hii *window period* mtu anaenda kupimwa leo anajitolea damu unakuta damu yake haina UKIMWI, na vipimo vingi vinapima *antibodies* hazipimi *virus*. Sasa kama hospitalini wakimwekea mtu damu ambayo ina ugonjwa sheria hii hajasema kitu chochote kuhusu yule mgonjwa atafidiwa kiasi gani kama ameambukizwa kwa bahati mbaya kutoka hospitalini ? Pia sheria ingeeleza hili. Kwa sababu uwezekano wa kupewa damu ambayo siyo sahihi upo. Manake ukinipima leo ukichukua damu yangu ukampelekea ndugu yangu hospitalini pale ukute baada ya *six weeks* nakuja ku-discover nina *UKIMWI*, itakuwaje ?

Baada ya kusema hayo machache Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. BENSON M. MPESYA : Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Muswada huu, Muswada ambao nimebahatika kuupitia na vilevile wapiga kura wangu ambao nilibahatika kupata maoni yao. Nimeomba leo nisimame na kuwasilisha yale ambayo yanatoka kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini.

Kwanza kabisa Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii na mimi kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu za dhati kwa wenzetu wa Kiteto kwa kupotelewa na aliyekuwa Mheshimiwa Mbunge wao. Naomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu ambacho wanamkosa mwakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze na sehemu ile ya kwanza ambayo inatoa jina la Muswada huu. Sina matatizo na kichwa cha Muswada kwa sababu lengo kubwa kama tunavyojuua ni kuzuia pamoja na kudhibiti. Lakini ninachotaka nizungumzie juu ya kichwa hiki wananchi wengi wanaona kwamba tulichelewa katika kuileta sheria hii, hivyo sheria hii tumeileta kwa wakati muafaka. Kwa sababu inawezekana kabisa wewe unawenza ukawa hujafikwa na hili lakini jirani yako tayari yamemfika ya namna hii.

Kweli kabisa tunashuhudia tukiwaona wenzetu ambao wanajitambua wazi kwamba wana virusi na wanafanya kazi ya kuvieneza kwa makusudi mazima. Kwa hiyo, wananchi wa Jimbo langu la Mbeya Mjini wamenitura niseme kwamba wanaafiki kabisa Muswada huu kuletwa, unaletwa katika wakati ambao ni muafaka ili tuokoe maisha ya watu wanaobaki na Tanzania yote kwa ujumla. Vilevile wale wenzetu ambao wameathirika tusiwe na *stigma* ya aina yoyote kwao waweze kuwa katika maisha yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 3 kifungu cha 7 juu ya elimu kwa umma. Katika suala hili naomba niseme tu kwamba yapo malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba pengine katika elimu hii ya umma wale wenye nafasi tunajipendelea sana tunapotangaza tunapokuwa na matatizo ya ugonjwa huu. Kule kwetu hasa kwenye misiba anapokuwa amekufa mtu mkubwa na inaeleweka wazi kwamba pengine mwenzetu alikuwa na matatizo haya, taarifa zake za msiba ule zinafichwa fichwa. Pengine ndio usiri

wenyewe, lakini pindi anapokufa mtu wa kawaida mambo haya huwa yanawekwa bayana kwamba huyu ametutoka kwa sababu ya ugonjwa wa kisasa au *UKIMWI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba hali ya namna hii basi kwa wale wenzetu ambao wanapewa jukumu la kutoa elimu hii, ugonjwa huu hauchagui mwenye nafasi na asiyekuwa na nafasi ni ugonjwa wa watanzania wote. Kama tunaamua kutoa elimu, elimu hii iwasaidie watanzania wote bila kuwaweka katika mafungu ya huyu tumfichie siri yule tusimfichie siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 4 hasa kifungu cha 15 kupima kwa hiari, naomba wakati mwinge itabidi labda tubadilishe kabisa hii hali. Kama tunazungumzia juu ya haki za binadamu, hata wewe unapomwambukiza mtu virusi unafanya hivyo kwa kukiuka haki za binadamu. Sasa mimi nakumbuka tulikuwa na wakati tulikuwa na ugonjwa wa kifua kikuu. Kila mtu alikuwa anajua kabisa pale kijijini kwamba huyu ana matatizo ya kifua kikuu. Na ndio maana tulipata nafasi ya kuutokomeza ugonjwa huu haraka sana. Pamoja na kusema pengine bado hatujautokomeza kabisa kabisa lakini tofauti kabisa na ilivyokuwa mwanzo. Mimi napendekeza kwamba inapofika mahali mgonjwa analalamika na ugonjwa haueleweki basi ni vema hata bila hiari vichukuliwe na vipimo vya *UKIMWI* kwa mgonjwa huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya hivi kwa akina mama wajawazito na imetusaidia sana, na ndio maana mama anapokwenda kupima kama ni mjamzito kupima *UKIMWI* si hiyari. Na ndio maana sasa utakuta hata watoto wanaozaliwa wanazaliwa wakiwa wengi, hawana maambukizi ya *UKIMWI* kwa sababu tayari iligundulika mapema na akina mama walianza kupata zile dawa zinazostahili. Lakini hii hatua tunayokwenda waswahili husema, au wahenga husema *mficha uchi hazai*. Kwa hiyo, naomba hili lieleweke wazi, kama kweli tunataka kudhibiti lazima wakati mwinge anayekwenda hospitali anaumwa achukuliwe na vipimo vya *UKIMWI* ili tujue mwenzetu ana matatizo tuweze kumsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kifungu cha 11 ambacho kinahusu adhabu, naomba niwasilishe maoni ya wananchi wa Mbeya, wanasema kuwa adhabu hii ni kubwa mno ya kufungwa kifungo cha maisha. Kwa sababu moja, ninapewa taarifa hapa na jirani yangu wa Nkasi kwamba kifungu hicho kimefutwa lakini... !

NAIBU SPIKA : Unamsikiliza Spika tu siyo... !

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa ushauri wako. Naomba niseme tu kwamba wataalamu wa sheria hapa mpo. Mtanieleza wazi kwamba kwa kweli kifungo cha maisha mpaka sasa hivi katika Tanzania bado hatujauja ni miaka mingapi ?

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya kwanza ilikuwa inajulikana mwanzo kabisa kwamba unaposema kifungo cha maisha ni miaka 30. Sasa kifungo cha maisha sasa hivi ni kipi ? Na kama huyu mtu anayefungwa leo kwa kusambaza *UKIMWI* alikuwa na watoto, watoto tunampa nani jukumu la kuwalea ? Kama ye ye tunamfunga maisha. Kwa

hiyo, naomba adhabu hii ipunguzwe. Kwa sababu lengo la adhabu ni kumfanya huyu ajutie yale anayoyafanya, ajirekebishe na hatimaye awe raia mwema. Adhabu si kumkomoa. Sasa napendekeza kama ikiwezekana adhabu ipunguzwe iwe miaka mi 5. Sijaleta *Schedule of Amendment*. Mwisho nimalize kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, ni hayo machache niliyonayo. Asante.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sikonge, napenda vilevile niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Kiteto kwa kuondokewa na Mheshimiwa Mbunge wao marehemu Lusurutia. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rwakatare kwa kupata Ubunge. Nakukaribisha sana Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niungane na wachangiaji walionitangulia kumpongeza Waziri na Wizara kwa kuleta Muswada huu. Niungane nao kwa kusema kwamba umechelewa lakini pamoja na kuchelewa sasa tuufanyie kazi. Nianze moja kwa moja na fedha za UKIMWI zinazokwenda wilayani kuitia *NGOs* na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za UKIMWI, naweza nikasema hazina mwenyewe. *NGOs* nydingi sana zinaota kama uyoga kudaka hizi fedha na zinatumika katika utaratibu ambao kwa kweli haziwanufaishi wale ambao fedha hizi zimeleengwa ziwafikie. Niombe Serikali ielekeze nguvu zake kuitia Wizara mbayo kwa kweli iko pale na ina wataalamu mbalimbali, hizo *NGOs* hazina hata wataalamu wa afya lakini fedha hizi zinakwenda.

Juzi juzi nilikuwa kwenye kikao cha UKIMWI kwenye Jimbo langu, huwezi kuamini kwamba baadhi ya *NGOs* zinafika mahali mpaka zinanunua dawa. Dawa zile kwa mfano mgonjwa akiwa na vipele zinakwenda zenyewe kununua. Hii ni hatari sana, kuendelea kuruhusu mambo ya namna hii bila kuzingatia utalaamu. Kwa hiyo, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuhakikisha kwamba Wizara sasa ipewe jukumu lake la kuhakikisha inashughulikia magonjwa yote kama tunavyoshughulikia malaria, kifua kikuu. UKIMWI sasa uondolewe Ofisi ya Waziri Mkuu upelekwe Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili tuweze kupata ufanisi katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kuzuia baadhi ya nguo zisizofaa kazini. Nguo hizi ni kichocheo kikubwa sana cha ngono holela, niombe kasi hii isibaki kazini iendelee hata huko mitaani. Wengine tukipita tunaona kichefuchefu. Unakuta mtu amevaa nguo ya ajabu. Kama nguo aliyovaa inafanana na ngozi yake akiwa mbali huwezi ukajua amevaa ama hakuva jinsi ilivyobana. Watanzania tunapoteza maadili yetu kwani huko nyuma hatukuwa tunavaa hivyo, utandawazi utatumaliza. Niiombe Serikali kwa kweli ielekeze nguvu zake katika kuhakikisha kwamba Watanzania tunaendelea na maadili yetu ya zamani ya kuva nguo ambazo akionekana tu mtu anajua huyu ni Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ushauri nasaha, nimekuwa nalisema sema sana. Hili toka siku za nyuma sipingani sana na watu waliobuni lakini sioni hoja ya

msingi sana ya kuliendeleza. Sasa hivi tunataka kuliendeleza tena watu wengi waanze kupata mafunzo ya wiki ya moja, mbili na kadhalika. Mimi nimetoka nyumbani kwangu nasema nakwenda kupima UKIMWI, nafika pale tena mshauri nasaha ananiuliza uko tayari kupima, namjibu niko tayari kupima ndiyo maana nimekuja mpaka hapa.

Kama nisingekuwa tayari nisingekuja hapa, hofu ya kwanza hiyo inaanzia hapo lakini na mambo mengine mengi utapewa pale, ndiyo maana idadi kubwa ya watu wanaopima wengi wao hawachukui vipimo, majibu hawayachukui. Mtu umekuja umejiandaa unafika pale unapewa maelezo mengi ambayo yanakufanya uchanganyikiwe. Huu ugonjwa ni wa kawaida tu mbona wanaopima malaria hawapati ushauri nasaha na malaria inaua watu wengi zaidi kuliko UKIMWI? Sipingani na utsalamu lakini vilevile wale ambao kwa kweli wanapata nafasi ya kuwapa ushauri nasaha basi wawe ni wataalamu ambao kwa kweli wamebobea katika hilo lakini vilevile wamepata mafunzo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya UKIMWI, ningeomba ianzie shulenii hasa shule za msingi maana takwimu zinatuonyesha kwamba matendo haya yanaanza huko. Mitaala iandaliwe haraka, kwa kufanya hivyo basi mafunzo haya yanaweza yakasaidia vizazi vijavyo kuweza kuwa na elimu ya kutosha ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kampuni kadhaa zimepewa kibali na Wizara ya Afya kufanya zoezi la kupima Ukimwi hasa kwa kutumia vipimo vyta kujipima mwenyewe. Kwanza suala la kujipima mwenyewe naliunga mkono sana kwa sababu ukijipima mwenyewe utakuwa na maamuzi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja kwamba ni vizuri vifaa hivi kweli vionekane kuwa vina viwango sahihi.

Kwa sababu mnaweza mkawa na vipimo vingi kumbe havitoi majibu ambayo kwa kweli mtu anastahili kuyapata. Lakini vilevile ningeomba Halmashauri za Wilaya nazo zingekuwa moja ya vyombo ambavyo ni mawakala wa kusambaza hivi vifaa hasa katika zahanati zake ambazo ndiyo ziko karibu sana na wananchi huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho suala la upimaji tumesema ni hiari. Lakini niungane na Mheshimiwa Msindai kwamba sisi viongozi tuwe wa kwanza kupima. Hata tulipokwenda kwenye upimaji Nyerere *Square* sio Waheshimiwa Wabunge wote walikuwepo. Sasa inawezekana wengi tulikuwa na dharura, lakini vipindi vilivyofuata tulipima? Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuonyesha mfano yeye na mke wake na sisi tuige. Ni viongozi wangapi wanaokwenda kupima na wake zao? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Au na wanaume zao?

MHE. SAID J. NKUMBA: Au na wanaume zao.

MBUNGE FULANI: Sawa sawa.

MHE. SAID J. NKUMBA: Haipendezi na wananchi wametuona tunasimama majukwaani tunasema UKIMWI ni tatizo lakini hatuonekani katika maeneo ya vipimo. Mimi nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge ambao kila linapotokea jambo la upimaji hapa wanajitokeza. Wale ambao mpaka leo hawajapima tupime, ukipima unajua afya yako lakini vilevile ni mtiririko wa viongozi wa Serikali na wanasiasa wenzangu huko katika maeneo ya wilaya na mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu, naomba nichukue nafasi kukupongeza na niishie hapo, asante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Sio tu waliopima hata waliopima siku ile hawajarudia mara ya pili waliambiwa warudie mwezi wa kumi hivi hawajarudi, kwa hiyo kweli kabisa mrudi mkapime.

MHE. SUSAN LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa kudhibiti UKIMWI. Lakini kabla ya kutoa hoja zangu ningependa kuungana na wananchi wa Kiteto kwa ajili ya kutoa pole kwa kupotewa na Mbunge wao Mheshimiwa Benedict Losuritia. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza na kumkaribisha sana Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba UKIMWI ni janga la taifa, kimataifa lakini pia nikutokana na ukweli huo Muswada huu ulipata wadau wengi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema. Hii inaonyesha ni jinsi gani suala la UKIMWI linavyowagusa wananchi wengi. Naomba niishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu ili baadaye uwe sheria kwa sababu tatizo hili limekuwepo kwa muda mrefu kama ambavyo tunajua UKIMWI umeanza toka miaka ya 80 huko Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupongeza Muswada huu nina *concerns* zangu ambazo nadhani Mheshimiwa Waziri anaweza akazichukua. Ni wazi kwamba suala la UKIMWI sio suala linalohusu sekta ya afya peke yake ni suala ambalo linahusu sekta mbalimbali. Ni kwa sababu hiyo basi nafikiri kwamba suala la UKIMWI kuwekwa katika Wizara ya Afya nadhani ni tatizo kwa sababu wote tunajua ni jinsi gani UKIMWI unavyosambaa kuanzia hospitalini lakini hasa huko nyumbani na ndiyo sababu wagonjwa wanapozidiwa hurudishwa nyumbani, hivyo pale Wizara ya Afya inakuwa haipo.

Pia tukiangalia Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) iko chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nafikiri kwamba ni muhimu kabisa suala la UKIMWI likawa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu Ofisi hiyo inaweza kutumia Wizara nyingine, kwa mfano kama nilivyosema suala la UKIMWI liko mpaka katika familia na tunajua Wizara ya TAMISEMI inahusika. Kwa hiyo, nafikiri kwamba kwa kuwa Wizara ya TAMISEMI iko chini ya Waziri Mkuu basi ni rahisi zaidi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuweza kuiagiza au kuituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kilichonifanya nisimame zaidi ni kuhusu adhabu. Ni kweli kwamba katika Kamati tuliongea hili, mwanzoni ilikuwa ni kifungo cha maisha

lakini sasa hivi imerekebishwa na kuwa kati ya miaka mitano hadi kumi. Mimi sina kipingamizi na kifungo, tatizo langu liko kwenye suala zima la jinsi gani mtu atakuwa amemwambukiza mtu kwa kukusudia (*intentional*).

Mimi ninavyoelewa *intentional* ni makusudi lakini tunavyojuu ni kwamba mpaka mtu ajulikane kwamba ana virusi nya UKIMWI kuna kitu tunaita *window period or incubation period* ambayo ni miezi mitatu hadi minne. Kwa hiyo, inaniwia vigumu kuona kwamba kwa sayansi tuliyonayo hapa Tanzania inawezekana kabisa yule aliye kwenda kushitaki ikawa ye ye labda ndiye amemwambukiza yule anayelalamikiwa kwa sababu bado haitajulikana virusi nya yule vina umri gani na nya yule anayelalamika ni nya umri gani. Sasa kuna haja kwa Wanasheria na wataalamu wetu kutueleza ni jinsi gani watajua yule aliye lamikiwa kweli ndiye amemwambukiza kwa sababu pale kuna kipindi cha *window period* cha miezi mitatu mpaka minne. Je, virusi hivyo vinaweza kugundulika kwa umri? Na pia tunaangalia *strain of the HIV* kwamba je, vinafanana? Ni nya *type* moja? Kwa hiyo, tuijilize, je, Tanzania tumekwishafikia sayansi hiyo kwamba tuna vipimo ambavyo kwa kitaalamu vinaitwa *phylogenetic analysis*? Je, tunavyo na kama hatuna hatuoni kwamba tutakuwa hatumtendei haki yule ambaye amelalamikiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kisayansi kuna watu ambao tunawaita HIV carriers ambao kimsingi hawaambukizi lakini wana vile vijidudu tu, je, atakapokwenda kupimwa akakutwa kweli anavyo lakini hajaambukiza ni *carrier*, hapo wataalam wanatwambiaje? Hatuoni kwamba tutakuwa hatumtendei haki? Kwa hiyo, naomba masuala haya pia yaangaliwe kwa undani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua kwamba kwa waathirika dawa namba moja kwa ajili ya afya zao ni lishe bora. Sasa tunapomfunga huyu mwathirika je, magereza yetu yatakuwa tayari kuwapatia milo ili waweze kuendelea kuishi au wataendelea kupata mlo mmoja kama ilivyo kwa wafungwa wengine? Naomba pia hilo tulitazame.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naliona kwa waathirika ni kwamba kitaalamu tunajua kwamba kuna *stages* mbalimbali mpaka mtu anapofikia hatua ya UKIMWI na kwamba wataalamu wanatwambia vile vijidudu *sometimes* huwa vinashambulia ubongo. Je, tutajuje kama mtu huyu amekuwa *insane* kiasi kwamba vile vitendo anavyovifanya siyo kwa sababu ya akili zake ni kwamba tayari amekwishaanza kuchanganyikiwa? Je, hilo wataalam wanatwambiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujuu kama Tanzania wameridhia Mkataba wa Kimataifa, kuna Mkataba wa Kimataifa ambao unasema, naomba kunukuu: “*Criminal and all public health legislations should not include specific offences against the deliberate and intentional transmission of HIV but rather should apply general criminal offences to this exceptional cases*”.

Sasa naomba kujulishwa kama Tanzania tumeridhia huu Mkataba wa Kimataifa na kama tumeridhia ni kwa nini tunakiuka kwa kuwafunga watu ambao wanasambaza virusi kwa makusudi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba niongelee kifungu cha 26 kinachozungumzia *health practitioner who is exposed or affected with HIV*. Mimi naomba kufahamu, hivi watajuaje kama huyu muuguzi au mfanyakazi wa afya ameathirika kutokana na kazi anazofanya na si kwa matendo yake ya ngono, yaani amefanya ngono zembe? Kwa nini huyu mtu kama amefanya ngono zembe alipwe wakati watu wengine hawalipwi? Kuna utaratibu gani? Pia kama nilivyosema awali ni kwamba, wagonjwa wa UKIMWI hawakai tu hospitalini, wapo majumbani na tuna ushahidi tosha kwamba mabibi na mababu zetu wameathirika sana kwa kuwaugiza watoto wao au wajukuu zao majumbani. Je, wao wametengewa fidia ya aina gani, maana hapa inaelekea ni watu wa afya tu, je, wale ambao wanahudumia wagonjwa ambao tuseme wanasaidia Wizara ya Afya wao wanasaidiwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba, kwa kweli nakubaliana na Muswada huu lakini naomba sana Wizara na Serikali kwa ujumla iangalie ni jinsi gani itawatendea haki wanaoshitakiwa kwa sababu kama tunaongelea suala la kuambukiza kwa makusudi ugonjwa wa *HIV* na UKIMWI bado tuna magonjwa mengine yanaambukiza na yanaua kama *cholera*. Je, hayo nayo tunafanyaje kwa sababu kuna watu wanaambukiza wenzao na wanakufa kwa *cholera* hilo tunalichukuliaje? Hatuoni kwamba tukianzisha hii ya *HIV* peke yake ni kuendelea kuwanyanyapaa wagonjwa hawa? Kwa hiyo, nadhani tunapaswa kuangalia kwa undani ili haki itendeke kwa wagonjwa hao ambao kwa kweli kimsingi wana matatizo makubwa sio tu ya afya lakini pia ya kisaikoloja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. (*Makofii*)

MHE. PROF. IDRIS MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nichangie kuhusu Muswada huu. Awali ya yote uniruhusu nitoe rambi rambi zangu na za wananchi wa jimbo la Rufiji kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Benedict Losurutia na kwa kifo cha mke wa Mheshimiwa Mbunge Adam Malima na kwamba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marchemu hawa mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe pongezi nyingi kwa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri waliyoifanya kutuletea Muswada huu. Nampongeza hususan Waziri wa Afya, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wakuu wote. Vilevile ningependa nitoe pongezi kwa *NACP* na *TACAIDS* kwa kazi nzuri waliyoifanya. Katika Muswada huu jambo kubwa ni kuzuia na hatua kubwa iliyochukuliwa na Mheshimiwa Rais na mke wake na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu kupima UKIMWI hadharani, pamoja na Mheshimiwa Spika na mke wake, Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge na wananchi wote. Kazi hii nzuri sana imefanya uchunguzi wa hivi karibuni kuonyesha kwamba UKIMWI umeteremeka kutoka asilimia saba kwenda mpaka asilimia tano. Hili jambo

kubwa na kwamba shughuli zilizofanywa na *NACP* na *TACAIDS* zimewezesha kuwepo na ufahamu wa watu (*public awareness*) kuwa UKIMWI ni nini. Ufahamu mefikia asilimia 99, hili ni jambo kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nigeukie Muswada hasa katika kifungu cha 2 chote hiki ndiyo *actually point* kubwa kabisa. Hapa kuna jambo nafikiri tusilionee haya, kwamba zimetajwa tu mila zisizopendeza yaani bila kutaja kweli kweli. Kwa mfano, kuna mila potofu ya kurithi wajane, mimi nadhani itamkwe wazi wazi kwamba hilo jambo sasa lifutwe kabisa nchi nzima isitokee kwamba mtu anamuwahi mjane aliyefiwa, hasa kama mjane huyo mume wake amekufa kwa UKIMWI.

La pili, yako makabila Mikoa ya Ziwa Victoria wana mpango wa kumtakasa mjane, yaani mume akifa basi yuko jamaa mmoja ye ye anakwenda kumtoa ukiwa hata wiki mmoja hajifika baada ya kilio. Mila kama hizi tusizichekee na ninaowasema makabila yao wako hapa hapa Bungeni. Serikali ipitishe amri kukataza kabisa kurithi wajane na kufanya vitendo hivi vya kutakasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine hapo hapo katika kifungu cha nne, zipo mila njema zinazosaidia kuzuia maambukizi ya UKIMWI. Katika uchunguzi uliofanywa Afrika Kusini, Kenya, Uganda na hapa kwetu umeonyesha wazi wazi kwamba mwanaume aliyetairiwa *male circumcision* inasaidia kukinga maambukizi kwa asilimia 60. Sasa kama tunaweza kupata asilimia 60 ya wanaume wetu wanaweza kuwa wanajikinga kwa jambo dogo tu la kutairi, naomba hili tusilionee haya, tuliseme waziwazi na kwamba kifungu hiki kiandike kabisa kwamba kutairiwa kwa wanaume kunapunguza UKIMWI kwa asilimia 60. Baada ya kusema hivi naiomba tena Serikali isione tabu kulifanya hili jambo la kutairi liwe *friendly*. Jamaa wasilione kama jambo bayu sana ili nchi nzima wanaume wataairiwe na tukawa na hakika na waliohairiwa, asilimia 40 tu ndiyo watakaokuwa na hatari ya kuambukizwa UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine la kufuatilia matatibu ya UKIMWI. Huwezi kufanya hivyo mpaka kwanza uwe na mashine kwa mfano *CD4 counting machine* na *viral load counting machine*. Mashine hizi ni ghali hazipatikani kwa urahisi, kwa hiyo, naomba kwamba Serikali ijotoe mhanga na kununua mashine hizi kwa wingi ili tuweze kuwafuatilia wanaotibiwa nchi nzima.

Lingine ni suala la *HIV test kits*. kwa hali tu iliyofika sasa kwa kila mtu anafahamu *HIV* na kwamba sera ya afya inataka kulenga kila Kata iwe na Kituo cha Afya kilichopanuliwa na kinachoweza kufanya operesheni ya kina mama. Damu inatakiwa na damu hii lazima ipimwe. Kwa hiyo, ununuzi wa *HIV test kits* lazima upanuliwe ili *HIV Test Kits* ziweze kufikia hatua kama ilivyo malaria mtu akienda mahali anapimwa *BS* na vilevile aweze kupata kipimo cha *HIV*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine ambalo Muswada huu upo kimya nalo ni lishe bora. Lishe bora haikutajwa vizuri kama ni moja kati ya njia za kuzuia sio maambukizi tu lakini ni kuudhibiti ule ugonjwa wenywewe. Mtu anayekula vizuri na viini

lishe nya kutosha mtu huyu kinga yake ya mwili huzidi na kwa kweli anaweza akaishi na virusi nya UKIMWI kwa muda mrefu zaidi kabla ya kufikia hatua ya mwisho ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nizungumzie juu ya haja ya kuwa na mabadiliko katika fikira na mtazamo wetu juu ya ugonjwa wa UKIMWI. Unyanyapaa na ubaguzi na kuonyeshana kidole, yule ana UKIMWI ni tatizo kubwa sana katika kuzuia na kudhibiti UKIMWI katika nchi yetu.

Hatua ya kwanza mtu anaogopa kujitokeza, anaendelea kuumwa chini chini, lakini kama alivyosema Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwamba “ukificha ugonjwa kilio kitakuumbua“ na ukweli ni kwamba hawa watu huja hospitalini wakiwa taabani kabisa. Unamcheiki unakuta *HIV CD4 count zero*.

Tumekwishapata wagonjwa wa namna hiyo tumewasaidia, lakini hakuna jambo kubwa kuliko kukubali kwanza kwamba UKIMWI ni ugonjwa mtu huuogopi. Kwamba njia nzuri ni kujipeleka na kwenda kupima mapema na ukipimwa mapema na ukaanza matibabu mapema, utapata faida ya matibabu hayo na nchi hii itapata faida kubwa. Kwa sababu wewe umesomeshwa kwa fedha nyingi na wewe unataka utoe mchango wako kwa taifa hili na kwa familia yako. Sasa hivi tuna rekodi ya watu waliofika zaidi ya miaka 25 wanakula dawa na wanaendelea vizuri. Naomba kufahamu kwa nini watu huona ufahari kusema kwamba nina malaria, shinikizo la damu, lakini wanaficha UKIMWI? Jambo jingine ni kwamba tumekwishaona kuwa mgongwa wa UKIMWI akitibiwa vizuri na mgonjwa wa shinikizo la damu, wote wataendelea kuishi vizuri kwa muda mrefu na watatoa mchango mzuri. Lakini kinyume chake ni kwamba lazima wote waanze matibabu mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naiomba sana Serikali ikubali tu kujitwisha mzigo kwamba sasa *HIV testing kits* itapelekwa katika sehemu yote inayotolewa huduma ya afya katika nchi yetu kwa mfano wa BS kwa malaria.

La pili, naomba sana kwa vile adui mkubwa katika kudhibiti UKIMWI, elimu ya UKIMWI *HIV and AIDS*, elimu ya kuwaonya vijana na elimu ya kuwaambia msingi wa ubinadamu kwamba hamna kunyanyapaa UKIMWI iingizwe katika mitaala ya elimu katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema sioni haya, nyumbani kwangu tunakula nao, tunaishi nao halafu unajua ile nyumba sijui kwa kuwa mimi mwenyewe ni daktari lakini hatuwezi kunyanyapaa mgonjwa yule kwa sababu kwa kweli ni hali ambayo haiambukizwi kwa kushikana mkono au kwa kula naye pamoja. Naomba sana Watanzania wakubali kwamba kwa pamoja tuondokane na unyanyapaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante bwana daktari kwa semina hii. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa Richard Nyaulawa ajiandae.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa natoa rambirambi zangu kwa Wananchi wa Kiteto kwa kifo cha Mbunge wao Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali peponi. Amina!

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba nitoe hongera nydingi kwa Mheshimiwa Getrude Rwakatare na kumkaribisha Bungeni na Bunge hili atajifunza jinsi tunavyochangia sisi wazoefu na safari inayokuja nadhani na yeye attachangia, karibu sana! (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono mapema kabisa kwa kuweka sheria hii inayohusiana na masuala ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI wenyewe. Mimi nashauri kuondoa usiri kwa watu wenye Virusi vya UKIMWI au wenye kuwa na UKIMWI kwa sababu unaposema ni usiri na ambao nadhani haupo. Kwanza unafanya kuongeza unyanyapaaji zaidi, halafu unaongeza woga usiokuwa wa lazima kwa watu kuhusiana na ugonjwa wenyewe. Najua kuna magonjwa mengi mabaya ambayo yamepata kutokea na yaliyopo kama vile magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu, kifua kikuu, saratani na mengineyo, lakini yote haya yanaonekana kuwa ni wazi, lakini ni mabaya zaidi na ninavyojua ukifanya kitu kuwa siri hasa ndivyo unavyotaka kukiongezea uovu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukitazama vitabu vikuu vinavyokataza maovu kama vile Biblia na *Quran* Tukufu, ukitazama sheria zinapotungwa kukataza maovu watu ndivyo wanavyozidi kutenda makosa zaidi, hawaogopi vitabu vya Mungu wala hawaogopi sheria, wanataka kujaribu. Sasa wewe unapoweka usiri zaidi maana yake ni kwamba unataka uongeze. Na sababu zangu za msingi ni kwamba unaposema hawa watu wakapime kwa siri ni wazi wanapima kwa siri na majibu yake unampatia kwa siri lakini dawa wanapogawa hawagawi kwa siri, kwa nini nasema hivyo? Hawagawi kwa siri kwa sababu unakuta wamewatengea siku maalumu ya kwenda kuchukua dawa, chumba maalum cha kuchukua dawa kukiwa na wahudumu maalumu wa kuchukua dawa zile za kupunguza makali wanazoiita, pengine na kadi maalumu za watu hao, je, usiri uko wapi? Huko ni kuwanyanyapaa maana unawatangaza bila ridhaa yao kwa kuwawekea mipaka hiyo ya waziwazi na watu wengi wanafahamu kwamba kumbe fulani naye amekwenda kuchukua dawa kule, sasa siri iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nadhani baadhi ya vifungu vinagongana. Ukitazama vifungu vya 15, 17, 46, 47, 48 kwa njia moja au nyininge vinagongana, kwa mfano kifungu cha 15 kinasema kwamba mtu ye yeyote anayeishi Tanzania kwa hiari yake anaweza kupima Virusi vya UKIMWI, Lakini kifungu cha 15(3) kinasema mtu halazimishwi na hatalazimishwa kupima Virusi vya UKIMWI na wakati huo huo wanaposema hatalazimishwa. Ukitazama kifungu cha 15(4)(a) kinaizuia Mahakama kwamba haitaruhusiwa kumlazimisha mtu akapime Virusi vya UKIMWI. Lakini ukitazama kifungu cha 47 kinasema mtu ye yeyote anayemwambukiza Virusi vya UKIMWI

mtu mwininge anatenda kosa na akipatikana na kosa atafungwa si chini ya miaka mitano na si zaidi ya miaka 10, lakini utapata ushahidi wapi kama katika kifungu cha 15(4)(a) kinaikataza Mahakama isiweze kulazimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukitazama kuna kifungu cha 18(h) hiki kinahusiana na msamaha wa kutokuvunja sheria ya usiri. Kifungu hicho kidogo kinaruhusu katika kutekeleza amri ya Mahakama juu ya kesi inayohusiana na Virusi vya UKIMWI kwa mtu binafsi. Kinaruhusu sasa Mahakama ilazimishwe yule mtu pengine kupima ili kupatikana ushahidi. Wakati katika kifungu cha 15(4)(h) kama nilivyosema kinamkatalia, sasa vifungu hivi vinapingana, kwa hiyo, nadhani kile kifungu cha 15(4)a kifutwe na badala yake kibakie kifungu cha 18 kwa upande wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika kifungu cha 46 kosa la kutotunza siri au kutoa habari za mtu mwenye Virusi vya UKIMWI au UKIMWI, bado pia kinakuja kupingana na baadhi ya sheria. Katika kifungu cha 17 kwa mfano, usiri wa kitabibu na wale wanaotajwa kupokea majibu kwa niaba ya wahusika kwa mfano katika kile kifungu cha 16(2)(a) na (b) kimewaruhusu watu wengine kuchukua majibu ya Virusi au UKIMWI. Mfano mtoto wazazi wake wanaweza kuchukua majibu au mlezi au kwa mtu ambaye kwa njia moja au nyingine hataweza yeze mwenyewe kwenda kuchukua majibu imemruhusu anaweza kuwa mke au mume kwenda kuchukua majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika kifungu 48 wamekekewa sheria hiyo ya kuhakikisha kwamba wanatunza siri, bado unakuta inapingana na utoaji wa ushahidi wanapokuwa Mahakamani kwa sababu hakuna kifungu kilichowaruhusu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tufikirie kuna watu wapo ambao wanataka kujiambukiza Virusi vya UKIMWI kwa hiari yao, anajua kabisa yule mtu ana Virusi vya UKIMWI anasambaza UKIMWI lakini kwa sababu tu pengine atamnunulia gari *RAV 4*, tena pengine nyekundu na atampa pesa nyingi, anaamua kwenda kujiambukiza na kuna msemo umezuka Dar es Salaam, sina uhakika nao, lakini wanausema sema tu. Baadhi wanasema afadhali maisha mafupi ukiwa umeponda raha kikamilifu kuliko maisha marefu ambayo umebobea kwenye shida. Watu wa namna hii ni wazi wanaenda kujiambukiza UKIMWI kwa hiari, sheria inasemaje juu ya watu hao? Kuna kifungu chochote kitakachowekwa kuhakikisha kwamba watu wa namna hiyo nao wanashitakiwa maana mtu uki-*attempt* kujinyonga, ukikusudia kutaka kujinyonga na zoezi la kutaka kujinyonga likashindikana, wewe unakwenda kushitakiwa kwa kosa la kutaka kujiua na ukipatikana na kosa unafungwa kifungo kikubwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hawa wanaokwenda kujiambukiza wenyewe UKIMWI kifungu chao kitakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja hii lakini naomba watazame kwa makini vifungu hivyo vinavyojichanganya kisheria ili kesho na kesho kutwa wasilazimike tena kuleta marekebisho katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ahsante kwa kunipa nafasi hii.
(*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Hao wanaosema waishi muda mrefu kwa raha wamesahau UKIMWI si kama ajali ya gari, unaweza ukaumwa kwa miaka mingi uko kitandani tu, kwa hiyo, nadhani muwaambie hivyo si lazima ufe siku hiyo hiyo. Mheshimiwa Richard Nyaulawa atakuwa mzungumzaji wetu wa mwisho kufuatana na muda.

MHE. RICHARD S. NYAULAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu. Kwanza kwa niaba ya Wananchi wa Mbeya vijijini natoa pole kwa kifo cha Mbunge wa Kiteto na tuombe roho ya marehemu ilale mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili, natoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare ambaye ni jirani yangu kwa kuwa Mbunge na tutatoa ushirikiano wote unaohitajika katika kufanya naye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, natoa pongezi kwa Serikali kwa kuweza kuleta Muswada huu Bungeni kwa sababu kwa hakika pamoja na kwamba umechelewa bado ni vizuri kuwa umeletwa na ni suala la msingi, kwa msingi huo basi na mimi naunga mkono Muswada huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi na utekelezaji wa sheria hii ambaeo leo hii tunataka kuipitisha unategemea sana kiwango cha elimu ambayo inaweza kutolewa kwa wananchi. Lakini pili, inategemea sana uelewa wa kuwepo au kutokuwepo kwa Virusi vya UKIMWI kwa kila mwananchi, kwa sababu kama mwananchi hana habari kama ana Virusi vya UKIMWI au anavyo basi tabia zake huwa zinaweza kubadilika kufuatana na ufahamu huo. Kwa hiyo, suala la uelewa na elimu ni suala la msingi ili kuweza kuhakikisha kwamba kunakuwa na ufanisi wa utekelezaji wa sheria hii lakini vilevile kungekuwa na umuhimu wa juhudini za pekee katika kuhimiza watu mbalimbali kupima Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo mengi kidogo katika kazi hiyo ya kuweza kupima kwa sababu ya kuwa na uhaba wa mipango hasa kwa sehemu za vijijini pamoja na uhaba wa vituo vya kupimia ugonjwa wa UKIMWI. Lakini kwa ujumla wananchi kwa wakati huu wana ufahamu mkubwa na wengi wangetaka kupima Virusi vya UKIMWI lakini kutokana na uhaba huo hasa katika sehemu za vijijini kazi hii imekuwa ngumu na haitekelezwi sawa sawa. Kwa hiyo, katika mipango inayokuja na hasa bada ya kupitisha sheria hii maana yake labda kuwe na kiwango kikubwa cha fedha ambazo zinaweza kutengwa kwa ajili ya kutekeleza sheria hii na kuwanusuru watu kutoka kwenye vifo vya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo ningetaka kwenda kifungu hadi kifungu na kujaribu kuelezea mawazo yangu katika vifungu mbalimbali. Tukienda ukurasa wa 36, Kifungu namba 4(2) kinaelezea kuhusu umuhimu wa kuzuia unyanyapaa

kwa kuwashirikisha watu wa aina mbalimbali wakiwepo wanasiasa, viongozi wa dini na viongozi wa mila.

Ushirikishwaji huu vilevile unategemea sana kuwepo kwa elimu hasa kwa viongozi wa mila. Viongozi wa mila wanakaa vijijini na wanakaa na wananchi wengi zaidi hasa tukielewa kwamba asilimia karibu 72 ya Watanzania wanakaa vijijini. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwamba viongozi wa mila wana nafasi kubwa sana ya kuweza kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi mbalimbali. Lakini cha msingi ni kuwawezesha hawa viongozi wa mila ili waweze kufanya kazi hiyo kwa mchango uliokuwa mzuri. Pasipokuwa na uwezeshaji mzuri inawezekana kazi ya kupunguza unyanyapaa na kueneza elimu ya UKIMWI vijijini bado inaweza kuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, ni usiri wa matokeo ya kupima kutolewa kwa watu mbalimbali, kifungu namba 16(2), ukurasa wa 41 kinasema kwamba usiri wa matokeo unaweza kutolewa kwa mke au mume au mshirikia wa kimapenzi. Lakini hakijaeleza kwamba utoaji wa taarifa hii inastahili uwe umeruhuswa na mtu aliyepima na kama hajaruhusu mtu aliyepimwa maana yake ni kwamba usiri huu unakuwa haupo tena, kwa hiyo, kutakuwa na uvunjaji wa usiri kwa sababu wametoa taarifa kwa mke au mume au mshiriki wa kimapenzi bila ruhusa ya muhusika.

Kazi kubwa katika kulizuia hilo ni kwamba pale ambapo panakuwa na nia ya kutaka kupima ingekuwa ni vizuri kama kunakuwa na ushauri kwamba mume na mke wote wawili wawepo wakati wa kupima. Kwa sababu kukiwa na ushauri huo basi bila shaka wote wawili watakuwa wameshiriki na usiri hautakuwepo na kila mmoja kati ya wote wawili watakuwa na taarifa nzuri ya afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 18 ukurasa wa 41 kinaelezea usiri kwamba unaweza kuvunjwa kwa kufuata taratibu za kutoa taarifa zinazohusiana na usimamizi na ufuutiliaji wa mipango ya utekelezaji. Natumaini katika kifungu hiki taarifa ambazo zinaelezwa siyo taarifa kuhusu majina ya watu lakini ni kuhusu taarifa za takwimu na kama ni taarifa za takwimu basi sioni jinsi ambavyo usiri huo unaweza kuvunjwa, lakini kama kutakuwa na kutoa majina ya watu wanaohusika basi katika kipengele hicho maana yake ni kwamba wapimaji watakuwa wanatoa siri ya watu waliopima. Kwa hiyo, mategemeo yangu ni kwamba takwimu zinazohitajika hazitakuwa na usiri lakini majina bado yatakuwa na usiri.

Kifungu cha 21(2) ukurasa wa 42 kinaelezea kuzuia kwa Virusi vya UKIMWI ikiwa ni pamoa na kutoa taarifa kwa mshiriki wa mapenzi. Kwa maana hiyo ni kwamba kabla mtu hajafanya mapenzi ni lazima atoe taarifa kwa mshiriki mwengine ili aweze kuwa na ufahamu na kama atakubali basi akubali akiwa na ufahamu huo. Tatizo kubwa hapa ni kwamba inawezekana watu wengi wanafanya mapenzi bila kujua afya zao na hawajui kama wameambukizwa au hawajaambukizwa. Hili linakuwa ni tatizo. Ili kuweza kutekeleza hilo itakuwa ni vizuri kama watu wengi wanaweza kuhimizwa kuweza kupima Virusi vya UKIMWI. Labda kama linaweza kuwa ni kosa la jinai basi kuwe na utaratibu wa kuweza kuwajua watu ambao wanaambukiza Virusi vya UKIMWI kwa makusudi kwa sababu inawezekana kabisa kwamba bila kupima huwezi kujuwa kama una

Virusi vya UKIMWI au hapana. Kwa hiyo, kama unaambukiza inawezekana kwamba unaambukiza kwa sababu huna ufahamu wa kutosha kama unavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu 23, ukurasa wa 42 kinaelezea kwamba Wizara itakadiria wingi wa kondomu zinazohitajika nchini, kwa maneno mengine itafanya *quantification* ya kondomu ambazo zinahitajika nchini. Sina hakika na neno *quantify* ambalo lilitahili kutumika lakini nafikiri kwamba *qualify* kwa maana ya kwamba kutoa ubora wa kondomu zinazohitajika ndio suala la msingi ili kuwawezesha kuwa na kondomu ambazo zinahitajika na ambazo zinaweza kuthibitishwa na *TBS* pale ambapo zinaingia nchini.

Lakini kazi ya kuingiza kondomu iwe ni kazi ya Wizara na wadau wa aina nyingine mbalimbali kwa sababu mahitaji ya kondomu ni makubwa sana na wadau wengine wanawenza kushiriki katika kununua kondomu na kuzileta hapa nchini ilimradi tu zimekuwa na ubora ambao unahitajika. Katika nafasi hii ningetaka kutoa ponezi kubwa sana kwa watu wa *PSI* wanaofanya kazi nzuri katika kusambaza kondomu za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele namba 26(h), ukurasa wa 43 kinaelezea wafanyakazi ambao wanatoa huduma za afya ambao wanawenza kuambukizwa Virusi vya UKIMWI. Katika hili napata matatizo kwa sababu wanasesma akiambukizwa wakati wa utekelezaji wa kazi yake. Sasa mtu anapokuja kupimwa inawezekana kwamba utekelezaji ulikwishafanyika miezi au miaka kadhaa iliyopita, kuweza kujua aliambukizwa kwa sababu alikuwa akitekeleza kazi yake au alikuwa amefanya ngono zembe inakuwa vigumu. Kwa hiyo, pamoja na kwamba labda wanahitaji kupata fidia labda kungekuwa na bima ya fidia endapo watu wa namna hii wanawenza kuwa na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natumaini hapo ni wafanyakazi wote bila kutegemea kwamba waliambukizwa wakati wa kutoa huduma au wakati mwingine. Maadamu kazi yao inahusika na kazi ya kutoa huduma kwa watu waliombukizwa basi wangewekewa bima ya fidia endapo wanapata matatizo ya namna hiyo. Nategemea kwamba kunawenza kuwa na utata mkubwa sana wa kubaini aliambukizwa namna gani. Tukiweka bima, labda tatizo hilo linawenza kuepukika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele namba 33(a), ukurasa wa 44 kinaelezea kuhusu utoaji wa huduma kwa kiwango cha juu endapo fedha zitapatikana. Mimi nataka kupendeleza kwamba utoaji wa huduma za kiwango cha juu utolewa kufuatana na fedha zilizopatikana. Ukitsemwa itategemea inaleta matatizo kidogo kwa sababu unawenza kubajeti kidogo au usibajeti kabisa na huduma zisiweze kutolewa, lakini kufuatana na fedha ambazo umekwishapata na ukatoa huduma inayostahili ndio suala ambalo la msingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele namba 39, ukurasa 45, kinaelezea kuhusu Serikali za Mitaa kuweza kuwasaidia watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu katika kuwasomesha na misada ya aina nyingine. Tunaelewa wote kwamba uwezo wa Halmashauri unatofautiana, kuna nyingine kama za mijini zina hali nzuri zaidi kuliko za

vijijini na inawezekana kwamba kuna sehemu nyingine zina hali nzuri zaidi kuliko sehemu ambazo ni maskini. Kwa hiyo, napendekeza kwamba maadamu tunatambua uwepo wa watoto wanaoishi katika hali ngumu basi Serikali ingekuwa inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa watoto hao na mgawanyo wa fedha hizo utategemea na watoto waliopo katika eneo hilo. Lakini vilevile vigezo vya maendeleo ambavyo vimewekwa na TAMISEMI wakati wa kugawa hela za maendeleo. Kwa hiyo, hivyo ndivyo vingekuwa vigezo kwa ajili ya kuwasaidia watoto yatima lakini tusiliachie jukumu hilo kwa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 36(2), ukurasa 46 wajumbe wa utafiti, napendekeza kwamba pale ambapo wameandika kuwe na mjumbe kutoka Muhimbili wangesema mjumbe kutoka kwenye Hospitali ya Rufaa. Sioni sababu kwa nini Muhimbili peke yake ihusishwe wakati kuna Hospitali nyingine za Rufaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza vilevile kuwe na mjumbe kutoka kwenye Sekta Binafsi kwa sababu hawaonekani kama wanahusishwa kwa njia moja au nyingine ingawaje katika kueneza elimu imeelezwa kwamba wahusike.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni vyombo vya umma na vyombo binafsi viweke takwimu za utafiti unaendelea. Sasa katika kuweka takwimu, sina hakika vyombo binafsi ni vya aina gani, yaani chombo chochote kile au ni vyombo vya aina fulani. Kwa hiyo, kunahitaji kuwe na maelezo zaidi juu ya aina ya vyombo ambavyo vinastahili kuweka takwimu za utafiti unaendelea. Vyombo binafsi vitapataje taarifa hizo kwa sababu hawahusishwi katika tafiti hizo kwa njia moja au nyingine, hivyo inawezekana kwamba kuweka takwimu hizo inaweza kuwa ni vigumu. Kwa hiyo, kinachohitajika hapa ni kusema kutakuwa na *interface* ya aina gani kati ya Kamati ya Utafiti na vyombo binafsi ambavyo vinataka kuweka takwimu ya tafiti mbalimbali ambazo zinaendelea katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya michango yangu hii ambayo imeenda kuchambua kipengele baada ya kipengele naunga mkono kwa asilimia mia moja Muswada huu ambaeo upo mbele yetu. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema kwa mchana huu huyo ndiye msemaji wetu wa mwisho. Kwa kuwa muda hautoshi tuna nia kwamba Muswada huu uendelee jioni yote leo na pengine Waziri aweze kutoa maelezo kesho baada ya kipindi cha mswali. Lakini tutambue kwamba tutakuwa na *Supplementary Order Paper* mchana huu kwa sababu ya taarifa aliyotoa Mheshimiwa Spika kabla hajaondoka. Kwa hiyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni.

(*Saa 6.58 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi ya leo wakati wa matangazo pamoja na mambo mengine nilitoa mwongozo utakaotumika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bunge wakati wa Kikao cha Bunge cha jioni hii. Katika mwongozo huo wa Spika nilieleza kuwa imeandalisha nyongeza ya shughuli za Bunge iliyohusu hoja za Kamati, Kamati ya Kanuni za Bunge itakayotolewa na Mheshimiwa Naibu Spika. Aidha, nililieleza Bunge kuwa hoja hiyo ya Naibu Spika itafanyiwa kazi na Kikao hiki cha jioni. Kwa sababu ya maelezo yangu hayo ya asubuhi ambayo ndiyo mwongozo nilioutoa, shughuli itakayoanza hivi punde ni ile iliyoko kwenye nyongeza ya Orodha ya Shughuli za leo na baada ya hapo tutaendelea kama kawaida. Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo namwomba sasa Katibu aweze kututajia shughuli inayofuata.

HOJA ZA KAMATI TAARIFA YA KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Novemba, 2007 Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la kuridhia Kanuni mpya za Bunge, Toleo la Mwaka 2007 kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge.

Pamoja na Kamati hiyo kupitisha mapendekezo kadhaa ilijitokeza kuwa pendekoz la kuwepo na kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kuhusu shughuli za Serikali lifanyiwe kazi zaidi kabla ya kuwasilisha Bungeni kwa uamuzi. Sasa imekubalika kwamba utaratibu huo wa kuwa na kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kuhusu shughuli za Serikali uwekwe kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge. Utaratibu huo utawezesha wananchi kupata taarifa, majibu au maelezo ya Serikali kwa mambo yanayotokea kwa wakati huohuo.

Utaratibu kama huu hufanywa katika Mabunge mengi hususan yale ya nchi za Jumuiya za Madola ambayo mfumo wake unafanana kwa kiwango kikubwa na mfumo wa Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 152 (1) ya Kanuni Kudumu za Bunge toleo la 2007 inaelekeza kwamba Bunge linaweza kupitisha Azimio la kufanya mabadiliko katika Kanuni yoyote ya Bunge kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, Kamati ya Kanuni za Bunge ilikutana Dodoma tarehe 14 Novemba, 2007 kupitisha pamoja na mapendekezo mengine pendekoz la kuwa na kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu. Aidha, Kanuni ya 152(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 inatamka kwamba mapendekezo yoyote ya kufanya mabadiliko ya Kanuni za Bunge yatawasilishwa Bungeni na Naibu Spika. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hiyo nimesimama mbele yenu ili niwasilishe mapendekezo ya kufanya mabadiliko ya Kanuni za Bunge, mabadiliko yanayopendekezwa kufanywa kwenye Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kiambatanisho A cha hotuba hii kinapendekeza kufanya mabadiliko kwenye Kanuni ya 30(4) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la 2007, inayohusu mpangilio wa Shughuli za Bunge ili kuweka Shughuli mpya inayohusu

maswali kwa Waziri Mkoo mara baada ya shughuli za Hati za Kuwasilisha Bungeni na kabla ya shughuli za maswali ambayo taarifa zake zimetolewa. Vilevile Kiambatanisho hicho kinapendekeza kufanya mabadiliko kwenye Kanuni hizo za Bunge kwa kuweka Kanuni mpya ya 38 inayohusu maswali kwa Waziri Mkoo. Aidha, utaratibu na masharti kuhusu maswali kwa Waziri Mkoo umewekwa bayana na fasili za Kanuni hiyo kama inavyoonekana kwenye Kiambatanicho hicho cha A. Kiambatanisho A kinasema: “Mapendekezo ya Mabadiliko kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge” kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 152 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ya Kanuni za Bunge inapendekeza mabadiliko yafuatayo kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge:

(i) Kanuni ya 30 (4) ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza shughuli (f) ya maswali kwa Waziri Mkoo katikati ya shughuli za Hati za Kuwasilisha Bungeni na shughuli za maswali ambayo taarifa zake zimetolewa.

(ii) Iwekwe Kanuni mpya ya 38 inayosomeka kama ifuatavyo:

(1) Waziri Mkoo anaweza kuulizwa maswali na Mbunge ye yote kuhusu maswali yoyote yanayohusu shughuli za Serikali.

(2) Mbunge ye yote hataruhusiwa kumuuliza Waziri Mkoo swali la kejeli au la uzushi au la mashambulizi binafsi au litakalokiuka masharti mengine yaliyowekwa na Kanuni ya 40 ya Kanuni hizi kuhusu maswali yanayoulizwa Bungeni.

(3) Maswali atakayoulizwa Waziri Mkoo hayatakuwa na taarifa ya awali kama maswali mengine.

(4) Kipindi cha maswali kwa Waziri Mkoo kitakuwa kila siku ya Alhamisi na hakitazidi dakika 30.

(5) Iwapo siku hiyo kwa sababu maalumu Waziri Mkoo hatakuwepo Bungeni hakutakuwa maswali kwa Waziri Mkoo.

(6) Waziri Mkoo anaweza kutumia kipindi cha maswali kwa Waziri kutoa taarifa au ufanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na Shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma kwa muda usiozidi dakika 10 ikifuatiwa na maswali ya Wabunge kwa dakika 20 kuhusu taarifa yake au maswali mengine yoyote ya Serikali.

(7) Maswali kwa Waziri Mkoo yatafuatiwa na maswali mengine kwa Mawaziri kwa dakika 60 kama yatakavyokuwa yamepangwa kwenye orodha ya shughuli za siku hiyo.

Mheshimiwa Spika, faida ya mabadiliko haya yanayopendekezwa ni nyingi, hata hivyo, baadhi tu ya faida hizo ni kama ilivyoelezwa kwenye utangulizi wa hotuba yangu:

Moja, ni kwamba Serikali kupata fursa ya kutoa majibu na taarifa juu ya masuala yanayotokea wakati huu.

Pili, kutoa fursa kwa Wabunge kumuuliza Waziri Mkuu maswali yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Serikali hususan yanayovutia hisia za wananchi. Serikali itapata fursa ya kuwa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge watapokea na kwa kauli moja watapitisha Azimio la kuridhia mabadiliko ya Kanuni za Bunge nitakalowasilisha yaani Azimio la kufanya Mabadiliko katika Kanuni za Bunge.

KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 115 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, ikisomwa pamoja na kifungu cha 4 (3)(a) cha Nyongeza ya Sita ya Kanuni hizo, moja ya majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge ni kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kufanya mabadiliko kwenye Kanuni za Bunge;

NA KWA KUWA, Kamati ya Kudumu ya Bunge ilikutana Dodoma tarehe 14 Novemba, 2007 kujadili mapendekezo ya mabadiliko ya Kanuni za Bunge na kwa kauli moja kupitisha mapendekezo ya marekebisho hayo;

KWA HIYO BASI, kwa mujibu wa Kanuni 152 (1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linalokutana katika Mkutano wa Kumi linayapokea na kuyakubali kwa kauli moja mapendekezo ya mabadiliko katika Kanuni za Bunge kama yalivyowasilishwa kwenye Kiambatanisho cha A cha Hotuba ya Naibu Spika iliyowasilishwa Bungeni leo tarehe 31 Januari, 2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofī*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Hapo mwisho nilikusikia ingawa umenong'ona tu kwamba umetoa hoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walismama kuiunga mkono, kwa hiyo, hoja imetolwa na imeungwa mkono. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba muiamue.

Mheshimiwa Kaboyonga karibu!

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sijui nitatumia Kanuni gani kuwasilisha hoja ninayotaka kuwakilisha. Kabla hatujatoa ufumbuzi napendekeza utoe ruhusa tujadili hoja iliyo mbele yetu halafu ndiyo tutoe uamuzi.

SPIKA: Inaelekea Waheshimiwa Wabunge mmeanza kuzisahau Kanuni, Spika akisimama akisema kwamba naomba muiamue na akiketi maana yake sasa msimame wale mnaotaka kuchangia ili awaone na kuwapa idhini ya kuchangia.

Baadaye sasa yaani baada ya mjadala nitamwita Mto hoja atajibu yale ambayo yatakuwa yamejitokeza na kama kawaida sasa baada ya hapo ndiyo nitawahoji, hapo ndiyo itakuwa “Ndiyo” au “Siyo”. Kwa hiyo, kama ilikuwa ni kusudio lako kuchangia hujakosea kabisa Mheshimiwa Kaboyonga unaweza kuendelea na wengine watakaoweza kuchangia basi mlango uko wazi.

Namwona Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, kwanza pongezi sana kwa kufanikiwa tarbushi, sasa inaruhusiwa, kwa hiyo, na kwa wale Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wananiuliza tarbushi ni nini basi ni hiyo kofia aliyoivaa Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, karibu!

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja iliyombele yetu.

Nianze kwa kumpongeza Naibu Spika kwa kuileta hoja hii nzuri na inaonyesha mapinduzi ya mwelekeo wa shughuli zetu hapa Bungeni. Naiafiki hoja hii ilimradi tu kama pendekezo langu kwenye kifungu cha 4 kuhusu muda wa maswali kwa Waziri Mkuu kitaongezwa kutoka dakika 30 mpaka saa moja kwa sababu dakika 30 hatuwezi kupata maswali na majibu ya kutosha kwa mujibu wa matatizo yanayotukabili nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza tu kwamba tuongeze muda kutoka dakika 30 mpaka saa moja. Vinginevyo naiafiki hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Zitto Kabwe, karibu!

MHE. KABWE ZUBERI ZITTO: Mheshimiwa Spika, na mimi napenda nikushukuru kwa kuniruhusu kuchangia mjadala huu, lakini kwa bahati mbaya sana wakati wa mjadala wa mabadiliko ya Kanuni za Bunge sikuwepo lakini nimeona ni bora nichukue fursa hii na mimi niweze kuchangia katika suala hili la maswali kwa Waziri Mkuu.

Lakini pia niweze kutoa pongezi za dhati kabisa kwa mabadiliko haya ambayo yanafanywa katika Kanuni zetu za Bunge hasa kwa kuzingatia kwamba mabadiliko haya ni ya ndani (*internally driving*), hayajatokana na shinikizo la wafadhili au la watu wowote wa nje, ni mchakato ambao umechukua muda mrefu, Kamati iliundwa na kuweka mapendekezo kama yalivyo.

Kwa hiyo, hii kwa kweli inaongeza nguvu katika juhudhi zetu za kupanua demokrasia ya nchi yetu na napenda kwa dhati kabisa niwapongeze Wabunge wote ambao mlisiriki katika kuitisha mabadiliko ya Kanuni kwa ujumla wake, Kanuni ambazo tunatumia hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nikirudi kwenye hoja yenyewe ya maswali kwa Waziri Mkuu napenda nilipongeze Bunge na Serikali kwa kukubaliana na suala hili kwa sababu ni suala ambalo lilikuwepo na lilikuwa lipite kwenye Kanuni za awali.

Lakini mijadala kati ya Bunge na Tawi la Utendaji ilikuwa bado inaendelea na leo asubuhi ilikuwa imetutaarifu kwamba muafaka umefikiwa na suala hili limekubaliwa na hivyo Bunge kuombwa kuweza kufanya mabadiliko ya Kanuni ambazo tunaaza kuzitumia hivi sasa.

Mimi napenda kuungana na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga kwamba muda wa maswali kwa Waziri Mkuu uwe ni muda wa saa moja. Na nyongeza katika kumuunga mkono Mheshimiwa Kaboyonga ni kwamba hatutakuwa na ubaya wowote kama katika wiki ambayo Bunge linakaa siku moja ikawa kipindi kile cha maswali ni maswali ya Waziri Mkuu tu kwa sababu ukichanganya maswali ya Waziri Mkuu na maswali kwa Wizara nyagine siku hiyo hiyo, unaondoa ule utamu wa siku yenyewe.

Ni vizuri kipindi cha maswali siku ya Alhamisi kiwe *dedicated* 100% kwa maswali ya Waziri Mkuu na kiwe ni kipindi cha saa moja na baada ya hapo shughuli nyingine za Bunge ziweze kuendelea. Hiyo kwanza itatoa fursa kwa Wabunge wengi zaidi kuweza kuuliza lakini pia itampa nafasi anayeulizwa maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu kupata muda wa kufafanua zaidi kwa sababu Serikali kwa vyovypote vile lazima ina maelezo mengi kuliko Wabunge kwa sababu yenyewe ndiyo inayotunga sera, inatekeleza sheria na kadhalika.

Kwa hiyo, nadhani kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuongeza muda wa maswali na majibu kwa Waziri Mkuu katika siku hiyo na ufikie saa moja kama Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga alivyopendekeza. Naamimi kabisa siku za Alhamisi asubuhi zitakuwa ni siku maarufu sana katika siasa za Tanzania kwa sababu ndiyo kipindi ambacho ule uhalisia kati ya Tawi la Utendaji na Tawi la Uwakilishi unakuwepo.

Kwa sababu kama unavyofahamu maswali ya papo kwa papo ni maswali ambayo yanaleta *debate* sana na ni maswali ambayo kwa kweli yanababisha vichwa vichemke, bongo zichemke na hiyo inasaidia sana. Na hata itawafanya wananchi waone raha kuliangalia Bunge na kulifutilia na vilevile Wabunge nao kuijandaa vya kutosha, Serikali nayo kuijandaa vya kutosha kwa sababu Waziri Mkuu hatakuwa anajibu yeye peke yake, kwa vyovypote vile ni lazima Mawaziri watakuwa wanamsaidia kuweza kumpatia maelezo yanayohusiana na Wizara zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kuunga mkono hoja iliyoletwa na Naibu Spika kwa dhati kabisa na kuwapongeza wale wote waliofikisha mchakato huu hapo ulipofikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nataka kutoa ufanuzi kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, hakuna Waziri mwingine ye yote anayeruhusiwa kujibu, muelewe hiyo na hicho ni kipindi chake tu ndiyo makusudi ya hili. (*Makofi*)

Pili, kipindi cha dakika 30 si kidogo maana yake mtaona kwamba hapa kwenye kiti tutakuwa tunawasahihisha sana kwa sababu kama mambo ya Sekta ya kawaida, Barabara za kutoka sehemu moja kwenda nyingine hayo siyo maswali yenyewe hayo. Kwa hiyo, na mimi nashauri tukae kwenye dakika 30 isaidie ili tujifunze. (*Makofi*)

Mheshimiwa William H. Shellukindo, karibu!

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kidogo.

Kwanza napenda kumshukuru sana Naibu Spika, kwa kuleta Azimio hili kwenye Bunge lako Tukufu. Mimi napenda kusema kwamba nadhani Tanzania tubaki kwenye nafasi yetu ya kuleta mabadiliko katika mifumo.

Kwa mfumo huo wa Bunge amba tulikuwa nao muda mrefu kwa kweli umetumika sehemu nyingine lakini inaonekana sasa kama tulikuwa tumedumaa, tumekaa pale pale, watu wengi wanataka kujua Tanzania mmebadili nini na katika hili kuna nini. Nina hakika kwamba kuna wengine amba hawana mabadiliko haya katika mfumo wa Shughuli za Bunge kwa maana ya kuimarisha demokrasia basi watafuata hii.

Kwa hiyo, haya ni mabadiliko mazuri tena ya kimapinduzi na tuisiyaogope, kitu chochote kile kwa kweli kina faida yake na hiki kina faida nzuri sana badala ya kuongojea mpaka uandike swali kwa kitu ambacho kimetokea leo inakuwa kidogo ni taabu. Waheshimiwa Wabunge, nafasi hii tuitumie vizuri mambo ya leo yaweze kupata maelezo ya Waziri Mkuu.

Mimi sina la kuongeza zaidi isipokuwa napenda kuunga mkono hili Azimio na kwamba tuweke Kanuni mpya ya 38 kwa ajili ya kuhalalisha hoja yetu hii. Naunga mkono na nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir!

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, na mimi nitamke moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja hii lakini pia niseme kwamba niunge mkono maelezo au matakwa ya Mheshimiwa Kaboyonga pale aliposema kwamba tuongeze dakika badala ya nusu saa iwe saa moja.

Lakini wakati huohuo tukiangalia kifungu cha sita kwenye ukurasa wa pili ambapo huku ndiyo inazungumzwa hiyo nusu saa, ukikisoma kifungu hicho cha sita kwa

kweli hiyo nusu saa yenyewe haipatikani kwa sababu hapa imetamkwa wazi kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa na dakika kumi na sisi Waheshimiwa Wabunge tutakuwa na dakika ishirini. Sasa hii nusu saa sijui hata ilikuwa ni nani, ni ya Mheshimiwa Waziri Mkuu peke yake au yetu sisi Wabunge peke yetu?

Hapo ndipo pamenipelekea niunge mkono matakwa ya Mheshimiwa Kaboyonga kwamba bora tuongeze muda ili basi tuongelee vizuri yale mambo ambayo tunataka tuyazungumze kwa siku hiyo ya Alhamisi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ningepata maelezo baadaye katika kifungu namba 38, maswali ya Waziri Mkuu, Kanuni mpya ya 40 inazungumzia namna ya kuuliza maswali. Sasa masharti mengine yaliyokuwepo katika Kanuni hiyo yanajieleza yenyewe kwa sisi Wabunge.

Lakini kwenye hoja hii iliyoletwa sasa hivi kuna nyongeza hapa Mheshimiwa Spika amezungumza kuhusu kumuuliza Waziri Mkuu maswali ya kejeli, uzushi au mashambulizi binafsi. Haya hayapo kwenye Kanuni ya 40, kwenye kifungu chake hayapo na hii ni nyongeza ambayo imekuja, sasa kwamba tusiulize maswali ya aina hii.

Hivi huku mwisho katika Kanuni baadaye naomba nielezwe kwamba kuna chochote ambacho kinambana Mbunge ambaye atakuwa anaogelea kwenye ukejeli, uzushi au maswali binafsi? Au mimi nikisimama Waziri jana tumepapurana njiani huko nakuja hapa siku ya Alhamisi namgonga maswali yangu ninayoyataka halafu naambiwa hili ni la uzushi iwe imekwisha? Tunaliangalia vipi hili kwa sababu mmetuonya tusilet kejeli, uzushi au mambo ya binafsi, kuna nini baadaye kwa mimi Mbunge ambaye nitaingia katika hali kama hiyo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, ila uliyoisoma najua mtoa hoja atajibu lakini ile uliyoisoma atakayotumia dakika 10 siyo kila siku ya Alhamisi ni siku ambayo kuna jambo muhimu tu ambalo anataka kutueleza. Tunaendelea! Na sasa namwita Mheshimiwa Nimrod E. Mkono atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niongelee kidogo kuhusu Kanuni ya 38, kwanza imechelewa lakini pamoja na kuchelewa kuletwa kwetu nadhani ni wakati muafaka kusema.

Mheshimiwa Spika, na mimi nilikuwa mmojawapo wa wale waliokuwa wakishughulika na hizi Kanuni na tuliyahi kutembelea sehemu nyingi sana ikiwemo India, Mauritius na Uganda pia Kenya na sehemu nyingine. Ninavyoilewa ni kwamba Kanuni hii inatumika sana kwa kuwapa Wapinzani nafasi ya kuhoji Serikali, wao ndiyo hawapati nafasi kuongeza ama kukaa na Waziri Mkuu. Lakini upande wa Wabunge wale

ambao wako kwenye Chama kinachotawala huwa wakati mwangi sana na Waziri Mkuu kwenye vikao vyao, kwa hiyo, tunayo nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu chochote *on topical issues*.

Upande wa Upinzani ambao wao ndiyo wanakuwa na hamu ya kuweza kuuliza Serikali ndiyo wangepewa nafasi kuu ya kuuliza, hivyo ndivyo nilivyoelewa mimi. Kama hiyo ndiyo nia ya Kanuni ya 38 naunga mkono kabisa, lakini kama ni nia ya kuongezea Wajumbe ambao wanatoka kwenye Serikali au kwenye Chama tawala sioni kama kweli dakika 30 zingetosha.

La pili, ni kwamba *topical issue* ni nini? Naona ni masuala ambayo yanahusu utendaji wa kazi wa Serikali, je, yanahusu Tanzania tu ama yanakwenda nje ya mipaka ya Tanzania ? Maana utendaji wa Serikali unavuka mipaka ya nchi.

Kwa mfano leo hii kuna jambo kubwa linatokea Kenya, huko sasa Serikali inatenda kazi ama hapana, pengine kama inatenda kazi ni kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa, vinginevyo itakuwa siyo jambo ambalo linahusu Tanzania pekee.

Mheshimiwa Spika, lakini siku hizi ulimwengu umekuwa mdogo sana kwenye kiganja chetu, nadhani nafasi hii tungeichukua ku – *test* kama Waziri Mkuu wetu yuko *well informed* na mambo ya *global issues* au asiwe anasoma magazeti haya kwamba leo Zitto Kabwe kafanya nini kama ufisadi hivi, tunataka tuone kama kweli Waziri Mkuu anajua yanayotokea ndani ya nchi na nje ya nchi maana ni *global village*.

Kama ndivyo hivyo ningedhani *topical issue* tuweze kuipanua kidogo pamoja na maneno machache tumesema hivyo mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa George B. Simbachawene na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe ajiandae.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu, ambayo inaongeza Kanuni moja itakayokuwa namba 38 katika kanuni zetu mpya za Bunge. Kanuni hii hasa kwa wakati huu ina ulazima mkubwa wa kuwepo katika kanuni zetu. Ninapenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa kukubal. Kanuni hii inajadiliwa hapa ili tuweze kuipitisha na ninaamini tutaitipitisha.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu wa kumhoji Waziri Mkuu maswali mbalimbali yanayoihusu Serikali, kama ulivyosema, nia yake hasa ni kutaka kupata majibu ya Serikali ya papo kwa papo, kwa shida na matatizo ya wakati huo huo na ndiyo maana ya neno lilitotumika pale, yaani *topical issues*. *Topical issues* kwa mazingira ya nchi yetu ni nyingi, kwa sababu hatuna mipango mingi madhubuti na ya muda mrefu katika mambo yetu mbalimbali ya maendeleo. Ninaungana na wenzangu ambao wamesema kwamba,

kile kipengele cha nne, pamoja na kwamba mtoa hoja amesema dakika thelathini zimetosha, lakini ninaona haki yangu ya kutoa mawazo yangu inabakia pale pale kwamba, kweli muda huu ni mdogo, tunahitaji uwe saa moja, kwa sababu mambo ya kuuliza yanayotokea papo kwa papo yapo mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninasema hivyo? Nichukulie alivyosema mzungumzaji aliyeppita, Mheshimiwa Nimrod Mkono na ninadhani kwa tafsiri ya kifungu hiki, isiwe na madhumuni ya kutoa fursa kwa upande wa Upinzani, kumhoji Waziri Mkuu peke yake kwa mambo yao. Mimi ninadhani hata sisi Wabunge wa Chama Tawala, hatuna mfumo rasmi wa kumhoji Waziri Mkuu na kama ni suala la kuongea kwenye *party caucus* ni masuala yanayohusiana na maslahi ya chama. Kwa hiyo, hapa ndipo tunapopata fursa na sisi ya kuweza kumwuliza Waziri Mkuu, masuala yanayohusu njaa, watu wanakufa Kibakwe au watu wamepata matatizo ya ugonjwa. Ninafikiri sote tupo sawa katika hilo. Sidhani kama Wapinzani tu ndiyo watapata fursa hii wakaitumia peke yao kwenye utaratibu rasmi kama huu na ikawa imetenda *justice* kwa mabadiliko ya sasa. Ninafikiri kama ni mfumo tunauiga basi tunaweza kuiga vitu vingine na vingine si lazima tukaiga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudie kupongeza kukubaliwa na kuletwala kwa kanuni hii, maana Mbunge mmoja ni *institution*, anapo-move hivi ana-move na wapiga kura wake wenye matatizo mbalimbali. Tunapokuwa tuna mambo ya papo kwa papo tunapigwa simu, utakuta simu za Wabunge zipo *busy*, unaambiwa kuna hili na hili linahitaji jibu, *then* unapata nafasi kila wiki unauliza papo kwa papo unajibiwa na wewe unaelekeza, ninadhani tutaisadia Serikali na itapata ufanisi mzuri sana katika kazi zake. Kwa hiyo, ninasema kuliko ilivyokuwa nyuma kwamba, unamfuata Waziri umwambie kwa kumnong'oneza katika utaratibu ambao siyo rasmi, unajua si wote wenye uwezo wa kuweza kumfuata fuata mtu katika mfumo usio rasmi, tunafanya kazi ya Kikatiba hapa, kwa hiyo, hatuwezi kufuatana fuatana tu, tuwe na utaratibu rasmi ambao utatufanya tupate fursa ya kuisaidia Serikali, kuipa habari na Serikali itoe majibu kwa mambo ambayo yanahuksika.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono moja kwa moja kipengele hiki kiongezwe lakini muda uongezwe ili uwe saa moja. Asante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Wakati tunaendelea, ninao wajibu wa kukiongoza kikao hiki ili tufikie pazuri. Mifano ambayo ameitoa Mheshimiwa George Simbachawene, ndiyo hiyo ambayo siwezi kuiruhusu. Kwa hiyo, tuelewe hii maana yake nini, kumetokea nini Jimboni jana, Katibu Tarafa kaibiwa pikipiki; huwezi kumwuliza Waziri Mkuu, mambo hayo kwa sababu itakuwa ni *misuse* ya muda huu. (*Kicheko/Makofi*)

Muda huu ni wa masuala mazito ya nchi, kumetokea jambo kubwa ndani ya nchi halieleweki, pamoja na masuala mengine ambayo mmekuwa mkihangwa nayo katika siku hizi za karibuni. Kama kuna gazeti limeandika jambo zito sana, mpakani kumetokea nini, kuna hivi na hivi, hayo ndiyo mambo, lakini ukitaka kila mara, italeta tabu tu kwa sababu mtaona *Presiding Officers* wabaya, lakini kama mnauliza juzi kijijini wamedhulumiana wakati wa kugawa chakula cha njaa, haiwezekani! *Anyway*

tunaendelea, ninaomba nimwite Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, wakati huo huo ajiandae Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia. Nianze kwa kukupongeza wewe binafsi na vilevile Mheshimiwa Naibu Spika na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, kwa muafaka mliofikia kuhusu kanuni hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa maswali tulionao sasa hivi, kama alivyosisitiza Mheshimiwa Shellukindo ni mfumo wa kurithi. Tumerithi mfumo wa kuuliza maswali viporo na kupewa majibu yaliyochacha na leo tunaweka historia kwa mapendekezo mazuri kabisa ya kuboresha utaratibu tulionao na ninadhani hii sasa itaboresha zaidi utendaji kazi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema neno moja tu kusisitiza kwamba, mabadiliko haya yanashahisha udhaifu tuliokuwa nao katika kutafsiri Katiba yetu ya nchi. Leo hii katika Bunge letu, tunakaa na mtu muhimu sana humu ndani, tunashirikiana naye kila siku, Ibara ya 52 inasema: "Waziri Mkuu ndiye mtu mwenye madaraka ya juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hadi siku hata siku ya kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano." Sasa tuko naye hapa lakini hatumtumii vizuri. (*Makofi*)

Vilevile Ibara ya 63 inasema: "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge, Bunge linaweza kumwuliza Waziri yejote, swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yamo katika wajibu wake." Sasa hapa ni Waziri lakini sasa tunapandisha kabisa hadhi tunamwuliza Waziri Mkuu. Ninafikiri hili ni wazo zuri na tunaliunga mkono sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba niseme la mwisho kwamba, wenzetu tuliowatembelea tukiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono, pamoja na wenzetu wengine kwenye Kamati Ndogo ya Kanuni, wenzetu kipindi hiki wanakiita *question hour*, sisi tulikarabati tu kwamba iwe nusu saa, lakini *normally* wenzetu ni *question hour* na si vibaya tukaigeuza kuwa *question hour*, ikawa saa moja kwa sababu kwanza ni mara moja tu kwa wiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN): Mheshimiwa Spika, nami ninashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Kwanza, ninakupongeza sana wewe binafsi, Naibu Spika na Kamati ya Kanuni, ambapo nami bahati nzuri nilikuwa Mjumbe wa Kamati hiyo, kwa kuweza kuleta hoja hii ya kuweza kuwa na utaratibu wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mzuri kama tutautekeleza vizuri kama inavyokusudiwa. Mimi niseme tu pamoja na

kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni ni vizuri wananchi wakaelewa kwamba, bado kuna Mheshimiwa Rais ambaye ndiye mwenye kauli ya mwisho, kwa sababu pamoja na kwamba sisi Tanzania tuna Waziri Mkuu lakini tuna *Executive President*. Kwa hiyo, katika utaratibu huu wa maswali ni vizuri basi wakaelewa kuna yale maswali ambayo hataweza kuyajibu papo kwa papo kama tulivyokusudia, yatahitaji *consultation*.

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme kwamba, kama ulivyokwishatoa angalizo, utaratibu huu ni mzuri na ni wa maswali ambayo yatakuwa kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla. Maswali ambayo yanalenga mambo ya Jimbo na maswali mengine, bado yataendelea katika utaratibu mzima wa maswali ambayo Mawaziri wanayafanyia kazi na maswali ambayo baada ya kufanyiwa kazi, majibu yale yanatoka yanakuwa ni ya uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, kwa kuunga mkono hoja hii, sisi Bunge letu tunakutana kwa muda mfupi kushinda Mabunge mengine. Vipindi vine tunavyokutana katika mwaka ni muda mfupi, lakini pia tuna Wabunge wengi, Wabunge 324. Kwa wingi huo, nafasi ambayo Waheshimiwa Wabunge wanapata kuweza kuuliza maswali ambayo yanahusu Majimbo yao ni muhimu sana na ni vizuri basi tukaona kwamba, hatutaweza kupunguza muda wowote kwa ajili ya faida ya wananchi amba kero nyingi kama mtakumbuka, zinahusu Majimbo yao. Kwa hiyo, ninavyoona kwa kuanzia, tuanze kwa hicho kipindi cha nusu saa kama tulivyopanga ili tuweke nafasi kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge, kuuliza masuala mengine ambayo yatakuwa yanakwenda katika masuala ya Majimbo, ambayo kuititia huko tutapata majibu yatakayokuwa yamefanyiwa kazi kwa muda mrefu na yakapatiwa ufumbuzi.

Tukitegemea kutumia nafasi hii ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, maswali ya papo kwa papo na akatupa majibu, tutakuwa hatujawatendea haki kwa sababu kuititia pale atasema basi ninahitaji kupata nafasi zaidi nipate ufumbuzi. Kwa hiyo, bado utasikika kweli umeuliza swalii, lakini lile jibu utakalopata linawezekana lisiwe na manufaa kwa wananchi amba watakuwa wanategemea kupata jibu lililokuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu wote waliotangulia kuunga mkono hoja na ninasema kwamba, kutoptana na kanuni na vipengele vilivyowekwa vyta kuweza kuhakikisha kwamba kanuni hii tunaitumia vizuri, ninaunga mkono hoja na ninasema kwamba ni utaratibu mzuri. Asante sana. (*Makofii*)

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Hoja iliyioletwa na Naibu Spika ni hoja muhimu sana. Mimi nusu ya maswali yangu na mtazamo wangu alijibu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, lakini hata hivyo hiyo nusu iliyobakia ninaomba niulize. Katika maelekezo ya Naibu Spika, alisema maswali yasiwe ya kejeli, sasa nini kinacho-*determine* kwamba, hii ni kejeli na hili ni swalii *genuine?* Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, halafu akaendelea kueleza kwamba, yasiwe maswali ya barabara; maswali ya barabara ni sehemu ya Serikali. Nitatoa mfano mmoja, kuna

barabara moja ilianza kujengwa toka binti yangu akiwa mjamzito, mtoto wake ameshazaliwa na ameanza *nursery school* ile barabara haijamalizika, mpaka *the comedy* wakaja wakaiombea ile barabara. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaona hili ni swali la Serikali, maana yake *contract* hatujui imesemaje, kwa hiyo lazima tuulize swali kama hili. Halafu sisi wengine wa upande wako wa kushoto tunapenda kuuliza ukweli, tunapenda *ku-call a spade a spade*, je, maswali yetu hayataonekana kama ni ya kejeli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, Waziri Mkuu ni Waziri Mkuu wa Tanzania, Tanzania maana yake ni *Mainland* na Visiwani; je, tutakuwa na nafasi ya kuuliza maswali yanayohusu Visiwani? Asante sana. (*Makofi*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, samahani kidogo kwa kuchelewa. Nami ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuongeza japo ninadhani sikustahili sana kwa sababu nilikuwa kwenye Kamati Ndogo ambayo ilizunguka nchi zote hizo. Ninadhani pia utakumbuka nilikuwa nimesimama kidete sana katika suala hili kwa sababu nilijua umuhimu wake. Ninaheshimu yote yaliyosemwa na wenzangu, niseme tu pia ninaungana mkono na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kwenye kile kipengele cha pili, kwa sababu kwenye kanuni za kawaida, iko pale ni marufuku Mbunge kusema uwongo, kejeli *and so forth*.

Kwa hiyo, ninaona hapa haikuwa na haja, yaani kama *repeation* kwa sababu inaweza kuingia kwenye kanuni. Niseme tu kwamba, ndugu zangu msiwe na hofu, jambo jipyä daima linatia wasiwasí, ninaomba msiwe na hofu, tunaumiza vichwa tutaulizaje, tutafanyaje, msiwe na hofu.

Mheshimiwa Spika, umetoa mwongozo hapa wa aina ya maswali, mimi ninaheshimu kabisa mawazo yako lakini ninaomba niseme tu maoni yangu mimi. Ninakumbuka tulivyokuwa kwenye Bunge la Uingereza, Mheshimiwa Blair kwa wakati ule alikuwa anaulizwa maswali mengine ya ajabu, kila swali lina jibu lake. Swali la kejeli lina jibu lake la kejeli, suala la uzushi lina jibu lake kwa sababu nitoe mfano, hapa sisi sote ni Wabunge, tumekuja kuwawakilisha wananchi, mtu akitaka kupoteza muda ambaó umewekwa kwa heshima kiasi hicho kwa ajili ya kupata majibu ya maswali ambayo wananchi yanawaongoza kwa wakati ule, sidhani kama kuna hata mmoja humu ndani mwenye azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninasema kwamba, kuna mtu anaweza kuja kwa swali, siyo ukweli lakini ninasema maana yake siamini mtu anaweza kusimama akasema Mheshimiwa Waziri Mkuu, timesoma kwenye magazeti unahusika na suala la *Richmond*; je, ni kweli? Anasimama anasema, Mheshimiwa Mbunge, nchi hii inaongozwa na utaratibu, kama ulivysikia na mimi nimesikia, tusubiri ambavyo itaelezwa anakaa chini. Anasimama mwininge anauliza swali, timesikia kuna upasuaji tata umetokea, Mheshimiwa Waziri Mkuu utatueleza nini kwa hilo? Maana yake hapa hapatakiwi takwimu wala *reference* ni maswali ya hapo kwa hapo ambayo yanazungumzwa hasa ambayo ni *burning issues* kwa wananchi na sisi wenyewe. Sasa

badala ya kukaa yanajenga *rumours* mpaka yanabadilika anaulizwa, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuwa na majibu kwa kila swali na siyo lazima aeletee kwa muda mrefu, no. In particular, tukiongelea Waziri Mkuu wa sasa hivi ana uwezo huo, swali, jibu, swali, jibu, unauliza swali la kijinga, unapewa jibu linalofanana na swali lenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nami niunge mkono, ninaomba niseme kwamba, badala ya saa moja tufanye dakika arobaini na tano, kama tulivyopendekeza awali ila kama Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuja na hoja yake, basi juu ya zile dakika arobaini na tano, ziongezwe hizo dakika kumi na tano pale anapokuja na hoja yake yeye ambayo inabidi aiseme halafu tuichangie, lakini kama hana ni maswali ya papo kwa papo, basi iwe dakika arobaini na tano.

Mheshimiwa Spika, asante sana. (Makofi)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia angalau machache, maana mengi tayari yamezungumzwa, lakini kabla sijasahau ninapenda niseme kwamba, ninaunga mkono azimio hili mia kwa mia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninataka niwashukuru wale wajumbe ambao wameibua hoja hii na kuileta hapa. Hili ni wazo geni lakini ni zuri. Vilevile ninataka nikushukuru kwa kukubali hili wazo liingie katika kanuni, kwa sababu mengi yanakuja hapa lakini mengine hayakubaliki. Kwa hiyo, ninakushukuru kwa kulikubali hili.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limejitokeza katika mjadala wetu mpaka sasa hivi na ambalo ninalunga mkono ni kwamba, muda hautoshi kwa sababu kama tunavyoju, Waziri Mkuu wetu ni makini na mahiri sana na hatapenda kujibu swali kwa kifupi bila kuelewesha vizuri, ikafahamika. Kwa hiyo, muda wa nusu saa ni mdogo, kama haiwezekani kwa saa moja, basi angalau dakika arobaini na tano kwa kuanzia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, katika kifungu cha 38 ambacho mtoa mada Mheshimiwa Naibu Spika, amekuwa akikieleza sehemu ya tano inasema: "Iwapo siku hiyo kwa sababu maalum, Waziri Mkuu hatokuwepo Bungeni hakutokuwa na maswali kwa Waziri Mkuu." Ni dhahiri kwa sababu hayupo na maswali hayapo, lakini ninasema Waziri Mkuu ana ofisi, kuna Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, ambaye ninafikiri ana uwezo wa kujibu maswali kwa sababu ni ofisi moja. Kwa hiyo, wazo langu ni kwamba, ikiwa Waziri Mkuu kwa sababu moja au nyingine hayupo, anaweza kuwa hayupo mara moja, mbili au tatu, kwa hiyo ule uhondo ambao wananchi wamekuwa wakiupata kwa kuangalia TV na kusikiliza itakuwa wanaukosa. Sasa ili wasiukose, kama haiwezekani kuwa msaidizi wake katika Wizara hiyo kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, basi itafutwe siku nyingine kufidia ili katika wiki lazima ipatikane siku moja ya kuulizwa maswali Waziri Mkuu. Ninaamini kwamba, maswali yote yatakuwa ni mazuri, ya kumjenga Waziri Mkuu na wananchi watafaidika sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, labda niulize utaratibu, kwa sababu kila mtu ana hamu ya kuuliza, tutatumia utaratibu gani ili angalau Wabunge wengi wapate nafasi ya kuuliza?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo katika hoja hii iliyo mbele yetu na niseme tu kwamba, nilipata fursa na bahati ya kuongoza ile timu ambayo ilikuwa ni Kamati ya Mheshimiwa Spika ya kuzunguka kwenye Mabunge ya wenzetu, kupata uzoefu wa nini kinafanyika. Katika uzoefu tulioupata, mmojawapo ni huu ambao tunaujadili, kwa hiyo, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tulilikuta kwa mfano, kwa jirani zetu Zambia, ambapo pale wao Makamu wa Rais ndiye anayejibu maswali. Nafasi ile sio ya Upinzani peke yake ni ya Wabunge wote kupata fursa ya kuweza kupata baadhi ya majibu muhimu ya mambo ya sasa. Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu mengi kwa mfano, yatakayojibwa kesho tarehe 1 Februari yalipelekwa rasmi Serikalini mwezi Novemba, 2007, ndiyo yatapata nafasi Februari, 2008 au mengine Aprili, 2008. Kwa mfano, sasa hivi mtu anataka kuuliza kinachoendelea Kenya, nchi jirani ambayo ni muhimu katika *region* yetu, utauliza wapi, huna nafasi, labda uvamie swalii la nyongeza mahali upenyepenye, ulazimishe hivi. Kwa hiyo, inakuwa ni vigumu sana kwa Wabunge au Wananchi, kuweza kupata majibu halisi kwa mambo yanayotokea wakati huo ambayo ni muhimu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli muda wa nusu saa ni mdogo na mimi ningueunga mkono kwamba lingetazamwa na wenzetu wanaita *Question Minister's Hour*, ninadhani saa moja inaweza kuwa inatosha zaidi, lakini cha kusisitiza hapa ni kwamba, kwa wenzetu tulichokiona ni maswali na majibu. Sisi kwa uzoefu wetu hapa, tumezoea kuwa na ngonjera nyingi kabla ya swalii. Kwa hiyo, hii nusu saa kama kweli itapita, inalenga kwamba linaulizwa swalii na linatoka jibu. Tulichokiona huko kama alivyosema Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ukiuliza swalii la kejeli utajibiwa kejeli pale pale kwa sentensi moja na sentensi moja utapata majibu yako, unakaa chini. Kwa mfano, kule Uingereza mtu anamwuliza Waziri Mkuu, hivi wiki hii ratiba yako inasemaje? Sasa ni swalii ambalo si muhimu sana. Anapata majibu yanayofanana na swalii la namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema katika kuunga mkono jambo hili, ni kwamba, kila Alhamisi asubuhi, litawapa fursa hii Watanzania wengi zaidi wataliangalia Bunge na Serikali itapata fursa ya kipekee ya kuweza kufafanua mambo mengi muhimu kwa nchi yetu na itaifanya kuwa siku ya kipekee kabisa katika ratiba nzima ya Bunge letu. Endapo Mheshimiwa Waziri Mkuu hatakuwepo, haiwezekani mtu mwingine kuchukua nafasi hii kwa sababu ni kipindi kwa Waziri Mkuu na itakuwa hivyo kama ilivyokuwa imelengwa, kwa hiyo si rahisi tena kuweka suala lingine. Nafasi hii ni

ya kipekee Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu mwenye nafasi ya kipekee kabisa katika Bunge letu na ndiye anayesimamia masuala yote ya Serikali katika Bunge letu. Kwa hiyo ni fursa ambayo ni vizuri tukaipokea, nina hakika wapo Wabunge ambaao wamekaa miaka thelathini, wengine ishirini, halijawahi kujibowi swali lao hata moja na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo ni fursa ambayo inapaswa tuipokee na tuitumie vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, asante sana. Awali ya yote, nami ninataka kukupongea wewe, pamoja na Kamati ya Bunge ya Kanuni, kwa kupata uwezo wa kuleta marekebisho haya kwenye Bunge letu Tukufu, hongera sana. Hiyo ni hatua nzuri ya uwazi na kuonyesha kwamba, Bunge linajua mambo ambayo yanatendeka sasa hivi na linataka majibu ya papo kwa papo na katika *issues* ambazo zitakuwa *topical*, kwa mfano, leo tumeputa *issue* kubwa sana; Rais Jakaya Kikwete, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa AU, kwa hiyo, hii ni jambo zuri na ninatumia nafasi hii kumpongeza sana, ninatumaini *appropriate* itafanywa na wanaohusika. Kwa hiyo ni jambo muhimu sana na mimi ninashangaa kwa nini watu wanaliogopa ogopa. Mambo yenye ni ya nchi yetu, tatizo ni nini; kama kuna jambo ambalo halieleweki vizuri kwa sasa hivi linaweza kuelezwaa tena baadaye, maana yake angalau katika wiki tatu, tutapata fursa angalau Alhamisi tatu za Waziri Mkuu kuweza kujibu maswali.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ninataka kuweka angalizo ambalo ni la maana, katika Mabunge mengi ya *Commonwealth*, nafasi hii inatambuliwa pia kama nafasi ambapo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, atajibishana na Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuwe wawazi tu ni vigumu sana wewe kwa upande wa Serikali *kum-face* ana kwa ana Waziri Mkuu, kwa *issues* ambazo ni nzito, jicho kwa jicho na mkaweza kujibishana; *we are trying to be an human*, kwa kawaida itakuwa ni vigumu sana kwa ndugu zangu ambaao wapo katika Kambi ya Chama Tawala, kuweza kufanya jambo kama hilo. Kwa hiyo, ili tutumie nafasi hii vizuri, ninawaomba wale viongozi wetu wa Bunge, labda watafute utaratibu ambaao ni mzuri, kwa mfano, katika utaratibu ule tunapozungumza wakati wa Kamati, wakati wa kupitisha vifungu mtu anapewa dakika, unauliza unapewa dakika kama tano, kwa hiyo, unaweza kuuliza swali ukapata jibu ukasema hujaridhika, ukauliza tena ukajibowi na nini, lakini katika muda ule ukimalizika, basi jambo hili liwe limemalizika. Ukifuata utaratibu huo, ndiyo kusema maswali sita tu peke yake yanaweza kuchukua dakika thelathini na bado hujatoa muda wa majibu.

Kwa hiyo, ni wazi kabisa kama kweli tunataka kutumia nafasi hii ya Waziri Mkuu ambaayo ni nadra na ni nzuri, inaonyesha wananchi wetu wataichangamkia sana saa hii kwa sababu tunaonyeshwa; uzuri wa siku hizi mambo ya mtandao, mambo ya televisheni, Waziri Mkuu anasimama anaonekana anavyosema na anaposema watu wanaangalia midomo yake na kila kitu na wanaweza kujua kama anasema ukweli au uongo. Hata wewe unayeuliza unaonekana kama unasema utumbo, watu watajua ahaa na huyu bwana mambo yake kama hayo. Kwa hiyo, kwa hali hii ya uwazi ni vizuri tukatumia nafasi hii

kwa ustadi zaidi. Kwa hiyo, muda ambao umewekwa wa nusu saa, wajaribu kuugawanya namna gani hautawezekana. (*Kicheko/Makofi*)

Katika Kanuni hizi hakuna mahali ambapo Mheshimiwa Spika, *do you respect* mimi ninakuamini kabisa kwamba, jicho lako litaangalia na upande wa huku, lakini mara nyingine huwa linaangalia juu zaidi na huku unaweza usione nafasi ya Kambi ya Upinzani kuweza kuuliza jambo. Kwa hiyo, ninaona ni lazima labda tungeweka kipengele ambacho kinamwajibisha *Presiding Officer* kutoa nafasi kwa Kambi ya Upinzani, kwa hali ya nusu kwa nusu kama ikiwezekana ili fursa hiyo ya kum-question *Prime Minister* kwamba, maswali ambayo Kambi ya Chama Tawala haiwezi ikamwuliza, waweze kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, hii ni nafasi nzuri, tuitumie vizuri, lakini tuweke muda ambao unafaa na tusilinganishe eti tutakata nusu ya maswali, hapana. Mimi ninaona wananchi sasa tunawatangazia, tumewapa nafasi ya Waziri Mkuu wenu saa nzima siku ya Alhamisi, watu wote kule watapiga vigelegele sana kwamba Bunge hili limewachagulia nafasi nzuri ya kusikia mambo ambayo Serikali inapaswa kujibu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii. Asante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea niseme tu kwamba, hata kwenye mjadala huu kila Mheshimiwa Mbunge wa Kambi wa Upinzani aliyeomba kuchangia, ameruhusiwa na Spika. Kawaida yangu mimi ni kusimama mahali pa haki, ninatambua sana Katiba imeweka wazi nafasi ya Upinzani Bungeni na mngejua Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani, mnalalamikiwa kwamba mara nyingine ninawapendelea. Kwa hiyo, ninadhani niko katika haki tu, kwa sababu upande huu wanasema na upande huu nao wanasema, basi ni vizuri, tutatenda haki tu. Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri.

MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, nami ninaomba niunge mkono hoja hii na niungane na wenzangu ambao wamependekeza kwamba, muda wa kipindi hiki cha *Prime Minister Question Hour* iwe ni saa moja badala ya nusu saa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilichonisimamisha ni kitu kidogo ambacho umekisema Mheshimiwa Spika kwamba, hii *question hour* ni ya Waziri Mkuu peke yake. Mimi ninakubaliana na hilo kabisa kabisa, lakini katika kuangalia Mabunge mengine, wakati huu wa kipindi cha saa ya Waziri Mkuu; Waziri Mkuu anayo fursa kwa sababu tuisahau ye ye naye ni binadamu, inawezekana kuna Waziri ambaye ana jibu sahihi zaidi, ninadhani ni vizuri tukamwachia Waziri Mkuu fursa ya kumgeukia Waziri fulani, ionekane kwamba ni sahihi kwa huyo Waziri kujibu kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwa hiyo, Serikali imejibu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninapendekeza kwamba, Waziri Mkuu ajitahidi kwa kiasi iwezekanavyo ajibu mwenyewe, lakini pale ambapo atajikuta anapata jibu la uhakika kutoka kwa Waziri, basi afanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, asante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hii itaharibu maana, mimi ninadhani tusirudi huko. *Prime Minister Question Time is Prime Minister Question Time.* Tunaendelea baada ya Mheshimiwa Ruth Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige. Nimefunga orodha yangu sasa, msiendelee kuleta maombi tena. Ninadhani tumepata changamoto ya kutosha. Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. (*Makofi*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Naibu Spika. Kwanza, nimpongeze na niipongeze Kamati ya Kanuni, waliofanya utafiti, iliyochambua ikaona ni vizuri washauriane na Serikali kuona kwamba, kuna umuhimu wa nusu saa kwa ajili ya kumwuliza Waziri Mkuu maswali na yeze aweze kujibu moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niwaunge mkono wenzangu ambao wamependekeza kwamba, Waziri Mkuu apewe muda wa saa moja. Mwanzo kabisa, nilikuwa na mawazo kwamba nusu saa inatosha, lakini jinsi ambavyo mjadala umeendelea, ninaona kuna haja ya saa moja.

Vilevile na mimi niliwahi kupata bahati wakati mmoja, kuhudhuria saa moja ya Tonny Blaire, ile saa moja Bunge linachangamka na nina hakika wale ambao wanakuwa ndani ya ukumbi na hata wale wanaokuwa nje ni saa moja nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ninamwamini kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu tulienaye sasa kwamba kwa kauli yake mwenyewe, kwa matendo yake mwenyewe tunavyoona kweli ni makini na ni mahiri. Mimi siamini kabisa kama atahitaji kusaidiwa na wala siamini kama ataweza akakosa majibu kwa swali lolote atakaloulizwa. Kwanza, ninaamini ameshauriana na Kamati ya Kanuni kukubaliana hoja hii iletwe hapa. Amejiandaa vizuri, kwa hiyo, mimi sina wasiwasi, utakapofika muda huo wa Mheshimiwa Waziri kujibu humu Bungeni, hakutakuwa na hofu ya namna yoyote.

Vilevile sidhani kama maswali atakayoulizwa humu ndani, yatahitaji mtu mwengine yejote wa nje kuweza kusema kwamba hapa labda kuna upungufu, kama yapo maoni nje yatatolewa kama kawaida, lakini kwa hapa ndani, ninaamini majibu yatakuwa yanayotosheleza.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili, ninaomba tukubaliane kwamba, hiyo saa moja ambayo na mimi ninaipendekeza kwamba ikubaliwe ni ya pande zote mbili; Kambi ya Upinzani wanayo nafasi na Kambi ya Chama Tawala inayo nafasi.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, hivi ni wakati gani ambapo Chama Tawala kimewahi kuwa na nafasi ya kukaa na Waziri Mkuu, kumwuliza maswali na yeze akawa

anajibu, mimi sikumbuki. Tunapokaa katika Vikao vya Chama, tunakuwa tunazungumza mambo ya Chama ambayo hakika hayana uhusiano wowote na halafu inakuwa ni siri, yaani tumekaa tumejifungia mahali. Tutakapokuwa tunamwuliza hapa Bungeni ni wazi vyombo vyote viko wazi na Watanzania wote wanaona.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuna hisia kwamba, labda Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala hawana hoja si kweli. Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala nao wana hoja ambazo zinawakera na wanglipenda kupata majibu ya Kiongozi wa Serikali, ambaye ni Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nafasi hii ndiyo ya kipekee. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile haiwezi kuwa nusu kwa nusu, pamoja na kwamba mimi nilikwisha kukwambia lakini Mheshimiwa Spika, siku nyingine unapendelea sana Kambi ya Upinzani ni kweli kwa sababu unawapa nafasi nyingi sana wakati si wengi sana wa kuweza wao kupata nusu kwa nusu kama idadi ya Wabunge wa Chama Tawala walivyo. (*Makofî*)

SPIKA: Wapinzani mnayasikia mambo hayo sasa! (*Kicheko/Makofî*)

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, itakapokuwa imefika siku ya Alhamisi, ninaomba wapewe nafasi zilizo *reasonable* kulingana na nafasi walizonazo Bungeni, asilimia yao ilivyo, siyo wapewe nafasi tano na Chama Tawala wapewe nafasi tano. Hiyo itakuwa kwa kweli haikuweza kutendeka haki.

Kwa hiyo, ninaomba nafasi hii pia itumike kwa haki na Chama Tawala wajione wana nafasi na Wapinzani nao waipate nafasi wanayoomba. Sote tunataka kusikiliza kwa kiongozi wetu, Waziri Mkuu ni mmoja na ni wetu sote, hakuna ambaye atasema ye ye anammiliki zaidi kuliko mwenzake, lakini tunapenda tupewe nafasi ya kumwuliza maswali na atujibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pendekero langu la kwanza, ninaomba saa moja tupewe. La pili, ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu, hana matatizo yoyote, atatujibu vizuri, asisaidiwe na Waziri mwingine yeyote, muda ule Mawaziri na wao wapumzike.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba kama inawezekana, ikipita hiyo saa moja, basi siku hiyo kusiulizwe tena maswali mengine, baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa amejibu ni kwamba, siku hiyo maswali yamefungwa, tutakuwa tumemaliza.

Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Ruth Msafiri asante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Paul Kimiti.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nishukuru kipekee kwa kunipa nafasi ya kuelekea mwisho mwisho kuchangia mada hii.

Mheshimiwa Spika, kimsingi ninakubaliana na hoja hii ya kuwepo hicho kifungu cha 38 kwenye Kanuni zetu, kwa ajili ya kupata muda wa kufanya mahojiano ya moja kwa moja na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu katika kuboresha hili, nilifikiri kwamba kwanza, ingefaa zaidi tukaitumia nafasi hii kujaribu kupata ufanuzi kutoka Serikalini na kwa maana hiyo, nilitaka kupendekeza pale ambapo Waziri Mkuu hayupo, basi hiyo siku mapema, kwa taarifa maalum ambayo inakuwa imeandaliwa, tuweze kuzungumza kuhusu suala la Wizara fulani. Kwa maana hiyo, siku ambayo Waziri Mkuu hayupo, basi tuweze kumhoji Waziri wa Wizara fulani kuhusu jambo fulani.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 63(3) ...

SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Maige, suala lililopo mbele yetu hapa ni *Prime Minister Question Time*, siyo lingine jamani. Kwa hiyo, tafadhalu rudi katika hoja. (*Makofi*)

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa hiyo, nilikuwa ninapendekeza kwamba, kwa kuwa masuala yapo mengi, basi tupate muda wa saa moja ambao wengi wameuzungumzia. Kwa hiyo, nilitaka na mimi pia kuongezea kwenye hilo, *of course* baada ya hilo la kwanza kuwa haliko sawa, *otherwise ninaunga mkono hoja*.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Maige, asante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Paul Kimiti, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na mwisho kabisa atamalizia Mheshimiwa John Malecela.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, nami ninapenda kuungana na wenzangu, kuunga mkono mapendekezo haya ambayo yameletwa na Naibu Spika, ambayo kwa upande wangu mimi ambaye nimekaa ndani ya Bunge hili kwa miaka mingi, ninaona ni ya kihistoria. Hivyo, ninafarijika sana ya kwamba, tumeanza kuleta mabadiliko makubwa sana katika nchi yetu. Ninakushukuru umeanza vizuri sana Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nia ya kujenga nchi hii ni yetu sote na si upande wa Upinzani peke yake. Jukumu letu ni kuhakikisha kwamba, Serikali inatekeleza wajibu wake kama inavyotakiwa na kama kuna makosa basi lazima tuyakosoe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, sasa leo nilipokuwa ninaangalia muda wa nusu saa nikauliza, hivi ni muda gani unamtosha Waziri Mkuu kujibu maswali ni nusu saa, saa moja, saa mbili au tatu? Waziri Mkuu, unaweza kumpa nusu saa akajibu maswali mawili, kutegemea atakavyovuta muda wake, ana haki kutumia muda mrefu kujibu swali moja akamaliza muda wake. Hilo la kwanza.

La pili, nisingependa kwa kweli kikao cha *question hour* ya Waziri Mkuu kikawa cha kuuliza maswali kama ni ya kawaida. Kiwe ni kikao rasmi cha ku-*question* utendaji wa Serikali yetu, cha kuulizia Serikali yetu utendaji wake, kama inavurunda ndiyo wakati mzuri wa kumbana Waziri Mkuu atusaidie. Sasa katika suala la kuuliza maswali, nilikuwa ninadhani mwanzoni nilipendekeza ya kwamba, dakika 45 zitumike *specifically* kwa maswali, lakini dakika 15 za kwanza, tumpe Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe maelezo ya mambo muhimu ambayo yanetokea katika nchi kwa kipindi hicho, itusaidie ili kuelewa mambo ambayo yanakwenda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, mwanzoni nilidhani kuna mambo mawili ambayo lazima tuyapendekeze hapa. Kwanza, muda ambao unatosha, kwa kuanzia hii saa moja tuigawe katika muda wa dakika 45 wetu wenyewe na dakika 15 za Mheshimiwa Waziri Mkuu.

La pili, katika mambo yale ambayo tunadhani ni muhimu kuwe na kipengele ambacho tunaweza kutumia kwa kutengua Kanuni, kama kuna jambo lolote muhimu, tunaruhusiwa kufuatana na Kanuni, tunaweza kubadilisha na kutengua kuongeza angalau muda kidogo ili kufafanua maeneo ambayo yatakuwa yamejitokeza. Ndiyo maana nikasema kwamba, saa moja ingekuwa ni nzuri, lakini pia tuwe na kipengele ambacho kinaweza kubadilisha Kanuni, tukatengua kama kuna jambo limejitokeza ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, asante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Paul Kimiti, ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba nitumie nafasi hii kwa ruhusa yako, kukushukuru wewe wenyewe, Ofisi yako, Serikali, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote wa Tanzania, kwa kuniombea dua wakati niko kwenye matibabu na leo Mwenyezi Mungu, amenijalia nimerudi tena hapa. Ninawashukuru wale wote walioniombea dua, walionipa huduma na afya yangu ni nzuri. *Inshallah*, tutaendelea na kazi pamoja hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupata fursa ya kuwa Mwenyekiti wa AU. Bara letu la Afrika, linakabiliwa na machafuko makubwa na yeche kwa uzoefu wake na kwa ahadi zake alizozichukua hapa Tanzania kwamba, atahakikisha Tanzania inabaki kuwa kisiwa cha amani, tunaamini tutamsaidia kwa pamoja tukishirikiana naye kuhakikisha Bara letu la Afrika linabaki nalo kuwa mfano. Kwa sababu huwa tunasema mambo yetu huanzia nyumbani, basi ninaamini pakitulia hapa petu nyumbani, atapata nguvu zaidi ya kuweza kuwaambia wenzake kwamba, jamani angalieni mfano wa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kukupongeza wewe, Kamati yetu ya Kanuni na Naibu Spika aliyewasilisha hoja hii leo kwamba, tendo hili lililotendeka ni la msingi sana katika mabadiliko makubwa ya kisiasa nchini kwetu. Toka nchi yetu ipate uhuru, hatukuwa na utaratibu wa maswali kwa Waziri Mkuu. Hili ni jambo la kwanza kabisa kufanyika, mimi ninaomba tulipongeze Bunge letu kwamba, sasa tunaingia katika mfumo wa demokrasia kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nne, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, suala la muda ni la muhimu sana. Muda wa saa moja ndiyo muafaka kwa Waziri Mkuu, kupata nafasi ya kuweza kujibu hoja mbalimbali zitakazowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Ninasema hivyo kwa sababu ni wakati pekee ambapo yale mambo ambayo yanalogusa Taifa letu, yanataka ufanuzi na pia kuvinyima Vyombo vyta Habari wakati mwingine visiandike vitu vya kubuni, basi ni wakati mzuri sana kulitumia Bunge, kuweza kutoa kauli sahihi kwa yale mambo ambayo yanawagusa wananchi kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakubaliana kabisa na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kipindi cha muda wa saa moja ndiyo muafaka kwa Waziri Mkuu kuweza kujibu hoja.

Tano, nikubaliane pia na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba ni vizuri tukautenga huu muda wa sasa moja kwa kuangalia kabisa uwiano wa aina fulani utakaowasadidua Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili, kupata fursa ambayo itatuwakilisha sote. Tuliopata bahati ya kupita katika Mabunge mbalimbali, sote tumegundua au tumekuta kwamba, nafasi za kwanza mara nyingi hupewa Kiongozi wa Upinzani, halafu baadaye wanapewa Wabunge wengine. Huo ni utaratibu wa kawaida ambapo Mabunge mengi yanafanya na sisi tunasema hatuko hapa kukomoana, tupo hapa kujenga nchi yetu. Tutahakikisha tunaendesha shughuli zetu kwa maslahi ya Wananchi wote wa Tanzania, hakuna hata mmoja atakayekuwa hapa kumkomoa mwenzake. Tutafanya kazi kwa uadilifu mkubwa, tukihakikisha kabisa Taifa letu linafaidika na yale tunayofanya ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba kwanza tusiwe na wasiwasi, tutakuwa *very constructive*, tutahakikisha tunauliza maswali ya msingi na tunategemea kwa kipaji na uwezo wa Waziri Mkuu, atatupa majibu ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba, ninaungana mkono hoja hii, lakini ninaomba tukubaliane katika suala la muda kwamba, muda wa saa moja utakuwa ni muafaka. Pili ni vizuri huo muda wenyele ukagawanywa vizuri ukaeleweka mapema ili kila mmoja ajue nafasi yake iko wapi katika kuuliza maswali hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ahsante sana. Mwisho, Mheshimiwa John S. Malecela.

MHE. JOHN S. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa AU. Ninampongeza hivyo kwa sababu ni lazima ieleweke kuwa, walikuwepo waliogombea wengine kwa mfano, kulikuwa na nchi ya Egypt walikuwa wanautafuta Uenyekiti huo, kulikuwa na Sudan walikuwa wanautafuta Uenyekiti huo, lakini walipoona Tanzania ni Kisiwa cha Amani na ndiye amependekezwa, wakatoa majina yao, kwa hiyo, Rais wetu akapita bila kupingwa. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami ningependa nichukue nafasi hii, nitoe wito kwa Bunge hili na kwa Watanzania wote kwamba, hii hali ya amani tuendelee kuilinda ili tuonyeshe kwamba, kweli waliomchagua Rais wetu wamefanya jambo la busara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa nije kwenye suala lililopo mbele yetu na ningependa niliseme kwa kifupi tu. Kwanza, wengine wanasema kama Waziri Mkuu hayupo awe mwakilishi wake; kwa nini? Jibu ni kwamba, sisi ndio tuliomchagua Waziri Mkuu, jina lake lilipendekezwa na Rais, halafu tukamchagua. Kwa hiyo, tuna imani naye, sasa akiondoka yeche, aje huyo mtu mwingine ambaye sijui atakuwa nani, mimi ninasema itakuwa ni kinyume kwa sababu hatukumchagua na akijibu majibu ya ovyo ovyo, hatuna haki ya kumfanya chochote. Tukiona Waziri Mkuu hatujibu sawasawa na yeche anajua kwamba tuna haki ya *vote of no confidence on him*. Ninamhakikishia Mheshimiwa Waziri Mkuu, si nia yetu hiyo ila nimelisema tu ili wananchi na Waheshimiwa Wabunge, wajue kwa nini tunasema Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika la pili, ninataka nikupongeze, wengine humu wameanza kusema tuwe sawasawa na Wapinzani, lakini jambo hili linatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, tangu umeanza kukalia kiti hicho, sijapata hata siku moja nafasi ya kunipa neno la kufikiri kwamba, kuna upande unaupendelea. Mimi nimeona umekuwa ukitoa haki kwa sisi sote na kwa hiyo, nina uhakika utaendelea hivyo. Juu ya maswali, mimi bado ninasema kama yatakuja maswali ya kejeli na ya kijinga, bado wewe kama Spika, unayo haki ya kusema kwamba, hilo si swali. Kwa hiyo, kwenye hilo mimi sina hofu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la muda, ningependa kusema kwamba, ninawasihi sana Waheshimiwa Wabunge wote, tukubaliane kwamba, muda uwe ni saa moja. Sasa katika ile saa moja, mimi ningesema kama Waziri Mkuu ana jambo lolote zito la kutuambia kwanza, tukumbuke anayo haki ya kufanya hivyo siku yoyote na Spika unasema tu Waziri Mkuu leo atatoa taarifa na atasimama hapo atatoa taarifa. Kwa hiyo, kwenye siku hiyo ya maswali ya Waziri Mkuu, kama anayo taarifa yoyote ya kusema, mimi ningesema badala ya kusema sijui iwe dakika ngapi, tuseme isizidi dakika kumi, kwa sababu tunatazamia kuwa, Waziri Mkuu anaweza kusema maneno mazito na ya maana katika dakika kumi. Kwa hiyo, tuseme isizidi dakika kumi. (*Makofi*)

Halafu tuje kwenye aina ya maswali; ninaungana na wenzangu wale waliosema maswali ya wakati huo yawe ni ya msingi, ya muhimu na yawe ni maswali ambayo pia yanaonyesha upeo. Mimi sitazamii nianze kuuliza habari ya barabara za Dodoma au

niseme Mtera kule kuna barabara yangu haipitiki, tuulize maswali ambayo yana upeo wa Kitanzania, yana upeo wa kimuongano na juu ya yote, turuhusiwe kuuliza maswali ya Kimataifa. Kwa mfano, ningependa wakati huo tumwulize baadhi ya maswali ambayo yanahusu *International Organizations*, tunafaidika na nini na wapi tunafanya nini? Nina hakika kwamba, wewe Spika, ukiona swali hilo ni gumu na linakwenda nje ya matumaini yetu, bado utakuwa na haki ya kusema hilo si swali na mtu akakaa tu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa niseme kwa upande wa maswali, bado tutategemea hekima na busara yako wakati wa kuuliza, kwa sababu mara nyingine mtu anaweza akafikiri hili ni swali la maana sana kwake yeye, lakini akiliuliza sote tukachecha, basi tukicheka ajue maana yetu ni kwamba, ameuliza swali ambalo kwa kweli si la kimsingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninaunga mkono hoja lakini nikisisitiza kwamba, muda wa maswali uwe saa moja na Waziri Mkuu asizidi dakika kumi. Ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja, kwa sababu mimi pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni, ninataka kusema mawili tu ya kufafanua.

La kwanza ni dhahiri, itanibidi nikae na Kamati ya Uongozi na Kamati ya Kanuni tutengeneze taratibu nzuri ambazo zitaitwa Mwongozo wa Spika, maana yake hapa mawazo yametoka mazuri sana. Sasa tusikiachie kiti, tuko wengi; yupo Spika, Naibu Spika na Wenyeviti sasa watakuwa watatu, tupo watu watano ambao tutaruhusiwa kwa Kanuni hizi kukaa hapa. Bila kuwa na Mwongozo ambao umepata mawazo ya wengi na Kamati ya Uongozi na Kamati ya Kanuni inazingatia tulivyo humu ndani ya Bunge, ninadhani tutakuwa tuna Mwongozo ambao ndiyo tutaugawa, kila anayetaka kusimama sasa kuuliza swali wakati huo kwa Waziri Mkuu, kwa mujibu wa Kanuni hii, atakuwa anaongozwa na Mwongozo ambao tayari upo.

La pili, ninadhani bado tunahitaji lugha yetu nzuri na tamu ya Kiswahili, sasa hapo ndipo tabu yake. Sisi ambao tumetembea na tumesikiliza maswali kwa mfano, *House of Commons*, hakuna kulemba na nini. Sasa wengine mnaotaka saa moja, maana yake fursa yenu ni ya kuogelea kwanza. Atasifia nchi yetu ilivyo nzuri na nini kilitokea viyi halafu ndiyo aulize swali. Hiyo siyo fursa. Kwa hiyo, nilikuwa ninataka kuweka wazi hilo ili twende tukiwa tunaelewana. Maswali ya *Prime Minister* ni *direct* na yanahusu jambo mahususi na yeye atajibu hivyo hivyo *direct*, kwa sababu ndiyo maana ni la papo kwa papo. Sasa ninamwita mtoa hoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba niwashukuru wote waliochangia mabadiliko haya makubwa katika kanuni zetu. Muswada huu sikutegemea kama utakuwa na wachangiaji wengi kama walivyojitokeza. Tumepata wachangiaji 19 na ningependa kuwataja; Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian,

Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Bri. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa John S. Malecela na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya ameandika mapendekezo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Waziri anapojibu maswali, anajibu kwa niaba ya sekta yake na kwa niaba ya Serikali. Naibu Spika anapojibu maswali ya Kanuni anajibu kwa niaba ya Kamati ya Kanuni na kwa niaba ya Spika. Kwa hiyo, haya mliyoniliza ni kwamba, yatarudi kwenye Kanuni. Kanuni yetu siwezi kufika hapa nikasema basi kuanzia sasa nitafanya saa moja, mimi madaraka hayo sina. Kwa hiyo, hoja ninadhani imesikika kwa wote kwamba, tatizo ni muda nilivyosikia mimi. Kwa hiyo, bado itarudi kwenye Kamati ya Kanuni yenewe na Kanuni yenewe ndiyo itaweza kusema iwe ama isiwe kwa kupendekeza hapa. Mimi kama Naibu Spika, hapa sina mamlaka ya kuamua kwamba, basi nimewasikieni inaelekea hoja ni kwamba mnataka saa moja, hapana. Kwa hiyo, ninadhani ndio utaratibu wetu wa Kanuni, mkisoma vizuri ndivyo inavyoeleza, lakini hoja ya kwamba pengine muda hautoshi imeelezwa.

Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke pia kwamba, hili suala ndiyo mara ya kwanza linaingia huku kwetu. Kanuni zetu sio msahafu, ndiyo bahati yetu nzuri, sio msahafu kwamba tukiamua ndiyo hatubadili. Tunaruhusiwa kubadili wakati wowote tunapofikiri kwamba, inafaa na mapendekezo ya kubadilisha Kanuni yanaweza yakatoka kwa Wabunge ama yakatoka kwa Spika au yakatoka kwa Kamati yenewe, hiyo ndiyo Kanuni yetu. Kwa hiyo, mimi ninasema hili suala bado litarudi kwenye Kamati watajadiliana, wakiona inafaa pengine itakuwepo, lakini kubwa tungenza maana yake tutakapoanza, mtakuta tunapata uzoefu wa aina fulani. Udhifu wetu kama alivyosema Mheshimiwa Spika na kama alivyosema Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Job Y. Ndugai ni kule kuanza kusimulia hadithi ambazo hazina uhusiano na kile unachotaka kuuliza.

Mimi pia nimehudhuria kipindi cha maswali cha Westminster wakati huo wala hakuwa Blaire, nilianza kusoma habari za kanuni mwaka 1980 nilipoingia Bungeni, nilikaa mwezi mzima kule Uingereza kufuatilia haya mambo. Waziri Mkuu katika muda mfupi anajibu zaidi ya maswali 120, sasa hapa Waziri Mkuu atakapowajibu kwamba hilo swalii sina habari amekaa, ninyi mtaanza kusema unaona Waziri Mkuu ameanza kujibu ovyo. Ndiyo majibu yanavyokuwa na kwamba sina habari ama atakwambia nitakwenda kutafuta habari, sio na yeze aanze kusimulia halafu mwishoni anasema sasa ninataka kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Hiyo itachukua muda, halafu hatuendi kwenye *substance* na wewe unayeuliza ni sharti uulize *direct questions* na utapata majibu ya *direct*. Sasa hilo kama hamtafanya, afadhali tujaribu kwa dakika 30 kabla hatujagombana kwa muda wa saa nzima. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge kweli kabisa tujaribu tuanze lakini tujifunze namna ya kuuliza maswali.

SPIKA: *Order, order please, tuna utaratibu humu hatuwezi kuzomeana tu!*

NAIBU SPIKA: Kwanza, mimi hata sikusikia kama wamenizomea.
(*Kicheko/Makofsi*)

Kwa hiyo, tunachokisema ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge hili lazima tubadilike nalo kwa sababu kwetu sisi tunatumia mtu mmoja dakika 20 kuuliza swali na dakika nyingine kujibu, kwa hiyo, unakuta wengi hampati nafasi. Kwa hiyo, hii itakuwa nafasi ya kujifunza namna ya kuuliza maswali mafupi na Waziri Mkuu atajibu kifupi hivyo hivyo.

La pili, Mabunge mengi na ninyi nyote mliokwenda kwenye semina mbalimbali hata za kwetu hapa, kuna kitu kinachoitwa *networking*, yaani mtu usisimame tu; unasimama tu unaanza kuuliza swali litakuwa halina uzito, lakini kama unajua Waziri Mkuu siku ya Alhamisi atajibu maswali, mnakuwa na hoja zenu mnazifanya kazi na pengine si lazima kila mtu aulize, anaweza kuuliza mmoja kwa niaba ya wote na likawa swali zito. Kama kila mtu atasimama, yatakuwa maswali mepesi kweli. Hiyo ni pande zote. Wakati mwengine katika kipindi hiki hakuna maswali ya Mpinzani au ya Chama Tawala, linaulizwa swali la Kitaifa, mnaweza pia mka-*network* ninyi nyote mkauliza swali ambalo linakuwa na uzito unaostahili. Hiyo pia ni stahili ya Mabunge, ukitaka hoja yako iwe nzito unazungumza na wenzio, si kukaa mwenyewe unasiliza wameuliza nini na wewe unasimama unauliza hivyo hivyo. Utaratibu mzuri ni kwamba, mnajifunza kufanya utafiti na kufanya kitu kinachoulizwa wiki moja baadaye, inakuwa hoja nzito. Sisi tuna tabia, kila mtu asimame mwenyewe aulize swali lake na pengine hata lisiwe na msingi sana kwa sababu amesimama tu.

Kwa hiyo, kitu kama *networking*, kufanya kazi kwa pamoja kuhusu hoja fulani za Kitaifa pia ni utaratibu ambao unakubalika katika Mabunge mengi na hasa katika hoja za siku hizi. Sasa hili nilifikiria ni suala mojawapo ambalo pengine tuanze kujifunza, sisi tuliookaa katika Mabunge ya zamani, *networking* ilikuwa ya muhimu sana. Utakuta mtu anasimama mwenyewe anatoa hoja yake, wengine wote ndio wanasilika kwa mara ya kwanza hapo hapo, hakuna mtu aliyemshirikisha mwenzie, anasimama wakati huo huo. Kwa hiyo, ule uzito wa hoja unapungua.

Kingine ambacho nilikuwa ninafikiria katika kipindi hiki, Waziri Mkuu anaweza pia akawaambieni nitajibu siku nyingine. Kuna maswali mengine mtamwuliza hapa, kama hana majibu atawea kusema nitajibu siku nyingine, nalo pia ni jibu. Sasa mtu asianze tena kumzomea anasema kwa nini amesema anajibu siku nyingine, anaweza akakwambia kwamba atajibu siku nyingine. Katika Kanuni zetu pia kuna mahali kuna Kauli ya Mawaziri, inawezekana alipojibu kwa kifupi hapa Serikali ikaona itoe Kauli ya Mawaziri, Waziri mwengine anayehusika na sekta ile, siku nyingine anaweza akatoa na yeye Kauli ya Mawaziri kuhusu swali fulani lenye urefu zaidi. Kwa hiyo, hayo yote mtegemee kwa sababu katika muda wa nusu saa, pengine majibu hayawezi kuwa marefu hivyo ya kutosheleza. Hiyo nafasi pia ipo, badala ya Mawaziri kumsaidia Waziri Mkuu, wanaweza kusaidia kwa namna nyingine ambazo zipo katika Kanuni yetu ikihusishwa na Kauli ya Mawaziri.

Waheshimiwa Wabunge ni kweli kama mlivyosema, *question hour* ya *Prime Minister* haiwezi ikajibiwa na mtu mwingine yeote zaidi ya yeye mwenyewe na siku mbayo atakuwa hayupo, itatolewa taarifa mapema kwamba, kesho *Prime Minister* hatakuwa na *time* kusudi wananchi wasijiandae wakati amekuwa na shughuli nyingine muhimu.

Kuhusu pande za Upinzani na kadhalika, kama tulivyosema, kwa kuanzia ninadhani lengo letu ni kuuliza maswali ya Kitaifa, ambayo yametokea wakati huu huu, yanaleta utata ama maswali mengi ambayo hayawezi kujibika. Kwa hiyo, ninadhani ndilo lengo la kipindi hiki. Ninaamini tukikitumia vizuri kipindi hiki, tunaweza kabisa kufika mahali pazuri na kufuatana na uzoefu tutakaoweza kuupata, kanuni zetu ziko wazi, hazizuii mabadiliko kama ulazima upo. Ninashukuru kwamba, Wabunge wote wameunga mkono hoja hii na kwamba, yale mliyopendekeza, yatarudi tena kwenye Kamati ya Kanuni ili yaweze kupata majibu. Kifungu cha 38 ndicho kitakachokuwa kinaruhusu Waziri Mkuu, kuweza kuulizwa maswali na yeye kutoa taarifa muhimu ambayo ninafikiri Wabunge wanapaswa kuifahamu.

Baada ya kusema hayo, ninaungana na wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa AU. Hii ni heshima kwetu kama Watanzania na pengine tunastahili, kwa sababu nchi hii ni kisiwa cha amani na tunaomba kisiwa hiki cha amani ni wajibu wa sisi Waheshimiwa Wabunge, kuendelea kuilinda amani tuliyonayo. Wabunge wana nafasi kubwa sana, kuendeleza Tanzania iwe kisiwa cha amani. Kwa hiyo, kauli zetu na misimamo yetu tunaposema tukiwa tunazungumza kama Wabunge ambao tunawajibika, tunaweza kujenga amani ya kudumu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mwongo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, nimeingiwa wasiwaso kidogo na ninaomba utusaidie mwongozo wa kiti chako katika utaratibu wa Kamati zetu, zinapowasilisha hoja Bungeni kupata maamuzi. Hivi Bunge linapotoa maamuzi kwa mfano, leo limesema tunataka saa moja, unachukuliwa tena uamuzi ule kurudishwa katika Kamati ikajadiliwe tena, inakuwa ni maamuzi ya Bunge au tunafanya maamuzi moja kwa moja hapa kwa sababu nilivyozae huwa unatuuliza wanaokubali saa moja au wanaokubali nusu saa; sasa utaratibu huu wa Kanuni mpya umebadilika, ninaomba mwongozo wako? (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa ninaelekea huko huko. Bila ya kurefusha mambo, tumeletewa hiyo kanuni hapa na Kanuni ya 30 fasili ya (4) inasema, kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, kitakuwa kila siku ya Alhamisi na kitazidi dakika 30; kuna ubaya gani kwa Bunge hili sasa hivi kusema itakuwa saa moja bila tena kwa Bunge hili kurudisha Muswada huu kwenye Kamati kuujaedili? Kamati walishasema dakika 30 wameleta hapa na Waheshimiwa Wabunge ndio wamesema saa moja, sasa turudi tena kutafuta kitu gani? (*Kicheko/Makofi*)

Jambo la pili, yale mambo mengine Mheshimiwa Naibu Spika ana wasiwasi nayo, wewe umeshatolea uamuza tayari baada ya hii kupita kwamba, utarudi kwa Kamati ya Uongozi na utushirikishe pia Kamati ya Kanuni ili utaratibu wa namna ya kuutumia huu muda uweze ukafanyika vizuri zaidi. Mimi ninaona tuheshimu kauli yako ambayo ni ya hekima na nzuri, lakini juu ya uamuza wa muda ambao ndio kitu pekee ninachokiona ambacho kimezungumzwa na Wabunge wengi hapa, tuamue hivi sasa, tubadili hiyo fasili ya 4 iseme saa moja biashara iishe, halafu tuanze mambo mengine. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimepokea maombi hayo ya kupata mwongozo wa Spika, lakini jibu liko wazi kabisa katika Kanuni zetu Kanuni ya 57. Hoja ikishatolewa ili iamuliwe, inaweza kubadilishwa kwa kuondoa maneno fulani na kuingiza maneno mengine kama vile dakika 30, 60, kuingiza au kuongeza maneno mapya, kuondoa maneno fulani bila kuongeza mengine.

Sasa nilidhani Waheshimiwa Wabunge, mlivyokuwa mnaendelea kujadili hapa, mmezingatia Kanuni hii ya 57(2), ambayo inasema; “Kabla ya kutoa hoja hiyo mto hoja atamkabidhi Katibu maandishi yenye saini yake na yanayoonyesha mabadiliko anayoyataka yafanywe.” Hadi sasa sijapokea mabadiliko yoyote na kwa hiyo, hakuna *debate*, hizi ndiyo kanuni. Hata za zamani ziko hivyo hivyo, kwa maana hiyo, hakuna badiliko lolote lililopokelewa na kwa hiyo hoja ile inabaki ilivyo.

Sasa nitawahoji hoja iliyo mbele yetu, imeungwa mkono na mazungumzo yamefanywa. Sasa nitawahoji, kama ni hivyo maana yake hoja inaondoka, kwa hiyo, *Prime Minister's Question* ndiyo haipo. Ndiyo ninavyouliza hivyo. Ninataka niwahoji tena tuelewane. Hoja iliyopo mbele yetu ni kuingiza katika Kanuni mpya ambayo inatenga muda kwa kumhoji Waziri Mkuu maswali, ndiyo hoja yenywewe; ninaomba muiamue.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya kutenga muda wa kumhoji Waziri Mkuu
ilipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Kwa hiyo, hoja kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Naibu Spika imepitishwa na kwa hiyo ninafurahi kulitangazia Bunge kwamba, Kanuni ya 38 sasa inaingia rasmi katika Kitabu cha Kanuni na ninashukuru sana kwa hilo. Asanteni sana. (*Makofî*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Ninaomba kuuliza kama tunaanza Alhamisi ijayo?
SPIKA: Amekumbusha jambo zuri sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ni dhahiri kabisa kutokana na mwongozo wangu wakati ninasimama hapa kwamba ili tutende haki, jambo hili linahitaji mwongozo kwa maandishi. Kwa hiyo, nitahitaji kushauriana na Kamati ya Kanuni na Kamati ya Uongozi ili kuutoa huo mwongozo utakaozingatia maoni mazuri sana yaliyotolewa katika kikao hiki. Kwa hiyo,

ninashawishika kusema kwamba, itakuwa vyema utaratibu huu tuuanze katika Mkutano wa 11. (*Makofi*)

Kwa makofi hayo, ninadhani umekubalika ili tutengeneze kitu kizuri tusianze vibaya. Ninashukuru sasa.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mabadiliko tulioyafanya leo ni sehemu ya mabadiliko ya jumla ya Kanuni za Bunge, ambayo yanatumika hivi sasa. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba mwongozo wako kwamba, hatuna haja ya kuwa na hoja katika mabadiliko ya Mheshimiwa Naibu Spika ya kusema kwamba, mabadiliko haya madogo yataanza kutumika mara baada ya Kikao cha Kumi, maana yake haya yanaingia kwenye kitabu cha jumla cha kanuni halafu inaweza ikatuchanganya *technically*.

SPIKA: Sijakuelewa vizuri Mheshimiwa Zitto, hebu rudia hiyo

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, mabadiliko ambayo tumeyafanya leo, yataingia kwenye mabadiliko ya jumla na yanakuwa ni sehemu ya Kanuni za Bunge. Katika maelezo haya, hakuna sehemu inayosema ni lini mabadiliko haya yataanza kutumika na kufuatia mwongozo wako, ina maana tunahitaji azimio la kusema kwamba, mabadiliko haya ni madogo, yataanza kutumika katika Mkutano wa Kumi wa Moja wa Bunge ili kuondoa mkanganyo, kwa sababu itawekwa kwenye kitabu kikubwa cha Kanuni za Bunge hili lina wiki tatu na leo ni kikao cha tatu tu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninaposimama hapa kutoa *ruling*, huo ndio uamuzi wa Spika. Kwa hiyo, kwa jambo dogo kama hili, kama tumekubali kimsingi tuwe na kipindi cha maswali cha Waziri Mkuu, tunakubali kama Bunge, kwa hoja hizo hizo mlizotoa kwamba, Spika aandae utaratibu mzuri. Spika hafanyi kazi peke yake, inabidi ashirikishe Kamati ya Kanuni na Kamati ya Uongozi, ndiyo muda huo unaouomba. Kwa *ruling* hiyo, maana yake ndiyo nimeshasema kwamba, utaratibu huo utaanza kutumika katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja, mwezi Aprili, 2008.

MHE JOHN M. CHEYO: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa ...

MHE. JOHN M. CHEYO: Kidogo tu Mheshimiwa Spika, *mood* ya Bunge zima ilikuwa ni saa moja, unaweza ukatupa mwongozo kama tunaweza kuleta *amendment* iwe saa moja na wakati huo ni wakati gani?

SPIKA: Kwa wakati huu, hilo haliwezekani, kwa sababu kanuni inatoka na uamuzi huo tuliopitisha. Sasa kuanzia hapo, ndiyo tunarudi pale pale aliposema Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna Mheshimiwa Mbunge mwenye mawazo tofauti

kuhusu hicho na kuhusu kanuni hiyo au nyingine, basi alete kwa utaratibu wa kawaida katika Kamati ya Kanuni ili tuzingatie. Asante.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vyta UKIMWI Nchini wa Mwaka 2007 (*The HIV and AIDS (Prevention and Control) Bill, 2007*)

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji kumi, nitawasoma majina ili wajiandae. Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Lediana M. Mngo'ng'o, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Maulidah A. Komu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama.

Kwa hiyo, bado muda unaruhusu na kwa sasa hivi kwa sababu ya udhuru maalum, ningeomba nimwite Naibu Spika aendelee na shughuli zinazofuata. Samahani sana, kumekuwa kama uvumi uvumi tu ambao tulipata; Mheshimiwa Rais wetu amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *African Union*, ninadhani ingekuwa vizuri kuhitimisha jambo hili, tukasikia kutoka kwa Waziri Mkuu, kwa sababu hizi taarifa za vyombo vyta habari mbalimbali hazitoshelezi, kwa hiyo, ninamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, nianze mazoezi ya kujibu maswali papo kwa papo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu na kuwaarifu Watanzania wanaotutazama kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amechaguliwa leo kuwa Mwenyekiti wa Nchi za Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina hakika hiyo ni heshima kwa Taifa letu na kwa kila Mtanzania. Nimearifiwa na Viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba, wanaandaa mapokezi makubwa hapo atakaporudi tarehe 2 Februari, 2008 jioni. Kwa hiyo, ningependa kutumia nafasi hii, kuwaomba wote ambao watakuwa tayari kumpokea Rais siku hiyo, wajitokeze kwa wingi pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Rais anakuja Dodoma tarehe 6 Februari, 2008, nina hakika Wabunge wako watakaopenda, wataweza kujiunga na watu wa Mkoa wa Dodoma kumpokea katika Uwanja wa Ndege wa hapa Dodoma. (*Makofi*)

Kama alivyosema Mheshimiwa John S. Malecela, hii ni heshima kwa Taifa letu, heshima kwa mambo yanayotokea katika nchi yetu, yanayotupa heshima duniani kwa vitendo vyetu sisi Watanzania na yeche kama kiongozi wa nchi yetu. Ninaomba

mshikamano, tumwombee ili aweze kuifanya kazi hiyo kwa heshima na atujengee tena umakini na umaarufu kote duniani.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuthibitisha hilo, hata mimi mezani hapa, nilikuwa nimepata taarifa za radio mabua, lakini nikaona itakuwa haina maana bila ya kulisikia kutoka kwako, kwa sababu tuko hapa Bungeni. Ninakushukuru sana kwa taarifa hiyo na nina hakika, Wabunge wote tutashiriki kwa kila hali katika kuweza kumpongeza Rais wetu, kwa heshima hii aliyoilettea nchi yetu. (*Makofi*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli ya Serikali. Sasa nitamwita Mheshimiwa Pindi H. Chana na Mheshimiwa Juma H. Killimbah ajiandae.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na Muswada huu unaohusiana na masuala ya *HIV* wa mwaka 2007.

Awali ya yote na mimi niungane na Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge, kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweza kuwa Mwenyekiti wa *African Union*. Hakika hii si bure ni kutokana na mambo makubwa mazuri ambayo nchi yetu imekuwa ikiyafanya. Kwa hiyo, ninampongeza sana, lakini zaidi ya yote, ninawapongeza Watanzania, wote kwa imani kubwa ambayo nchi jirani wamekuwa nayo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue nafasi hii, kumpongeza Mbunge mwenzetu ambaye ameapishwa hivi karibuni, Mheshimiwa Mchungaji Mama Getrude Rwakatare, ninampongeza sana kwa kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Vilevile nichukue nafasi, kutoa pole kwa familia ya Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge mwenzetu. Huu ni ukweli kabisa tumekuwa na pengo na ninawapa pole watu wote wa Kiteto.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja kwa idhini yako, ninaomba sasa niende kwenye huu Muswada unaohusiana na masuala ya *HIV*. Muswada huu ni mzuri na umekuja kwa wakati unaofaa, ingawa ni kweli kwamba umechelewa kidogo, kwa sababu janga hili la UKIMWI likuwepo muda mrefu sana, lakini wenzetu wana lugha inayosema; “*Better late than never.*” Kwa hiyo, maadamu umekuja, tunaupokea Muswada huu na nianze kwa kusema ninaunga mkono hoja. Janga la UKIMWI limekuwa ni kikwazo katika nchi yetu, watu wengi wamekuwa wakitumia muda wao mrefu kuangalia watoto yatima, kuangalia wagonjwa limekuwa ni tatizo kubwa. Kimsingi tatizo hili la UKIMWI watu wengi wamelipa tafsiri mbalimbali, kwa hiyo limekuwa ni janga kubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja, nikienda katika kifungu cha masuala ya *interpretation*, kwenye tafsiri kuna tafsiri inayozungumzia suala la *Local Government Authority*. Ninakubaliana kabisa na tafsiri hii, kwa mujibu wa Muswada imesema, *it means the Local Government Authority established under the Local Government District Authority Act and the Local Government Urban Authorities Act*. Ninashauri Serikali iangalie kuongeza mwaka wa hiyo *Local Government Act*, waongeze maneno yafuatayo mwaka 1982 as amended.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika kifungu cha sita, kimeelezea majukumu ya sekta mbalimbali kwamba, zitakuwa na majukumu ambayo zinahusiana na masuala haya ya *HIV*, zitapewa majukumu ya kupanga *plan* na kuprogramu shughuli mbalimbali za masuala ya UKIMWI. Pamoja na kupanga huku shughuli mbalimbali za masuala ya UKIMWI, Muswada unaelekeza kwamba, programu hizo na mipango hiyo kabla ya utekelezaji ni lazima ipelekwe *TACAIDS* ili *TACAIDS* waweze kuratibu na kushauri. Hapa tukizungumzia *TACAIDS* kwa jinsi ninavyofahamu, ofisi zao zimekuwa *centralised* Dar es Salaam, lakini mipango hiyo ya shughuli za UKIMWI kuna watu wako kule Ludewa, Makete, Mufindi, Kilolo sasa shughuli zote kabla ya utekelezaji tukisema lazima zifikishwe *TACAIDS* ili watoe baraka ndipo zitekelezwe, hili ni jambo kwanza linachukua muda mrefu na litakuwa lina gharama kubwa. Kwa hiyo, aidha, *TACAIDS* iwe *decentralised*, ofisi zao ziwepo katika Halmashauri za Wilaya au tuangalie kutumia *system* ya *Local Government* iliyopo, lakini tukisema kwamba, mipango yote ni lazima ifikishwe *TACAIDS* ni kweli itakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, ninatoa ushauri *TACAIDS* iwe *decentralised* kufikishwa kwenye *Local Government Authority* au jambo hili lifanywe na *Local Government Authorities*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia sehemu ya 3 kipengele cha 7 kinazungumzia juu ya elimu kwamba, wadau mbalimbali wanaoshughulikia masuala ya *HIV* iwe ni Wizara na *Media* watashiriki kutoa elimu kwa jamii. Hili jambo ni muhimu na ni zuri sana, kwa sababu kama nilivyosema, UKIMWI umekuwa ni janga kubwa, watu wengi wanatoa tafsiri mbalimbali. Wengine wanauita ngoma, umeme, wamredio au wanaita wamTV. Kwa hiyo, imekuwa ni janga sasa hapa. Kwa kuwa wadau mbalimbali watashiriki katika kutoa elimu, ninatoa ombi kwa Serikali, ijaribu kujadiliana na vyombo vya *media* na *press* ili tatizo hili wakiweza watoe kwa bei nafuu au ikiwezekana iwe ni bure kabisa. Wanapokuwa wanatoa matangazo mengine ya biashara, wanachaji fedha kadhaa na hili ni janga watu wengi wanakufa. Kama tunawenza kutoa dawa za *ARV* bure, basi tujadiliane na wahusika wa vyombo hivi ili ile elimu kwa wananchi wetu itolewe bure. Watu wengine hawajui hata kama tatizo hili linaitwa upungufu wa kinga, yaani UKIMWI, ndiyo maana wanasema wamredio, yaani wanaulizana anaumwa nini, wanasema anaumwa ule ugonjwa wa kwenye redio kwa sababu hawaelewi.

Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kuishauri Serikali kwamba, tuangalie jinsi ya kukaa mezani na kujadiliana na vyombo hivi vya habari, iwe ni magazeti, TV au redio. Wakati umefika sasa kila mwananchi aweze kupata elimu hii kwamba, UKIMWI ni kitu gani, unaambukizwaje, taratibu zipi zitumike katika kinga na kadhalika na kadhalika.

Kwa hiyo, ni ombi langu, Serikali iangalie jinsi gani inaweza kuzidisha kutoa ufahamu juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya suala la *gender*. Nimeona Muswada huu umetambua suala zima la jinsia. Ninazungumzia jinsia kwa sababu ni kweli kwamba, waathirika kweli ni wanaume na wanawake. Katika nchi yetu, wanawake ni wengi ukilinganisha na wanaume. Wanawake wapo karibu asilimia 51 ya idadi ya watu milioni 36 au milioni 34 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002. Sasa kama wanawake ni wengi, maana yake tunapozungumzia umaskini basi wanawake ni waathirika zaidi, tunapozunguzia janga la UKIMWI wanawake ni waathirika zaidi, ndiyo wanaolea watoto yatima, ndiyo wanaowaangalia wagonjwa. Endapo kuna masuala ya kutafuta maji huko vijiji, wanawake ndio wahusika wakuu.

Kwa hiyo ni ombi langu kwamba, katika utekelezaji wa Muswada huu unaohusiana na masuala ya *HIV* iwe ni elimu, iwe ni *donors* wanapokuja katika nchi yetu kutoa misaada au ufadhili wa aina mbalimbali, kundi hili la wanawake ni muhimu sana likaangaliwa na kupewa kipaumbele. Katika nchi yetu kuna mambo mengi sana, ambayo yanamuweka mwanamke nyuma, mambo hayo yapo na sisi sote ni mashahidi. Mira na desturi zipo kwa mfano, baadhi ya maeneo mpaka sasa wanaendelea kutumia utumaduni wa ukeketaji, hili bado ni tatizo kubwa sana na mwathirika pale anakuwa ni mwanamke. Vilevile wakati mwingine, zipo Sheria nyingine zinasema kwamba, *there shall be a chairman*. Sasa ile *man* inapokaa mwisho, inakuwa ni kazi, *unless tuseme there shall be a chairwoman* au *there shall be a chairperson*.

Tukienda kwenye Muswada huu huu kifungu cha 36 kimesema kwamba, kutakuwepo na Kamati (*National HIV and Research Fellowship Committee*), kimeonyesha *members* watakuwa ni akina nani na moja kwa moja kwenye (a) pale kimesema *chairman*. Kwa hiyo ni ombi pia pale kwenye neno *chairman* libadilishwe liwekwe *chairperson* ili wanawake nao waangaliwe kwa sababu wana mzigo mkubwa sana.

Mheshimiwa Niabu Spika, kifungu cha 34 kinaelezea kwamba, watu ambao ni waathirika zaidi ni watoto ambao wanatakiwa wapate elimu na huduma mbalimbali za afya. Nigeppenda kuishauri Wizara, kwa maoni yangu, baada ya neno watoto kwa mfano, kwenye kifungu cha 34(1) mstari wa tatu kinasema, *the most vulnerable children within its respective area*, baada ya *children* pale iongezwe and women. Tukija kifungu cha pili vilevile kinasema, *the most vulnerable children* tuongeze tena and women na pale kwenye kifungu cha tatu kinazungumzia *the most vulnerable children includes orphans and women* ili wanawake nao waweze kupunguziwa mzigo huo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 12(3) kinaelezea juu ya *penalty* isiyopungua kiasi cha shilingi laki tano. Wapo baadhi ya watu ambao itakuwa ngumu sana kutekeleza, sasa ni muhimu Wizara ikaangalia, kama mtu akishindwa kutekeleza ile *penalty*, kuna *option* nyingi ya adhabu nyingine ambayo itafaa, maana hii ni *offense* au kosa la jinai. Pale ambapo daktari wa meno anamtibu mtu meno bila kuchemsha vifaa au

kutumia vifaa vya ncha kali na kumwambukia mtu bila kuangalia. Kwa hiyo, kama ni *offense* tukisema kwamba *penalty* yake ni shilingi laki tano, *suppose* mtu amefeli kulipa laki tano basi kuwe na *option* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15(5) kinasema, *every pregnant woman and every person attending healthcare facility shall be counseled and offered voluntary HIV testing.* Hili ni jambo muhimu sana, lakini ushauri wangu pale imesema *every woman and every person*, sasa ukishasema *every woman and every person*, kwa maoni yangu huyu *woman* naye ni *person*. Kwa hiyo, *every pregnant woman* ninashauri tungei-delete ili ibaki *every person*, maana *every woman* inaingia kwenye *every person*. Vilevile kifungu cha sita kinaelezea kwamba, watoa huduma watapimwa. Sasa swali langu ni kwamba; je, wakipimwa na ikaonekana kwamba ni *positive*; je, wataendelea kutoa huduma za afya?

Ninadhani hilo liangaliwe na kiwepo kifungu kabisa kwamba, watoa huduma baada ya kupimwa na ikaonekana naye amekuwa *affected*, si vyema sana akaendelea kutoa huduma hizo za afya, kwa mfano, upimaji na kadhalika, kwa maana watakwenda kutumia vifaa vya ncha kali na inaweza ikamletea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ni ya tano ambayo inazungumzia suala la usiri, imeelezea kwamba, mtu akitoa siri juu ya masuala ya upimaji, itakuwa ni kosa. *Penalty* yake au adhabu yake imeonyeshwa sehemu ya kumi na moja. Kwa hiyo, ninashauri katika kifungu hiki cha tano, ileze kabisa kwamba, itakuwa kosa na ileze kwamba, *penalty* yake itaonekana katika kifungu cha kumi na moja pale kwamba *it will be an offense*. Vilevile kifungu cha 21 kinaelezea mtu akimwambukiza mwingine pale yeye anapojija ana-HIV, adhabu yake ipo kwenye kifungu cha kumi na moja, lakini kosa lenyewe lipo sehemu nyingine. Waelezee kwamba, mtu akijua kwamba ana-HIV hajamwelezea mwenzi wake au mke au mume wake, itakuwa ni kosa. Kwa hiyo ni muhimu kuipa *status* kwamba, itakuwa ni kosa na adhabu yake itakuwepo kifungu fulani, kwa sababu mtu yejote utakayemwambukiza ni sawasawa kama umemwekea *timing* bomu mwenzi wako kwamba, baada ya muda fulani naye atakufa. Kwa hiyo, hiyo ni sawa kabisa na kuiita ni kesi ya mauaji ama ni kesi ya *murder*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ni kuongeza waathirika katika *section* ya 36(2)(a). Wameonyesha ni wadau gani ambao wanatakiwa kuingia kwenye Kamati ya UKIMWI, kwa hiyo ni muhimu sana kuongeza wale watu ambao wanaishi na virusi wawe *one of the members*. Wameweka tu wataalam *representing higher learning institution*, lakini hawajaweka waathirika kuwa Wajumbe wa Kamati ya *Research Fellowship Committee*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na niseme kwamba, ninaunga mkono hoja, nikiendelea kuweka msisitizo kwamba ni muhimu sana kundi hili la wanawake likazingatiwa. Ninakushukuru sana. (*Makofii*)

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu jioni ya leo, kuhusiana na masuala ya

Muswada huu muhimu. Kabla sijaanza kuzungumzia Muswada wenyewe na mimi kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Iramba Magharibi, kwa sakafu ya moyo wangu na kwa dhati kabisa, ninapenda nitoe pongezi za dhati kwa Rais wetu mpandwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa *African Union*. Kuchaguliwa kwake ni sifa ya Watanzania wote kwa ujumla, kwa hiyo, anastahili pongezi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii ya pili pia niweze kutoa salamu za rambirambi kwa aliyejikuwa Mbunge mwenzetu wa Jimbo la Kiteto, Marehemu Benedict Losurutia, kwa Bunge zima na kwa Wananchi wa Jimbo la Kiteto. Ninaamini kwamba, Mwenyezi Mungu atawapa subira katika wakati huu mgumu baada ya kupata kifo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia nimpongeze Mheshimiwa Mchungaji Getrude Pangalile Rwakatare, kwa kupata nafasi ya Ubunge na kuingia kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninasema sisi Wabunge tunashukuru sana na tunakukaribisha, lakini ninaamini ujio wako ndani ya Bunge, utakuwa na baraka kubwa sana kwa sababu wale ambao watahitaji neno la kiroho, basi ninaamini utatoa huduma hiyo na kadhalika. Kwa sababu yeye ni mdau mkubwa wa elimu, basi itakuwa ni fursa nzuri hata kwa Wabunge, kupata ushauri kwake kuhusiana na masuala mbalimbali yanayohusu elimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Muswada wenyewe. Mimi ninaipongeza Serikali kuleta Muswada huu muhimu. Ukweli ni kwamba, UKIMWI unanitisha na unaua. Nguvu kazi na rasilimali nyingi ya taifa inakwenda, kwa sababu tatito hili la UKIMWI huanza taratibu; linapomwanza mtu kwa imani, anaamini kwamba, atapata tiba; anaanza kutoa rasilimali zake na anajitahidi mpaka zinamwishia, yeye anakwenda na anaiacha familia ikiwa maskini. Kwa hiyo, hili janga kwa kweli sote tunalionia; ni kubwa na ambalo linahitaji liwekewe mkono wa Serikali na sisi Wabunge kama wawakilishi wa wananchi, lazima tukae na kujadili kwa kina, tuone namna tutakavyoondokana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru pia Serikali, kabla ya kuleta Muswada huu, imekuwa ikionyesha juhudzi za makusudi, ambazo kwa namna moja ama nyingine ni katika dhamira ya kuwapenda watu wake; imekuwa ikitoa ushauri na kwa wale ambao wameonekana kuwa na maambuki za virusi vya UKIMWI, wameweza kupatiwa dozi ya ARV. Haya yote tunayakubali, tunasema ni mapenzi makubwa kwa Serikali na tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija ndani ya Muswada wenyewe, sehemu ya tatu inazungumzia kuhusiana na elimu. Ninaamini tangu UKIMWI umekuwepo ndani ya nchi yetu, elimu imeweza kutolewa vya kutosha sana na Serikali yenyewe au na asasi zisizokuwa za Kiserikali na pia kumekuwepo Kampeni ambazo pengine zinafanywa hata kwa ngazi ya familia na kadhalika. Ninaona katika utoaji wa hii elimu, bado kuna matatizo na hasa kwa sababu zipo pesa nyingi zinazotumika kwa elimu zaidi kuliko pesa hizo kutumika kwa ajili ya kuweza kutoa lishe, kwa wale ambao wamepata maambukizi ya ugonjwa huu wa UKIMWI. Wapo watu ambao wamegundulika na wana maambukizi

haya, lakini badala yake unaweza ukakuta kwamba, tunaendelea na elimu na pesa zinawekwa kwa elimu. Kikubwa zaidi, mwaka 2007 tulipokuwa kwenye Bunge la Bajeti, tulitenga pesa karibu kwa kila Wizara na tukasema kwa sababu hili ni suala mtambuka, kila Wizara inahusika, lakini mbona hili suala la UKIMWI linaachwa peke yake kwa Wizara ambayo inaonekana, Ofisi ya Waziri Mkuu ya Maafa na UKIMWI. Sisi hatuoni kwa namna moja ama nyingine, Wizara nyingine zinafanya kazi gani fedha hizo ambazo tulipitisha ndani ya Bunge hili na ili ziweze kufanya kazi zikishirikiana na hizo za fungu ambalo lipo katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la elimu ni lazima kama ni nguvu basi ilishatolewa ya kutosha, sasa tuelekee kwenye kiini na tutakaposema tunapitisha Muswada huu hasa, pesa nyingi ambazo zitakuwa zinapatikana kwa njia za misaada, zielekezwe kwa ajili ya kuweza kutoa lishe kwa ambaao tayari wameshapatikana na huu Ugonjwa wa UKIMWI. Sehemu ya nane, kifungu cha 35 na hata kwenye marekebisho imeeleza, nitakwenda kwenye kipengele (b), hii sehemu ya 35 inazungumzia juu ya hizi Asasi Zisizo za Kiserikali, pamoja na haya mashirika ya kihari ya kidini, kuweza kupokea misaada na namna ya kuweza kutumia misaada hii inayohusiana na masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pamoja na utaratibu uliopo, mfumko mwingi wa hizi asasi zisizokuwa za Kiserikali na utendaji kazi wake kuhusiana na musuala haya ya UKIMWI, kwa namna moja ama nyingine, unaleta mashaka sana na hasa pale pesa zinazopatikana na zinapotumika kwa walengwa na bado hakuna uwazi na utaratibu ambaao unaonekana, utaratibu ambaao unaonufaisha walengwa. Kwa hiyo, mimi ningombwa katika hili, Wizara tutakapokuwa tunahikisha na hili ninataka liingie hata kwenye Muswada kwamba, pamoja na hizi *NGOs* ambazo zimesajiliwa kwa uhalali, lakini lazima Wizara ya Afya izitambue bayana ni zipi zinazoshughulika na UKIMWI. Utaratibu ueleweke, misaada inapopokelewa inatumika kwa namna gani.

Kipengele (b) kimependekeza adhabu uki-*misuse* hizi pesa kinasema; *of any NGO, CBO, FBO, Private Organizations or Corporations to fine of not less than five million shillings and not exceeding five million.* Sasa ninasema tu kwamba, *NGO* imepata mamilioni ya pesa; imepata karibu milioni 100 lakini ika-*misuse* hizi fedha halafu akienda pale akapatikana na hatia, unamtoza *fine* ya milioni tano. Milioni tano kwa fedha ambazo amezipata za milioni 100. Ninapendekeza kwamba, uwepo utaratibu; *NGOs* yoyote ikipatikana na kosa la ku-*misuse* hizi *fund*, lazima uzirejeshe na iondolewe kwenye daftari la usajili, kwa sababu imekosa uaminifu na imekosa uwezo wa kuendesha shughuli kwa mujibu inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 47 kimezungumzia juu ya adhabu ya anayeambukiza virusi vya UKIMWI kwa makusudi. Hapa bado ninashindwa kuelewa, huyu mtu tunaweza tukampata vipi kwamba leo kaja kaambukiza na suala la mapenzi au suala la kufanya mapenzi, linashirikisha watu wawili na ni suala ambalo linakuwa ni la siri; lakini leo hii tunasema kwamba tuitishe Muswada huu tukiamini kwamba, huyu mtu ameambukizwa? Sasa sijui tutaweza kugundua vipi, maana yake kama

walivyozungumza walionitangulia, yawezekana kabisa kati ya wenzi wale wawili, wakawa wote tayari wana maambukizi na tayari wakawa wamekutana lakini kwa makusudi mmoja anataka kumkomoa mwenzake?

Sasa ninasema kwamba, Waziri atakapokuwa anatoa ufanuzi, atuambie *methodology* ya kuhakikisha kwamba, huyu anachokisema ndicho sahihi na si uongo. Pengine tuna adhabu ambayo tumesema imependekezwa kwamba, mtu akipatikana na kosa hili, ahukumiwe kifungo cha miaka mitano na kisizidi miaka kumi. Tatizo la huko gerezani kama tunavyosema, magereza yetu tunayajua, matatizo ya mlo mmoja unajulikana, lakini bado hatujazungumzia hata huko magerezani wako amba wana maambukizi ya virusi vya UKIMWI, sijui tunawasaidiaje? (*Makofi*)

Sasa tunapompeleka mtu gerezani, anakula mlo mmoja kwa kipindi hiki cha miaka mitano kiama, angeweza kuishi huku katika hali ya kawaida kwa kipindi cha miaka ishirini, basi ninaamini miaka mitano hiyo itapungua kutoka ishirini na anawenza akaishi kwa miaka hiyo mitano na hata akitoka sidhani kama atawenza kuendelea kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninataka nichangie hayo. Ninaipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa Muswada huu mzuri na ninasema ninauunga mkono kwa asilimia mia moja. Asate sana. (*Makofi*)

MHE. DR. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaomba nichukue nafasi hii kwanza, niwatakie Waheshimiwa Wabunge wote, pamoja na wewe na Mheshimiwa Spika, heri ya mwaka mpya wa 2008. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuvusha na ninaomba aendelee kutupa baraka na afya njema tuwatumikie Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *African Union*. Hiyo imetupa sifa na ninaamini kwamba, sisi sote ni wadau wa amani, kwa sababu Tanzania tunapewa sifa kwa kuwa na amani. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kuhimiza na kuboresha amani ndani ya jamii ambazo tunaziongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Rais, ningependa nichukue nafasi hii sasa nitoe rambirambi kwa Wananchi wa Jimbo la Kiteto. Rambirambi hizi zinatoka kwa Wananchi wa Morogoro, kuwapa pole kwa kufiwa na mpandwa Mbunge wao, ndugu yetu, Marehemu Benedict Losurutia. Ningependa pia nichukue nafasi hii, kumpa pole Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, kwa kufiwa na mpandwa mke wake. Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nichukue fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare kwa kuapishwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamkaribisha tuunganishe nguvu zetu, tuweze kulisukuma gurudumu la maendeleo kwa Wananchi wa Mkoa wa Morogoro. Mama karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nimpongeze mtoa hoja, pamoja na Naibu wake, wataalam wake na wadau wote ambao wamechangia katika kuutengeneza na kuuboresha Muswada huu, ambao umekuja kwa wakati muafaka ambapo janga la UKIMWI linaendelea kuwa ni nyundo kubwa ya kuzuia maendeleo ya Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nichangie kwa nia ya kuboresha. Ninaomba nichangie kwa ujumla kwa sababu kwenda kipengele hadi kipengele, itachukua muda, nitashindwa kuzungumza ninayotaka kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Muswada huu inazungumziwa elimu ya UKIMWI na usambazaji wa elimu ya UKIMWI. Wizara ya Afya na Serikali yetu imejitahidi, lakini ninaomba kusema kwamba, njia zinazotumika kutoa elimu ya afya na usambazaji wa elimu ya afya kuhusu UKIMWI, zinabagua kidogo, kwa sababu wananchi walio wengi walioko vijijini hawawezi kupata hizi habari, kwa sababu zinatumika televisheni na redio. Wananchi wengi sasa hivi unapopita kwenye vijiji vyetu, hata ile redio ya kusikiliza wanashindwa kuwa nayo, kwa sababu ya ugumu wa maisha. Ningependa nipendekeze kwamba, sasa hili suala la UKIMWI lichukuliwe kama ni suala la kijamii na tujaribu kui-focus mikakati yetu kama ifuatavyo:-

Tuhamasishe familia zizungumzie UKIMWI kwenye ngazi ya familia. Zipo nchi ambazo zimeanza kuzungumza na watoto majumbani; baba na mama, kaka na dada na wengine wote wanazungumzia UKIMWI kama suala ambalo linafanya wao washindwe kupata huduma nzuri na maendeleo, kwa sababu umaskini wa nchi unakuwa *translated* kwenye *hard life* kwa wananchi wake. Jambo hili tuliangalie kwa namna ambavyo tunaweza tukafanya *complete community mobilization*. Tuanze tena upya kuhamasisha viongozi wa dini misikitini na makanisani; kwenye misikiti kuna swala za Ijumaa, masheikh wajaribu kuangalia namna ambavyo wataingiza hata neno moja tu kuhusu UKIMWI, unyanyapaa au namna ya kuacha zinaa na matatizo mengine ambayo wanafikiri yanaleta maambukizi katika jamii; na makanisani kwenye mahubiri, tuwaombe wachungaji, mapadri na wengine wote ambao ni wadau muhimu, kwa sababu bila kuwepo na wananchi wenyе afya njema, hawatapata waumini. Waangalie namna ambavyo wataliangalia tena upya hili suala, tusiliangalie tu kwa mtazamo wa kutenda dhambi ndiyo kupata UKIMWI, tuliangalie sasa kwa mtazamo wa kuboresha afya za waumini wetu.

Kwa hiyo, litolewe makanisani, kwenye shule za watoto wadogo (*Sunday Schools*) wazungumzie, wale watoto wanaelewa kwamba kuna UKIMWI, tuangalie lugha ambayo tutawazungumzia. Nchi ambazo wamekubali kuchukua hiyo *approach* ya kuzungumza na watoto kuanzia kwenye umri mdogo kwenda mashulen i mpaka vijana kwa njia endelevu, imeweza kuleta matokeo na mafanikio mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahali pengine ambapo ninafikiri kwamba ni vyema Serikali pia ikawashauri viongozi wa dini; wanakumbuka kuwatuma wanaofunga ndoa kuja kupimwa UKIMWI, lakini wanapowapa mafunzo ya ndoa, hatuna uhakika kama wanazungumzia juu ya UKIMWI na wanazungumzia jinsi ambavyo kama kwa

bahati mbaya mmojawapo anapata UKIMWI, wanawezaje wakaishi kwa amani na kwa njia ambayo hawataambukizana katika jamii yetu. Ninaomba hilo liangaliwe na viongozi wa dini, basi iwe ni changamoto yao ya namna ambavyo wanaweza wakaingiza mafunzo ya UKIMWI katika mafunzo ya kutayarisha wanandoa watarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kuzuia, ninaomba nizungumzie kondomu. Mwanzo kwenye miaka ya tisini, Serikali yetu ilikuwa inatoa kondomu kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, hospitalini na mahali popote ambako kulikuwa na mdau ambaye alikuwa tayari kutoa elimu ya kondomu na kuweza kugawa zile kondomu kwa njia ambayo ilikuwa ni sahihi.

Bahati mbaya, kwa kipindi hiki ninafikiri hiyo fursa ya kuwa na kondomu za kuweza kugawa haikuwepo, lakini pia ningependa kusema, kumetokea mfumo kwamba, kwenye maduka ya dawa wanaiza kondomu hata vijijini, lakini kwa bahati mbaya, hakuna mtu anayetoa elimu ya matumizi bora ya kondomu kule vijijini hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye sehemu za kazi, kumekuwa na mtindo wa kuweka kondomu chooni. Sasa kama hizi kondomu mnasema zitumike kwenye tendo la ndoa, watu wanafanya mapenzi chooni au tendo la ndoa limekuwa ni chafu kama uchafu unaokwenda chooni! Ninaomba tusianze kunyanyapaa uzuiaji wa kuenea kwa UKIMWI, kwa kuweka hizi kondomu chooni. Kama kondomu zipo, watu waelimishwe na waambiwe kwamba ukizitaka zipo kwenye ofisi ya fulani, zipewe heshima yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kondomu za kike; akina mama tumekuwa ndiyo wahanga wakubwa wa kuambukizwa UKIMWI kwanza, kwa kutokujua na pili kwa kutokuwa na nyenzo za kutusaidia kujikinga. Ninaomba Serikali yetu iangalie uwezekano wa kuweza kusambaza kondomu hususan vijijini, pamoja na elimu yake. Kondomu za kike zinaweza kutusaidia kwenye uzazi wa mpango, pamoja na kuzuia magonjwa yaambukizwayo kwa njia ya kujamiihana na kuzuia hili janga. Ninafikiri Serikali yetu ina uwezo wa kusambaza kondomu. Tunaomba hilo liangaliwe na litiliwe mkazo, kwa sababu itikadi za dini zipo tunaziheshimu, lakini tunaposema kama taifa tunatangaza vita dhidi ya UKIMWI, basi tutumie silaha zozote zile kwa sababu tunataka kulinusuru taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nilishukuru taifa letu kwa kutoa fursa kwa wananchi ambao wameathirika, kuweza kupewa tiba ya kuweza kurefusha uhai wao na kupunguza makali ya UKIMWI. Ninaomba niseme kwamba, mfumo unaotumika sasa hivi hauna manufaa makubwa sana kwa wananchi hususan wa vijijini. Mwananchi wa kijijini atachukuliwa na ndugu yake atakuja atapimwa *CD4 count* au ataambiwa *machine* imekufa, anaondoka anarudi kijijini, *next time* hana pesa ya kupanda basi. Ninatoa mfano wa Morogoro, kutoka Kisaki mpaka afike hospitali kubwa ya Mkao aweze kuja kupimwa *CD4*, aende kwenye darasa la wiki mbili na huyo mtu anaumwa, *mind you* na ni mtu ambaye kipato chake ni kidogo, ninaomba Serikali yetu iangalie namna ya ku-focus upya utoaji wa *ARV* kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine; wananchi wanalamika wanasema taifa letu linatupenda, linatupa dawa, hasa wale wa mijini wanajulikana kwamba wengi wao ni maskini, hawana hela ya kununua chakula. Ninaomba Serikali pia iangalie namna ambavyo tunaweza kutoa lishe angalau *the cheapest* ya mahindi lishe, ambayo sasa hivi yanapatikana nchini kwenye Shirika la *Tanseed Limited* yanagawa, yale yana *protein* na *vitamins* 80%. Sasa yale tumeyatumia sisi Morogoro na tumeoana yanasaidia watoto wanaoishi na virusi vya UKIMWI, pamoja na wale ambao wameathirika wanaotumia dawa, wanaweza sasa wakapata unafuu kidogo wa maisha, wakaendelea kwenda kuzichukua zile dawa, wasiishie kati kati, tukaanza kujenga *generation* ya watu ambao wana virusi ambavyo havitasikia dawa, virusi sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na utoaji wa hizo dawa, ningependa kuzungumzia *access* au upatikanaji wa tiba wakati mwathirika anaumwa maradhi mengine, ambayo yanatokana na kinga yake kwenda chini. Mpaka mtu mwenye virusi vya UKIMWI agundulike kwamba ana *TB* ambayo ingetibiwa mapema, huyu mtu angeishi vizuri, inakuwa ni ngoma. Kwa nini inakuwa ngoma ni lazima achangie kupima kwenye *X-Ray* kwa sababu kwanza kukimbia kwenda kuomba kibali tu usamehewe, itakuchukua hata wiki moja/mbili; utakuwa umeshakufa. Ninaomba Serikali pale ambapo inasema kwamba waathirika watapata tiba bure katika hospitali zetu, basi wapewe vibali ambavyo kila atanapoumwa atakwenda hospitali, hatakuwa anakimbia tena kwenda kwa Afisa Ustawi wa Jamii kule hospitalini kuomba kila wakati aweze kupata kile kibali. Ninaomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie juu ya *confidentiality*. Kwa sasa hivi Watanzania wanaelewa dalili zote za ugonjwa wa UKIMWI. Sasa kwa njia hii tunaposema mtu atakayetoa siri ataadhidiwa, wale wahudumu ambao wanatoa ushauri nasaha na kupima watu, wanaweza wakaanza kusingiziwa mambo mengi kwa sababu *by the time* mtu anakuja, watu kwenye jamii wameshamwona amedhoofika na ana dalili zote, wanaanza kusema ana UKIMWI. Sasa wengine watasema *okay*, ngoja nikapime halafu niseme yule aliyenipima ndiye aliyenitangaza. Ninaomba hili liangaliwe namna ya kuliweka ili liweze kuwalinda wahudumu wetu wa afya hospitalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie lingine kuhusu kampeni yetu ya *VCT* ya kupima. Hili ni jambo zuri sana, lakini ninaomba niseme, mtu anaposhauriwa na kupimwa kati ya kipindi cha dakika kumi na kuambiwa, halafu anaachiwa Mwenyezi Mungu na kusononeka kwake mwenyewe rohoni hana pa kwenda, inakuwa ni ngumu. Ninaomba sasa tuweze kuangalia uwezekano wa kuweza kuweka vituo vya *Post VCT Treatment/Care and Counseling* kwa wale ambao walio wengi wanajulikana kwamba wana virusi vya UKIMWI, lakini bado *CD4 Count* yao haiwapeleki kwenda kwenye *CTC Clinic* kupata dawa za *ARV*. Hawa ni binadamu, wanahitaji kujua waende kwa nani, wazungumze naye, siyo kila mahali kuna mashirika ya kuweza kutoa ushauri nasaha. Ninaamini kwamba, kwa busara ya Wizara ya Afya na Serikali yetu, wanaweza wakaangalia namna ambavyo wanaweza wakaweka mfumo wa *Community Based Volunteers*, ambao utatusaidia kuanzisha *Post VCT Clinic* na *Support Groups* kwa hawa ambao bado wana afya wamepimwa, mwenye virusi vya UKIMWI anapokuwa na tatizo ajue atakwenda kwa nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaomba kuzungumzia watoto wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Hawa watoto wasiangaliwe kama wale watu wazima, wengine wameshapoteza wazazi wao, wanaishi na bibi zao au wanaishi kwa mtu aliyewachukua kwa mapenzi mema. Lishe yao siyo nzuri, huduma ya tiba kwa *opportunistic infections* (magonjwa nyemelezi) siyo nzuri. Hawa watoto wengine tunamshukuru Mwenyezi Mungu, wamefikia umri wa kwenda shuleni. Huyu mtoto kule shuleni anakuwa-*treated* kama mtoto mwengine. Ninaomba Wizara inayohusika, pamoja na Serikali itoe tamko kwamba, hawa watoto waweze kupata huduma maalum kule shuleni, waweze kupata angalau uji. Kila shule ambayo inajua ina watoto wa aina hiyo, ilazimike kuwa na mshauri nasaha, ambaye atakuwa anawashauri hawa watoto, kufuutilia *welfare* yao na kuhakikisha kwamba, angalau wanapata hata kikombe cha uji wa ishe.

Watoto hawa wana haki ya kusoma na wana haki ya kuishi vizuri, lakini kwa bahati mbaya, wamezaliwa na virusi vya UKIMWI. Wengine wameanza kwenda sekondari, sasa zile sekondari zetu za Kata nyingine ziko mbali, wanatembea mwendo mrefu. Ninaomba Wizara ya Elimu, iangalie namna ambavyo watoto hawa wanawenza wakasaidiwa wakaenda kwenye shule za *boarding* ili waweze ku-*maintain* na kuboresha afya zao, wasome kama watoto wengine. Hilo ni ombi maalum, licha ya kwamba kila siku wanafukuzwa shule kwa michango midogo midogo, hakuna anayeangalia hilo. Mtoto unamkuta anakimbia kabisa anatafuta niende kwa Mbunge, niende kwa kiongozi wa dini nikamweleze kwamba, nimefukuzwa shule kwa sasabu kulikuwa na mchango wa shilingi 200 shuleni au mchango wa mwenge na kadhalika.

Ninaomba, hawa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ni watoto ambaa hata kama wanakaa na msamaria mwema, yule msamaria mwema ana watoto wake anawatunza na hawa wa ziada. Ninaomba hayo yaangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine sasa kwenye hizi Kamati zetu za MVCC, wamesahaulika na unapouliza unaambiwa huyu anaishi na bibi yake ambaye ana ng'ombe wawili. Mimi ninaomba Halmashauri sasa zetu zipewe msisitizo maalum kwamba, hao watoto wafuatiliwe hata kama hawakuwekwa kwenye orodha, basi kuwepo na *provision* ya kuwaweka kwenye orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. Asante. (*Makofsi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, waliobakia yupo Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Maulida A. Komu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba na Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini. Tutaendelea kesho asubuhi, baada ya kipindi cha maswali na orodha imefungwa kusudi Waziri aanze kujibu na tuufunge Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwapongeze kwa kazi za leo. Ninaahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa
Tarehe 1 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*